**9 APRILI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Tano – Tarehe 9 Aprili, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE:**

**KIAPO CHA UAMINIFU NA AHADI YA UZALENDO KWA WABUNGE**

Mhe. Angela Charles Kizigha
Mhe. Dkt. Evaline Wilbard Munisi

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliotajwa hapo juu waliapa Kiapo cha Uaminifu na Kutoa Ahadi ya Uzalendo)*

**SPIKA:** Katibu.

**9 APRILI, 2026**

**NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Maswali kwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu. Tunaanza na Mheshimiwa Arif Premji. *(Makofi)*

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukizingatia Sheria ya Uwekezaji Tanzania *(Tanzania Investment and Specia Economic Zones)* ya mwaka 2025, mradi wa *LNG* wa Kusini ni kipaumbele cha Taifa kuanzia mwaka 2014, na sasa hivi ni miaka takribani 12 imeshapita.

Mheshimiwa Spika, ni zuio lipi la kisheria au la kisera ambalo linasababisha mradi huo usitekelezwe? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza Mbunge kwa kufuatilia jambo hilo kubwa lenye maslahi mapana kwa nchi yetu. Mradi anaouulizia ni mradi mkubwa zaidi kuwahi kutokea kwenye mpangilio wa nchi yetu ambao ni wa takribani dola za Kimarekani bilioni 42, shilingi za Kitanzania trilioni 100. Huu ni mradi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba hakuna zuio la kisheria wala kikanuni linalofanya mradi huo usitekelezwe. Kinachofanyika ni masuala ya majadiliano, kwa kutambua ukubwa wa mradi huo na kwamba nchi yetu haijawahi kuingia kwenye uwekezaji mkubwa kama huo, tuliona kwa kweli ili kuweza kuitendea haki nchi yetu na rasilimali zilizopo ndani ya nchi yetu, ni vyema Serikali ikawa makini katika kila kipengele cha majadiliano ili kuweza kulinda maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, neno la faraja kwa Mbunge na Bunge lako Tukufu ni kwamba majadiliano yanaendelea vizuri na yapo hatua nzuri na yanasonga mbele na yanaelekea kuhitimishwa, na ni vipengele vichache ambavyo bado vipo kwenye hatua ya

umaliziaji wa majadiliano ili kuweza kuhakikisha kwamba sasa tunaenda kwenye utekelezaji wa mradi huo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, vipengele ambavyo vilikuwa vinajadiliwa ni vingi, lakini baadhi tu ambavyo tulikuwa tunatamani kama nchi, lazima pia viangaliwe pamoja na yale mengine makubwa. Baadhi ya vipengele vingine ambavyo navyo tuliona tuviangalie ni lazima iwepo angalau asilimia tatu ama zaidi ya gesi itakayozalishwa itumike ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mwanzoni mapendekezo yaliyokuwa yamewekwa mezani, ilikuwa ishafanyika uwekezaji gesi iende nje. Sasa lile tuliona kama nchi, na mabadiliko ya dunia yanayoendelea kila siku, lazima pia pawe na gesi ambayo itatumika kwa matumizi ya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, lingine tuliona lazima pawe na ushiriki wa makampuni ya kizawa. Mara zote Rais amekuwa akielekeza kwamba ili tujenge uchumi ulio imara na *tax base* pana, ni lazima tuyajengee uwezo makampuni ya kizawa. Kwa hiyo, hilo na lenyewe lilikuwa moja ya jambo ambalo ilikuwa lazima lizingatiwe katika makubaliano yatakayofanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jambo hili ni kubwa, Bunge litakapokuwa limekamilika tutaendelea kutoa taarifa hata hapa Bungeni ili kuweza kuhakikisha kwamba, Bunge lako Tukufu nalo linajua kwamba nini Serikali inafanya kwenye jambo hili kubwa.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo.

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa. Kwa mujibu wa takwimu mbalimbali za Kitaifa, kati ya vijana 600,000 hadi vijana milioni moja wanaingia katika soko la ajira kila mwaka, huku ajira zinazozalishwa zikiwa hazina uwiano mkubwa na vijana wanaoingia katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha vijana kuwekeza na kuwaunganisha na

wawekezaji mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kukuza wigo wa ajira zao? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mbunge wa Vijana kwa kuleta swali zuri sana ambalo linagusa maslahi mapana ya vijana na linagusa ajenda kubwa ya ajira kwa vijana ambayo ni ajenda ya dunia, siyo tu ni ajenda ya Tanzania, ni ajenda ya dunia.

Mheshimiwa Spika, jambo alilosema ni kweli kwamba vijana wengi wanaingia katika soko la ajira, duniani na hapa nchini kwetu. Zamani ilikuwa vijana wakiwa bado wako kwenye masomo tu, wakiwa wamemaliza *middle school*, wanaelekea vyuo na wengine wakiwa vyuoni walikuwa wanapokea barua za kuambiwa wachague kazi wanazotaka kwenda kufanya, wanakuwa na barua moja, mbili, tatu achague kazi, lakini kwa sasa siyo jambo la ajabu kukuta mstaafu yuko na *graduates* wawili, watatu wakiwa tegemezi kwake. Kwa hiyo, ni jambo kubwa, hii ni ajenda kubwa ambayo Mbunge ameileta.

Mheshimiwa Spika, Mbunge amesema Serikali ina mkakati gani? Moja, ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2025/2030 kutengeneza ajira zipatazo zaidi ya milioni nane. Hili siyo andiko tu la Ilani, ni andiko ambalo limewekwa kwenye mikakati ya utekelezaji, ikiwemo mipango ya mwaka mmoja mmoja na ile mipango ya miaka mitano mitano ambayo ipo kwenye Dira ya Taifa ya 2050.

Mheshimiwa Spika, lile pato tunaloliongelea la takribani dola trilioni moja ifikapo 2050, tunatarajia mchango mkubwa utoke kwa vijana. Vijana hawa tunaandaa mazingira bora ambayo yatawawezesha kupata ajira ndani ya sekta ya umma pia kwa wingi katika sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vitu gani tunavyovifanya? Tayari tumepitisha kwenye sheria, Sheria ya Uwekezaji (Na. 6) ya Mwaka 2025, ambapo sasa vijana wanaweza kunufaika na zile *incentives*

ambazo walikuwa wanapata wawekezaji wakubwa. Sasa tumepeleka, kwamba hata vijana wa Kitanzania wakishapata cheti kile cha *TISEZA*, wanaweza wakanufaika na vile vivutio ambavyo wawekezaji wakubwa walikuwa wanapata.

Mheshimiwa Spika, ni nini tunaongelea hapo? Wataweza kupata ardhi, wataweza kupata punguzo kwenye masuala ya kodi, ushuru pamoja na tozo mbalimbali, pia kwenye yale madirisha ambayo wawekezaji wakubwa walikuwa wanapata, sasa tumefungua, vijana na wenyewe wanaweza wakapata fursa hizo.

Mheshimiwa Spika, dirisha la kuwanufaisha na masuala ya viwanda, dirisha la kuwanufaisha na masuala ya kupata masoko, pia dirisha la kuwauganisha na taasisi za kifedha ambalo na lenyewe lilikuwa moja ya jambo kubwa linalowakwamisha vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, Rais ameunda Wizara mpya ambayo inashughulika na masuala ya vijana, tena iko Ofisi ya Rais. Wizara hii hajaiunda tu ili ipate Waziri, kuna maelekezo ambayo ameyatoa ya kufanyia kazi, ambayo tayari tumeshaanza kufanya kazi kwa kushirikiana na Wizara hiyo ya Vijana ambapo tunataka vijana hawa wanufaike na fursa zinazojitokeza.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya fursa ambazo zinajitokeza ni pamoja na Serikali kufungua lile dirisha la *export guarantee scheme,* ambapo ndani ya mwaka huu tunatarajia dirisha hilo la kutoa dhamana kwa vijana wanaokosa dhamana lianze kutumika kwa ukubwa wake, ambapo sasa itakuwa kampuni ya kutoa dhamana kwa vijana ambapo vijana wengi wataweza kunufaika zaidi na dirisha hilo la kuweza kupata dhamana, ambapo tayari hivi tunavyoongea ndani ya Benki Kuu ya Tanzania kuna shilingi bilioni 280 ambazo zimewekwa kwa ajili ya kutumika kama dhamana kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ambalo Mbunge ameliongea, mimi ni mmoja wa watu ambao nimeliishi nilipomaliza Chuo Kikuu,

nilifanya kazi za kubeba zege na kufyatua tofali na mke wangu akifanya kazi ya Mama Lishe. Kwa hiyo, najua adha ya kijana kukosa ajira.

Mheshimiwa Spika, tumeshaanza hata kuongea kwamba vijana wanapata mikopo wakiwa kwenye masomo, wakimaliza wanapata vyeti vyao vile, wanahangaika kupata mikopo kwa sababu hawana dhamana.

Mheshimiwa Spika, tumeanza kuwaza kupitia maelekezo yale ambayo Rais aliyaelekeza kutafuta namna ya kuwakwamua vijana hawa. Tumeanza kuwaza kwamba kijana aweze kutumia cheti chake kile alichohitimu kuweza kukopa. Kama kamaliza Phamasia na imejulikana amemaliza phamasia aweze kutumia cheti chake kile kukopa aanzishe *Pharmacy*. Kama amemaliza uhandisi, na ana cheti chake cha uhandisi, anahitaji vifaa vya umeme, aweze kutumia cheti chake kama dhamana aweze kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo hili tutalileta hapa Bungeni tutakapokuwa tumemaliza hiyo sheria ambayo tunataka itengeneze kampuni ya kutoa dhamana, pia kuweka dhamana mali ambazo zinaweza zikahamishika.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, hili ni swali zuri, na Serikali inalifanyia kazi kwa ukubwa wa ajenda hiyo ya ajira kwa vijana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali.

*(Hapa Mhe. Nassriya Nassir Ali aliuliza swali kupitia mtaalamu wa lugha ya alama)*

**MHE. NASSRIYA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote, ninaomba ridhaa yako niweze kutumia mkalimani wa lugha ya alama wakati nauliza swali kwa Waziri Mkuu. Unaniruhusu niweze kukaa?

**SPIKA:** Unaweza kukaa.

**MHE. NASSRIYA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Spika, ninafurahi kupata nafasi ya kuuliza swali la moja kwa moja kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika elimu hapa nchini, lakini pia Serikali imeweza kujenga miundombinu bora ya elimu hapa Tanzania, ikiwemo madarasa. Pia kumekuwa na uhitaji wa madarasa hususan kwa watu wenye ulemavu, je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha haya madarasa ya watu wenye ulemavu pamoja na miundombinu katika shule za wilaya na mikoa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kulileta swali zuri ambalo linagusa watu wengi katika jamii yetu ya Tanzania na dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuzingatia miundombinu ambayo inajumuisha watoto wa Kitanzania wenye mahitaji maalumu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ametoka kuulizia.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoongea, Serikali imekuwa ikiboresha baadhi ya shule ambazo hazikuwa na miundombinu hiyo na kuzingatia katika ujenzi wa shule hizi mpya, kwamba, ni lazima pawe na miundombinu rafiki ambayo inazingatia mahitaji maalumu ya watoto wa Kitanzania ambao wana uhitaji wa miundombinu iliyo rafiki.

Mheshimiwa Spika, nimetembea mikoa mbalimbali, na kila shule ambazo nimezitembelea, nimekuta zimewekewa utaratibu huo wa miundombinu ambayo ni rafiki kwa watoto wenye mahitaji maalumu katika miundombinu hiyo. Tunavyoongea, tuna takribani shule zaidi ya 7,600 ambazo ni jumuishi, zinazingatia mahitaji maalumu kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalumu.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni katika miaka minne iliyopita Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amejenga shule 26 maalumu kwa ajili ya watoto wa kike. Katika shule hizo zote 26 maalumu kwa ajili ya wasichana zimezingatia pia watoto wenye mahitaji maalumu. Kwa ujumla, kwa shule za sekondari zipo shule 54 ambazo zimezingatia mahitaji maalumu ya watoto ambao wanahitaji miundombinu mahsusi kwa ajili ya watoto wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, zipo shule sasa ambazo zinajengwa mahsusi kwamba ni shule maalumu kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalumu. Kuna shule moja ninadhani inajengwa kule Chato, pale Mbuye. Pia kuna shule nyingine inajengwa Mkoa wa Mbeya ambayo nayo itakuwa maalumu kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalumu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuzingatia uhitaji wa miundombinu rafiki kwa watoto wenye mahitaji maalumu pamoja na uwekezaji kwa walimu watakaokuwa wanawafundisha watoto hao kulingana na mahitaji yanayotakiwa kwa wanafunzi wenye uhitaji huo mahsusi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante. Mheshimiwa Agnesta Kaiza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi siku ya leo niweze kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali chini ya Wizara ya TAMISEMI inatekeleza sera yake ya elimu bila ada kwa shule za umma kwa maana ya kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili, ninaomba niipongeze sana Serikali kwa jinsi ambavyo imeona mbali sana kwa kumpa thamani mtoto wa Kitanzania, mtoto wa mzazi mnyonge ambaye kwa hali ya kawaida wasingeweza kuwapeleka watoto wao mashuleni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hii nia njema ya Serikali, ipo changamoto kubwa sana inayowakumba wazazi pamoja na watoto hawa. Changamoto hiyo ni michango isiyokuwa rasmi, michango holela ya shuleni.

Mheshimiwa Spika, ninatambua kwamba suala la watoto la shuleni ni jukumu la wazazi, hilo halina tatizo, lakini hii michango ya mara kwa mara, kwa mfano, unaambiwa kila mtoto kwa siku ni lazima aende na shilingi 1,500/= kwa ajili ya *speed test*. Sambamba na hilo, watoto wanaambiwa kila siku ya Alhamisi waende na shilingi 3,500/= kwa ajili ya kufanya mitihani saba kwa pamoja, yaani mitihani ya masomo saba kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, nia na dhamira njema ya Serikali ya kuleta sera hii ya elimu bila malipo ilikuwa ni kwa ajili ya kuhakikisha watoto wote wa wanyonge wanapata elimu hii ya msingi ya darasa la kwanza mpaka ya kidato cha nne.

Mheshimiwa Spika, sasa, chini ya waraka namba tatu wa mwaka 2016, ningeomba kufahamu, nini kauli ya Serikali juu ya shule hizi na kwa walimu hawa ambao wameleta mfumo kana kwamba sasa ni kausha damu kwa wazazi? Wanawakausha damu wazazi kwa kuwalazimisha waweze kupeleka hii michango ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, mfano mzazi mwenye watoto watano, kwa sababu anajua hakuna ada, ni suala la madaftari, ni suala la *uniform* na chakula wamewapeleka watoto kwa kasi kubwa sana. Unakuta, mzazi mmoja ana watoto watano, chukua 1,500 x siku tano...

**SPIKA:** Mheshimiwa twende kwenye swali lako, twende kwenye swali.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, swali langu, ninaomba kupata kauli ya Serikali juu ya kukomesha hii dhana ya michango holela shuleni ambayo inaathiri kabisa utekelezaji wa sera hii ya elimu bila malipo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri. Alichokisema ni kweli kwamba katika baadhi ya maeneo kumekuwepo na michango ambayo inaondoa ile maana halisi ya elimu bila ada. Ni kweli pia michango hiyo ikiwa mingi ina athari kwa watoto na wazazi na familia hizo hasa familia ambazo hazijiwezi.

Mheshimiwa Spika, ninasema ni kweli kwa sababu nilipokuwa ziara katika Mkoa wa Katavi, alikuja mama mmoja kati ya wananchi waliouliza maswali, akasema mwanaye amekosa masomo kwa takribani miezi miwili, inaenda mitatu kwa sababu aliambiwa asiende shule mpaka aende na mchango wa takribani shilingi 50,000 ambalo ni jambo baya mtoto kukosa masomo kwa sababu mzazi wake amekosa michango.

Mheshimiwa Spika, nilielekeza mtoto yule arudishwe shuleni, na nimpongeze Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa amenipatia taarifa kwamba yule mtoto alirudishwa shuleni. Nilielekeza mamlaka zinazohusika na masuala ya nidhamu kwa walimu wetu, wamwite yule Mwalimu Mkuu kwa uzembe huo, kwamba mtoto amekosa masomo, hakuwepo shuleni muda wote ule na wao wakaendelea na maisha kama vile hakuna kitu kilichotokea, na lenyewe hilo tutaendelea kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameweka wazi kwamba yapo mambo ambayo ni ya msingi, nami ninawapongeza walimu, katika maeneo mengi wamefanya hivyo kwa nia njema ya kutaka watoto wafanye vizuri.

Mheshimiwa Spika, bila kwenda moja kwa moja tu kwenye eneo hilo ambalo pengine limepitiliza na kuleta athari, lakini pia tutambue walimu wamejitoa sana katika baadhi ya maeneo kwa *initiatives* zao kuhakikisha watoto wa Kitanzania wanafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu linatambua kwamba kwa wingi wa watoto ambao wameendelea kuongezeka kwa vipindi tofauti, ikiwemo kutokana na hii sera ya elimu bila ada

pamoja na *re-entry programs* ambazo zililetwa, imesababisha katika baadhi ya maeneo uwiano wa walimu kwa wanafunzi haupo sawa. Kwa hiyo, walimu wanajitahidi, wale wale kwa uchache wao, ili kuhakikisha kwamba watoto wana-*cover syllabus* zote zile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niende tu kwenye hoja hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ametoa; nimetoa waraka ambao unatoa miongozo ya masuala yanayohusu michango. Moja ya michango ambayo tunakubalina nayo ni endapo tutataka watoto wapate chakula shuleni. Tukasema hata wangekuwa nyumbani wangepata chakula, *anyway.* kwa hiyo tukasema hili siyo jambo linaloleta mzozo, na hata katika baadhi ya maeneo hawajaona kama ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, michango mingine ambayo inapitiliza, tumesema ni lazima ifuate mwongozo na iwe na ukomo. Maeneo haya tumeshawaelekeza Wakuu wa Mikoa, tumewaelekeza Makatibu Tawala wa Mikoa na tumetoa waraka ambao unaenda sambamba na waraka huo ambao Mheshimiwa Mbunge ameunukuu.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa yanajitokeza, shule zetu hizi zinakuwa na walimu wanaojitolea na walimu wale wanalazimika walipwe nje ya utaratibu ule wa walimu walioajiriwa. Nimeelekeza halmashauri zote ziweke bajeti ya mapato ya ndani, kuweza kuhakikisha kwamba walimu wale ambao wanawaongezea kwa ajili ya kuwafundisha watoto wetu, walipwe kutoka katika vyanzo vile, kwa sababu wazo lenyewe la kuwa na walimu wa kutosheleza ni wazo zuri.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hata sisi hapa Waheshimiwa Wabunge mnakumbuka kuna wakati enzi zile kulikuwepo na utaratibu wa *tuition.* Wakati mwingine tulikuwa tunamwelewa mwalimu wa *tuition* kuliko yule anayefundisha pale darasani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wazo la kuwa na walimu wanaojitolea siyo jambo baya, lakini walimu hawa hawapaswi sasa kulipwa na wazazi. Nchi yetu haijataka wazazi kuajiri walimu kwa ajili ya watoto wao. Kwa hiyo, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, pale ambapo pana uhitaji huo, wajiratibu, watumie mapato ya ndani kuweza kuhakikisha kwamba, badala ya kwenda kwenye michango, watumie mapato ya ndani kuweza kuhakikisha wana-*cover* masuala ya aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia kwa kuwa tunaenda kwenye utekelezaji wa mitaala mipya, mahitaji yanaendelea kuongezeka katika kumwezesha mtoto aweze kusoma vizuri. Kwa hiyo, tutaendelea kuboresha pia bajeti ya Serikali, kwa sababu kingine kinachosababisha haya ni ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuboresha bajeti ya Serikali kwenda kwenye sekta zetu za elimu ili kuweza kuhakikisha kwamba shule zetu hizi zinajitosheleza kibajeti ili kuweza kutimiza yale malengo ambayo walimu wanataka wafanye kwa ajili ya kuwawezesha watoto kuelewa na kufaulu vizuri masomo yao.

**SPIKA**: Ahsante. Mheshimiwa Isack Copriano.

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupata nafasi ya kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ziara za Mheshimiwa Waziri Mkuu, hususan nchini, amekuwa ukipokea kero mbalimbali kutoka kwa watu binafsi na wananchi. Kero hizi nyingine zimekuwa zikipata majibu ya papo kwa papo na nyingine hazipati majibu, na kwenye ile timu ya tathmini ya ufuatiliaji majibu mengine ni hafifu. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha timu ya tathmini na ufuatiliaji ili kuharakisha na kupata majibu ya kero za wananchi hawa kwa wakati, hususan wananchi wa vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri na hasa hasa akinukuu mambo

yanayojitokeza kwenye ziara. Nikiri, kwamba nilikwenda jimboni kwake pale Mto wa Mbu, Monduli, nilikuta wananchi wengi sana wamekusanyika wakiwa na masuala yao ambayo yanahitaji kupata majibu ya Serikali. Serikali itaendelea kuimarisha vitengo vyetu vya tathmini.

Mheshimiwa Spika, kama unavyotambua kwamba, kila Wizara ina vitengo vyetu hivi vya ufuatiliaji na tathmini, tunapanga kuendelea kuviboresha, kuongeza bajeti ili viweze kutimiza wajibu wao wa masuala ya ufuatiliaji wa miradi, lakini pia na ufuatiliaji wa masuala yote yanayohusu uendeshaji wa Serikali, na shughuli nzima za kila siku za Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali imeendelea kuboresha utaratibu wa tathmini na ufuatiliaji, na hasa namna ya kufanya *engagement* na wananchi wetu. Tumekwenda kwenye utumiaji wa mifumo ili katika baadhi ya maeneo ambapo wananchi wanaweza wakatumia mifumo waweze pia na wenyewe kuweza kupeleka hoja zao na kupata mrejesho wa hoja hizo ambazo wamezipeleka kupitia *e-Mrejesho*, ambapo kila Wizara sasa ina hiyo *platform* ya *e-Mrejesho,* ambapo umeona katika baadhi ya Wizara, kazi hiyo inaendelea ikiwa inaongozwa na Wizara yetu ya Ofisi ya Rais, Utumishi.

Mheshimiwa Spika, nimeshaona pia Wizara za Kisekta, nimeona kwenye Afya wakitumia dirisha hilo la Ongea na Waziri, na Wizara nyingine zote hata Ofisi ya Waziri Mkuu na sisi tumeshatengeneza hiyo *dashboard* ambayo tutakuwa tunaendelea kufanya ufuatiliaji, na kupeleka mirejesho kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali imeanzisha *Call Centre,* ambapo itakuwa ni *National Call Centre,* ninadhani *Centre Number* 190, ambapo mwananchi anaweza akaongea kwa simu ama akaongea kwa ujumbe mfupi kwa kutumia simu zote; simu janja na simu za kawaida, ili kuweza kupeleka hoja yake na aweze kupata majibu.

Mheshimiwa Spika, kingine, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu, kwamba usikilizaji huu wa kero haitakuwa jambo la ziara tu, tumeimarisha utaratibu ambao sasa tutataka kila mwezi pawe na jedwali linaloonesha ni mwananchi gani alifika katika ofisi ya Serikali? Alienda na hoja gani? Ile hoja imetekelezwaje katika ngazi ambayo mwananchi aliipeleka?

Mheshimiwa Spika, kama ni ngazi ya kijiji watasema walipokea hoja kutoka kwa mwananchi gani, inahusu kitu gani? Namba yake ya simu ni ipi? Wameitatua namna gani? Ama kama hawajaitatua, tunataka turejeshe utaratibu wa kiongozi wa Serikali kubeba hoja ya wananchi kuipeleka katika ngazi inayohusika badala ya utaratibu ambao umeanza kuzoeleka wa kila mwananchi kuhangaika yeye mwenyewe kupambana kutafuta kupeleka hoja katika ngazi ya juu ilhali Serikali imeshapokea hoja hiyo katika ngazi zinazohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaratibu huu tutaendelea kupokea taarifa zake za kila mwezi, za kila ngazi. Hapo ndipo tutakapoanza kupimana kwa utekelezaji wa majukumu yanayohusu wananchi badala kupimana kwa kukaa sana ofisini, kwamba huyu ameshakaa miaka kadhaa anastahili kupandishwa daraja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana tunakushukuru sana kwa majibu mazuri. Muda wetu wa maswali kwa Waziri Mkuu umekwisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa, sasa tuna kikao kingine, hivyo ninamwita Mwenyekiti, Mheshimiwa Najma, aendelee na kikao.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma M. Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na maswali ya kawaida. Tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jasmine Chesco Ng'umbi, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 36

**Ajira kwa Vijana**

**MHE. JASMINE C. NG'UMBI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha vijana wanapata ajira katika miradi mikubwa kama *SGR* na viwanja vya ndege?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasmine Chesco Ng'umbi, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza sera na sheria mbalimbali zinazolenga kuhakikisha kuwa miradi mikubwa inatoa fursa za ajira kwa Watanzania. Miongoni mwa sera na sheria hizo ni pamoja na Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008, Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2015, Sheria ya Mafuta, Sura 392 pamoja na Sheria ya Madini, Sura 123.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia miradi mikubwa inayotekelezwa nchini, vijana wananufaika na fursa za ajira katika sekta mbalimbali. Kwa mfano, zaidi ya ajira 35,000 zimetolewa

katika ujenzi wa reli ya *SGR*, zaidi ya ajira 10,000 katika mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, na zaidi ya ajira 2,497 zimetolewa katika ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, Dodoma na upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, zaidi ya ajira 1,500 zimetolewa katika ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi, na zaidi ya ajira 3,000 katika upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam. Vilevile, Serikali inahakikisha kuwa vijana wanapata ujuzi unaohitajika katika miradi hii kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi, inayowawezesha vijana kupata ajira na kushiriki kwa ufanisi katika kazi za viwandani na miradi mikubwa ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jasmine Chesco Ng'umbi.

**MHE. JASMINE C. NG'UMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza ninakushukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini niendelee kuipongeza Serikali yetu kwa uwekezaji mkubwa unaofanyika katika miradi mikubwa ya kimkakati, lakini nilikuwa nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza; kama Mheshimiwa Waziri alivyojibu, ni kuwa vijana hawa wanapata ajira, lakini pia wanapata ujuzi. Sasa nilitamani kujua baada ya hawa vijana kupata ujuzi kwenye hiyo miradi mikubwa ya kimkakati kama miradi ya kujenga viwanja vya ndege pamoja na miradi ya *SGR* yaani miradi ya reli, maana hii miradi sote tunajua ni miradi ya kimkakati na ni miradi ya muda mfupi, siyo miradi endelevu, je, baada ya hapo, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wanaendelea kubaki na ujuzi na kuutumia katika hiyo miradi mikubwa ya kimkakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Ninatambua kuwa sisi vijana tunasaidiwa sana na tunaangaliwa sana katika suala la ajira. Je, ni kwa namna gani Serikali yetu imejipanga kuwasaidia vijana hawa wapate ajira kwa kuangalia suala zima la

jinsia? Kwa maana tunaona na tuna imani kuwa vijana wa kike na vijana wa kiume wote wanapata haki sawa; kama ni kusoma, wote tunasoma sawa, lakini linapofika suala la ajira, unaweza ukaona vijana wa kiume ndiyo wanapata ajira zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha na jinsia Ke (vijana wa kike) kama mimi niliyesimama hapa nao wanapata ajira, lakini pia kama tunavyomwona Mheshimiwa Waziri anayejibu swali naye ni kijana, na ni binti kama sisi. Ninaomba kujua Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha vijana jinsia Ke, nao wanapata ajira kama jinsia Me? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu maswali mazuri ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Jasmine kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi mikubwa ya kimkakati Serikali imeweka sharti la *Local Contents* ili kuhakikisha vijana wa Kitanzania wanapewa nafasi ya kujifunza na kuendeleza ujuzi hususan urithishaji wa ujuzi na teknolojia kutoka kwa wataalamu wa kigeni wanaofanya kazi adimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tukitekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati panakuwepo na ubia kati ya wawekezaji wa makampuni Kitanzania ili Watanzania waweze kuajiriwa katika miradi mipya na kutumia ujuzi tulioupata kwenye miradi mingine na kuboresha huduma zinazotolewa kwa vijana ambao wananufaika na fursa hizo za ajira na kuendelea kuboresha ujuzi waliokuwanao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba wavulana hawapewi nafasi zaidi kushinda wanawake, hakuna kitu kama hicho Mheshimiwa Mbunge. Fursa za ajira hutolewa nchini bila ubaguzi wa kijinsia. Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (Na. 6) ya Mwaka 2004,

inakataza ubaguzi wa kijinsia, na inataka waajiri kutoa fursa sawa kwa wote bila kujali jinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inasisitiza kuwa wafanyakazi wa jinsia tofauti wanaofanya kazi zinazofanana na zinazoshabihiana, kama upandaji wa vyeo na vipaumbele vyote viende sawa kwa wote kupewa fursa sawa. Hivyo, Serikali kupitia Maafisa Kazi Wafawidhi wa Mikoa hufanya ukaguzi katika maeneo ya kazi ili kuhakikisha waajiri wanatekeleza Sheria ya Masuala ya Kazi, ikiwemo suala la ubaguzi wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa zile shilingi bilioni 200 kwa vijana. Vijana wana mfuko wao pia, lakini pia halmashauri zetu zimekuwa na pesa kwa ajili ya uwezeshwaji wa vijana. Je, ni uelewa na elimu kiasi gani inatolewa kwa vijana wakiwemo wa vijijini mpaka kule Kilolo ili hizi pesa ziweze kuwafikia ili vijana sasa waanzishe makampuni hasa wasomi waweze kuwaajiri na vijana wengine? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, umemwelewa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Vijana, tumeendelea kutoa elimu kupitia makongamano, maadhimisho na kwa vijana wa vijijini tunaendelea kuwabandikia matangazo katika ofisi za watendaji kata ili kuweza kujua fursa na mikopo inayoendelea ambayo Serikali imekuwa ikiwapatia vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Chamazi aulize swali lake.

Na. 37

**Ujenzi wa Barabara Kata ya Kilungule**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga barabara katika eneo la Kwa Mwarabu, Kata ya Kilungule ili kuondoa adha ya usafiri kwa Wananchi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa leo ni siku yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, naomba kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim aliyenijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba nitumie fursa hii kwa dhati ya moyo wangu kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani hii kubwa aliyonipa ya dhamana ya kuwatumika Watanzania wenzangu katika nafasi ya Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nitumie nafasi hii

kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na niwaahidi viongozi hawa wakuu kwamba nitafanya kazi kwa juhudi, maarifa na weledi wa hali ya juu kwa kadiri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushirikiano nikiwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, na niwahakikishie nitaendelea kuwapa ushirikiano katika Ofisi hii ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Injinia Hamad Yussuf Masauni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa malezi yake na uongozi wake mzuri, na nimshukuru sana Mheshimiwa Prof. Riziki Shemdoe, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa kunipokea, lakini pia kwa miongozo ambayo tayari ameanza kunipatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Wanging'ombe kwa imani yao kwangu na niwahakikishie kwamba nitaendelea kuchapa kazi kuhakikisha tunapeleka maendeleo katika jimbo la Wanging'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya machache ya shukurani, sasa naomba kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI nijibu swali la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Jimbo la Chamazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kilungule inajumuisha eneo la Kwa Mwarabu katika Manispaa ya Temeke yenye urefu wa kilometa 0.88. Barabara hii katika eneo la Kwa Mwarabu ina changamoto ya kutuama kwa maji msimu wa mvua na hivyo kupelekea kuwa na madimbwi makubwa na kutopitika kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa adha ya usafiri kwa wananchi, Serikali katika bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 imetenga jumla ya shilingi milioni 165.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Kwa Mwarabu kwa awamu, ambapo awamu ya kwanza ya ujenzi itahusisha ujenzi wa mita 200 kwa kiwango cha zege. Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu ili kuboresha barabara hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wa Kwa Mwarabu wamekuwa wakiteseka kwa zaidi ya miaka 10 kwa kukosa mawasiliano ya barabara, je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuhakikisha barabara hiyo inapitika hasa kipindi hiki cha mvua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Barabara ya Kontena Alfurkan mpaka kwa Mnyani iliyopo katika Mtaa wa Kwa Mzungu na Uzombokoni, imekatika na hivyo kukosekana kwa mawasiliano kati ya upande mmoja na upande wa pili. Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha eneo hilo la Alfurkan ili barabara hiyo iweze kupitika na kupunguza gharama ya maisha kwa wananchi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, Mbunge wa Jimbo la Chamazi kwa namna ambavyo mara kwa mara ameendelea kuwasemea wananchi wa Jimbo hili; tunampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Chamazi kwamba tutaendelea kuwapa ushirikiano kuhakikisha tunapeleka miradi ya maendeleo. Ni kweli kwamba barabara hii ya Kwa Mwarabu ina changamoto ya

muda mrefu, na tunafahamu kwamba kutokana na mvua nyingi mwaka huu, barabara hii imekatika kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie, pamoja na mpango wa bajeti ya shilingi milioni 165 ya kujenga barabara hii kiwango cha lami, mwaka ujao wa fedha tunaoanza Julai, hivi sasa Serikali imeshatoa maelekezo kwa Mameneja wa *TARURA* Mikoa na wilaya kote nchini, akiwemo Meneja wa *TARURA* wa Temeke kwamba wafanye tathmini ya haraka katika barabara hii hasa eneo la Kwa Mwarabu ili tujue namna ya kupata fedha za dharura kwa ajili ya marekebisho na kuwezesha barabara hii kupitika kwa sasa wakati tunasubiri mpango kwenye bajeti ijayo ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya kwa Mzungu na Kontena, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafahamu ziko barabara ambazo ni mbovu kutokana na hali ya hewa ya mvua nyingi mwaka huu. Tutaendelea kuzifanyia tathmini na kutafuta fedha. Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweka kipaumbele cha juu sana kwenye barabara za vijijini na mijini zikiwemo barabara hizo za Temeke.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape Nnauye, swali la nyongeza.

**MHE. NAPE M. NNAUYE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, barabara nyingi zinazosimamiwa na *TARURA* na hasa za mikoa ya Pwani, kwa maana ya Pwani ukija mpaka Kusini, Lindi, Mtwara hasa katika Jimbo la Mtama, zimekatika sana baada ya kupata baraka ya mvua kubwa na kwa kuwa tunaelekea mwisho wa msimu wa mvua, kukatika kwa hizi barabara kwa bajeti za kawaida hatuwezi kuzi-*repair*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kuagiza Maafisa wa *TARURA* wafanye tathmini hasa zile barabara ambazo kwa kweli bila hizo, maisha ya watu wetu yatasimama ili itengwe bajeti ya ziada kwenda kuzi-*repair* au kuzikarabati katika

hali ambayo tunayo sasa baada ya mvua kubwa ambazo zimeendelea kunyesha nchini?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninampongeza sana Mheshimiwa Nape Moses Nnauye kwa kazi kubwa anayoifanya kwa wananchi wa Jimbo la Mtama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie, ni kweli kwamba barabara zetu za ukanda wa Pwani, Kusini, lakini kote nchini kwa ujumla kufuatia baraka ya mvua mwaka huu, barabara nyingi zimeathirika. Serikali imeweka mpango mkakati wa kufanya tathmini, na hivi ninavyoongea, Mameneja wa *TARURA* mikoa na wilaya, wanaendelea kufanya tathmini ya barabara zote muhimu kote nchini na kutambua gharama za fedha zinazohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuandaa fedha ili baada ya msimu wa mvua barabara zote ambazo ni muhimu ziweze kufanyiwa matengenezo maalum na kupitika vizuri ili kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji kwa wananchi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, barabara za Jimbo la Mtama na majimbo yote kote nchini zitapewa kipaumbele katika mpango huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab Kawawa.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika Mkoa wa Lindi, barabara ambazo zimekuwa sugu kabisa katika baadhi ya wilaya ambazo mimi nimezipata *so far*, katika Wilaya ya Kilwa, Kijiji cha Kandawale, lakini kuna daraja la Kibata limekatika kabisa, Kijiji cha Mingumbi pia barabara hazipitiki kabisa, lakini katika Wilaya ya Liwale Kata ya Nangano Kijiji cha Nahoro hakupitiki kabisa, kimekuwa kilio kikubwa hasa cha akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Mirui pia hakupitiki kabisa, na sehemu nyingine nyingi kama ambavyo Mheshimiwa Nape Nnauye, Mbunge mwenzangu anayetoka Jimbo la Mtama katika mkoa wa Lindi ameliwasilisha. Kilio cha barabara katika Mkoa wa Lindi ni kikubwa sana, wataalamu wanasema kwamba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab uliza swali

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la msingi ni kwamba madaraja yamekuwa yakikatika kwa kiwango kikubwa sana katika mkoa wetu wa Lindi hasa katika barabara za ndani, pamoja na barabara kubwa *of course* hiyo ni ya Wizara nyingine, lakini kwa nini sasa wakandarasi wetu tunaowapa hizi kazi hawajengi madaraja yaliyokuwa imara ili kuzuia uharibifu unaotokea wa barabara zetu wa mara kwa mara hasa kipindi cha mvua zinazonyesha maana katika vijiji hivi madaraja yanajengwa lakini yanakatika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninamshukuru Mheshimiwa Zainab Kawawa kwa swali hilo muhimu, lakini kwanza nianze kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi wa barabara na madaraja yetu unasimamiwa na wataalamu wenye sifa na tunafanya malipo na kuidhinisha ukamilishaji wa miradi hiyo baada ya kujiridhisha na ubora wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba mwaka huu tumepata baraka kubwa zaidi ya mvua na imekuja na madhara ya kuwa na maji mengi ambayo imepelekea kukatika kwa baadhi ya barabara na pia baadhi ya madaraja, ikiwemo Daraja la Kipati ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja na barabara za Wilaya ya Kilwa, Kusini na kote nchini kwa ujumla. Naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua kwamba barabara hizo zimekatika na madaraja hayo yamekatika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumeshaanza kupata tathmini na taarifa za gharama ambazo zinahitajika kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara hizo. Tunachosubiri sasa ni mvua zipungue, kwa sababu siyo rahisi kufanya matengenezo kipindi hiki cha mvua. Mvua zikipungua, niwahakikishie wananchi wa Kilwa na kote nchini kwamba tutakwenda kurekebisha barabara hizo ili ziweze kupitika na kurahisisha usafiri na usafirishaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salma Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote naomba niwape pole na kuwapongeza sana wananchi wangu wa Kata ya Milola. Hii ni kutokana na ahadi ya Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa ambaye alituahidi kutujengea barabara ya lami ya kilometa 4.5, lakini mpaka hivi leo hiyo barabara haijajengwa hata kilometa 0.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini mpango wa Serikali au nini mkakati wa Serikali wa kutupatia hizi fedha kwa haraka ili wananchi wale waweze kupata hiyo barabara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimpongeze sana mama yangu Mheshimiwa Salma Kikwete kwa namna ambavyo anafanya kazi kubwa ya kuwasemea wananchi wake wa Jimbo lake la Mchinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi za viongozi wetu wa Kitaifa ni kipaumbele katika bajeti zetu, na tayari tunatambua kwamba kuna ahadi ya barabara kiwango cha lami katika kata ya Milola kilometa 4.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali inaendelea na taratibu za kupata

fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa awamu ili kuweza kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu Mstaafu. Hata hivyo, hiyo pia ni dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alan Mvano.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kakonko kuna mradi wa ujenzi wa barabara ya lami kuelekea kwenye hospitali ya wilaya, na kipande kilichobakia ni mita 550 tu. Hivi karibuni mkandarasi amewasilisha hati ya kuomba malipo na na amesitisha kuendelea na shughuli, kwa hiyo, inaathiri watu kuingia hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, je, ni lini Serikali itatusaidia kupata fedha ili kuendeleza eneo lile wananchi waweze kupata nafasi ya kuingia hospitali bila kupata changamoto kama iliyopo sasa? Ninashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Alan Mvano Mbunge wa Jimbo la Kakonko, na nimhakikishie kwamba moja ya vipaumbele vya barabara zetu ni barabara ambazo zinakwenda kwenye huduma za kijamii, kama hospitali, kwenye shule na maeneo mengine ya huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba barabara ile yenye mita 550 tayari mkandarasi yupo *site,* lakini amesimama kwa muda kwa sababu anahitaji malipo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshapokea *certificate* kwa ajili ya malipo hayo. Naomba kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI nimwelekeze Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Kigoma, na wa Wilaya ya Kakonko, kufuatilia kwa karibu malipo hayo ili mkandarasi aweze kulipwa na kuendelea kukamilisha kipande hicho ili wananchi wafike katika hospitali ya wilaya kwa urahisi zaidi.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Amina Mussa Mkumba, Mbunge wa Kibiti.

Na. 38

**Ujenzi wa Stendi ya Mabasi – Kibiti**

**MHE. AMINA M. MKUMBA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Stendi Kuu ya Mabasi Kibiti?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mussa Mkumba, Mbunge wa Jimbo la Kibiti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na stendi kuu ya mabasi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti ili kuchochea uchumi na kutoa huduma bora za usafiri kwa wananchi. Katika kulishughulikia hili, Serikali imejipanga kutekeleza maboresho kwa hatua mbili, ambazo ni matengenezo ya muda mfupi na mpango wa ujenzi wa stendi mpya ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa muda mfupi, halmashauri imetenga kiasi cha shilingi milioni 21 kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Fedha hizi zitatumika kufanya matengenezo ya dharura katika stendi inayotumika sasa, ikiwemo kufukia mashimo na kuondoa kero ya maji kutuama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa muda mrefu, halmashauri imetenga kiasi cha shilingi milioni 100 katika bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 kwa ajili ya fidia na kuanza ujenzi wa stendi mpya katika Kata ya Kibiti. Tayari eneo lenye ukubwa wa ekari mbili limeshapatikana. Mara baada ya taratibu za utwaaji

wa ardhi na fidia kukamilika, Serikali itaanza mchakato wa kutafuta fedha za ujenzi kupitia vyanzo vya mapato ya ndani ya halmashauri na pia Serikali Kuu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mkumba.

**MHE. AMINA M. MKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maswali mazuri. Pia ninaipongeza sana Serikali kwa kuweza kutenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya mpango wa muda mrefu na fidia. Kwa sasa hakuna stendi, lakini hii inakwamisha matumizi sahihi ya mifumo ya kisasa ya ukusanyaji wa mapato. Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba mapato yote yanakusanywa kwa uwazi na ufanisi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Amina Mussa Mkumba, Mbunge wa Kibiti kwa kufuatilia maendeleo ya jimbo na Wananchi wa Kibiti. Hata hivyo, nimhakikishie kwamba Serikali ilishaweka mwongozo na taratibu za ukusanyaji wa mapato, kwa kutumia mashine za kieletroniki za *POS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika stendi hii ya muda ya Kibiti kuna mashine za *POS* zipo mbili ambazo inatumika kutoza ushuru na malipo mbalimbali kwenye eneo la soko, lakini ipo *POS* moja ambayo inatumika kwenye maeneo ya vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaendelea kusimamia kuhakikisha kwamba utaratibu huu unafuatwa, na fedha za Serikali zinakusanywa kwa utaratibu unaotakiwa ili tuweze kuboresha huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi wa stendi hii utaanza baada ya kupata eneo na kutoa fidia, na kwa bahati njema tayari fedha imeshatengwa kwenye bajeti ya 2026/2027.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nami niulize swali la nyongeza. Huu ni mwaka wa 16 nauliza swali la *stand* mpya ya kisasa Jimbo la Bunda Mjini, na Jimbo hili ndiyo limebeba wilaya. Ni lini Serikali itajenga stendi ya kisasa kupitia mradi wa *TACTIC*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kama una majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya, ni kweli amekuwa akifuatilia sana suala hili hata kipindi alipokuwa kule Misri alikuwa anafuatilia sana suala la Bunda Mjini, lakini ninamkaribisha sana hapa nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu kwamba Serikali inatambua umuhimu wa stendi ya kisasa katika Mji wa Bunda kwa sababu mji ule unakua, tayari umewekwa kwenye mpango wa *TACTIC,* tathmini zinaendelea. Kwa hiyo, ni suala la muda, baada ya tathmini na kupata makandarasi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Bunda Mjini watapata stendi ya kisasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Karatu haina stendi inayokidhi viwango hasa tukizingatia kwamba mji ule ni mji wa kitalii, na hasa kipindi hiki cha mvua kunakuwa kuna adha kubwa kwa sababu maji yanajaa. Nini mkakati wa Serikali kujenga stendi nyingine kubwa ya kisasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Cecilia Paresso kwa uwajibikaji wake, na kwa swali hili muhimu kwa wananchi wa Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu wa miundombinu ya stendi katika halmashauri zetu na maeneo yote nchini ambapo kuna sifa za kujenga stendi. Tayari Serikali ilishatoa maelekezo kwa Wakurugenzi wa halmashauri kuzingatia kwenye mipango yao ya bajeti, kutenga fedha kwa awamu, kuainisha maeneo yanayotosha na kuanza ujenzi wa stendi kupitia mapato ya ndani kwa sababu ni moja vipaumbele vya halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo, Serikali Kuu imeendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa stendi hizo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Cecilia Paresso kwamba suala hilo tutakwenda kulifanyia kazi kwa kushirikiana na halmashauri kupitia mapato ya ndani, lakini pia Serikali Kuu kila fursa itakaopatikana tutatafuta fedha kwa ajili ya kujenga stendi ya kisasa katika Mji wa Karatu.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 39

**Kukamilisha Ujenzi wa Shule ya Sekondari Mashimba**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Miundombinu ya Shule ya Sekondari Mashimba katika Halmashauri ya Maswa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilitoa shilingi milioni 470 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya Mashimba inayojumuisha madarasa nane, jengo la utawala moja, maktaba moja, maabara tatu, chumba cha TEHAMA kimoja, matundu ya vyoo 20 na matenki ya kuvuna maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu yote iliyopangwa kujengwa iliishia hatua ya ukamilishaji. Aidha, halmashauri kupitia mapato ya ndani iliongeza shilingi milioni 9.5 kwa ajili ya ukamilishaji wa baadhi ya miudombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya tathmini ya ukamilishaji wa miundombinu hiyo na tathmini hiyo inaonesha kuwa jumla ya shilingi milioni 185 zinahitajika ili kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya shule hiyo. Serikali inaendelea na utaratibu wa kupata fedha hizo ili kukamilisha ujenzi wa shule hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa shule hii leo ni mwaka wa sita miundombinu yake haijakamilika, na kwa kuwa, Serikali imekamilisha tathmini ya majengo, na Serikali inatafuta utaratibu wa kupata fedha, ningependa kujua, ni lini sasa Serikali inapata fedha kwa ajili ya kumalizia miundombinu ya shule hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Watoto wa Shule za Msingi Gihu, Ikungu na Nyashimba wa darasa la sita na la saba watahitajika kwenda sekondari mwakani, na kwa kuwa shule yao pekee ndiyo hii Mashimba Sekondari, je, Serikali ina mkakati upi kuhakikisha miundombinu ya Shule ya Sekondari Mashimba inaongezwa ili ku-*accommodate* watoto watakaotoka kwenye shule hizo tatu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki Mbunge wa Maswa Magharibi kwa kazi kubwa anayoifanya kuwasemea wananchi wa jimbo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba shule hii imechukua muda mrefu tangu kufikia hatua ya ukamilishaji. Hatua ambayo Serikali ilichukua kwanza ni kutambua thamani ya gharama zinazohitajika kwa ajili ya kukamilisha ujenzi. Kazi hiyo tayari imekamilika, na imebainika kuwa tunahitaji shilingi milioni 185 kwa ajili ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Maswa Magharibi kwamba, hatua iliyopo hivi sasa ni Serikali kutafuta fedha ili kuikamilisha shule hiyo mapema iwezekanavyo ili watoto wa shule hizo za msingi ambao wanatarajia kuingia sekondari mwaka 2027 kupitia *Mashimba Secondary School* wasikwame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawakahikikishia kwamba Serikali itakamilisha ujenzi wa shule hiyo kwa kutumia mapato ya ndani ya halmashauri na mapato ya Serikali Kuu ili dhamira ya Serikali ya kuhakikisha watoto wote wanapata fursa hiyo mapema iwezekanavyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, Jimbo la Tabora Mjini ni jimbo la mjini, lakini baadhi ya kata hazina shule ya sekondari kabisa. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha kata hizo zinapata shule za sekondari ili kukidhi haja ya wananchi wa maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini, kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba safari ni hatua. Serikali katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, imefanya kazi kubwa sana ya kujenga shule mpya za sekondari zikiwemo shule katika Jimbo la Tabora Mjini na majimbo yote kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, safari hii inaendelea na kata zile za Jimbo la Tabora Mjini ambazo zina sifa ya kujengewa shule za sekondari, tunazitambua. Tumeanzisha taratibu zinazoendelea, ni namna ya kupata fedha kwa ajili ya kwenda kujenga shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Tabora Mjini kwamba Serikali ipo kazini, na kazi hiyo itafanywa kuhakikisha shule za sekondari zinajengwa katika kata hizo.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Fajari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya.

Na. 40

**Kuinua Kiwango cha Elimu Msingi na Sekondari – Mara**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuinua kiwango cha elimu msingi na sekondari Mkoani Mara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali yenye lengo la kuimarisha ubora wa elimu nchini. Utekelezaji wa hatua hizi umeleta matokeo chanya, ambapo takwimu zinaonesha ongezeko la ufaulu katika mitihani ya Kitaifa kati ya mwaka 2024 na 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalan, kwa mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, ufaulu umeongezeka kutoka 80.87% mwaka 2024 hadi 81.80% mwaka 2025 sawa na ongezeko la asilimia sifuri nukta tisa tatu, kidato cha nne ufaulu umeongezeka kutoka 92.37% mwaka 2024 hadi 94.98% mwaka 2025 sawa na ongezeko la asimilia mbili nukta sita moja; na kidato cha sita ufaulu umeongezeka kutoka 99.92% mwaka 2024 hadi 99.95% mwaka 2025 sawa na ongezeko la asilimia sifuri nukta sifuri tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mkoa wa Mara, ufaulu wa mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi umepungua kutoka 78.05% mwaka 2024 hadi 67.90% mwaka 2025 sawa na upungufu wa 10.15%; kidato cha nne ufaulu umeongezeka kutoka 90.9% mwaka 2024 hadi 92.30% mwaka 2025 sawa na ongezeko la asilimia moja nukta sifuri nne; na kidato cha sita ufaulu ulikuwa 100% mwaka 2024 na mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendelea kuboresha ufaulu katika Mkoa wa Mara, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya elimu kwa kujenga jumla ya shule 32 mpya za msingi na shule 27 mpya za sekondari mwaka 2021 hadi 2026. Aidha, Serikali imeongeza idadi ya walimu kutoka walimu 9,613 mwaka 2021 hadi kufikia walimu 11,766 mwaka 2026 ikiwa ni pamoja na kuboresha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji kwa kujenga miundombinu muhimu, kuajiri walimu wapya, kulipa stahiki za walimu na kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafari Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini tukiri kwamba changamoto ya walimu kwa Mkoa wa Mara bado ni kubwa. Kwa mfano, Wilaya yangu ya Rorya Mheshimiwa Naibu Waziri unakuta shule yenye wanafunzi 800 mpaka 1,000 ina walimu wawili au walimu watatu peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua, ni lini Serikali sasa itafanya tathmini kwanza kuzitambua shule hizi? Pili, kupeleka walimu ili kuokoa na kuinua kiwango cha elimu mkoa mzima na Wilaya ya Rorya kwa ujumla wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili ni kwamba, lipo wimbi la walimu sasa wanahama kutoka maeneo ya vijijini kwenda maeneo ya mijini. Ninatambua ni takwa la kisheria, lakini zipo sababu nyingine ambazo hazihusiani na sheria. Kwa mfano, sababu ya mazingira, na miundombinu ya walimu kufundishia, na pia mazingira ya walimu wanayoishi kwenye maeneo haya ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba sasa inaanza ujenzi wa nyumba za walimu hasa kwenye maeneo ya vijijini kama sehemu ya motisha kwa maana ya *incentives* ili kuwafanya walimu wakae maeneo hayo ya vijijini badala ya kuendelea na wimbi hili la kuhama kutoka maeneo ya vijijini kwenda maeneo ya mjini kama sehemu ya kuinua kiwango cha elimu kwa Mkoa wa Mara na Wilaya ya Rorya kwa ujumla wake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Jimbo la Rorya kwa kazi kubwa anayofanya kuwasemea wananchi wa jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumhakikishia kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita kwa kipindi chote cha

kwanza cha miaka mitano iliyopita imeendelea kuajiri walimu. Pia katika siku 100 za uongozi wa kipindi cha pili cha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, walimu 7,000 wameajiriwa kote nchini na walimu wamepelekwa katika Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba kwanza tumeendelea kutambua mikoa yenye upungufu mkubwa zaidi wa walimu, na Mkoa wa Mara ni miongoni mwa mikoa yenye upungufu mkubwa wa walimu, na tumeendelea kuwapa kipaumbele kikubwa zaidi katika ajira za waimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Wambura Chege kwamba katika ajira ambazo zinaendelea, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele cha hali ya juu kwa Mkoa wa Mara kwa Jimbo la Rorya na pia kote nchini kuhakikisha walimu wanapatikana na kutoa elimu bora kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni kweli kumekuwa na wimbi la baadhi ya waajiriwa wapya kuomba uhamisho mara baada ya kuthibitishwa kwenye vituo vya kazi vijijini. Maelekezo ya Serikali yapo wazi kwamba waajiriwa wote wanaoajiriwa maeneo yoyote kupitia mfumo ambao wanachagua maeneo ya kwenda kupata nafasi hizo za ajira, lazima wafanye kazi angalau kwa miaka mitatu kabla hawajaanza kuhama kwa sababu ambazo ni za msingi zinazosababisha kuhama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI niwaelekeze Wakurugenzi na Makatibu Tawala wa Mikoa kuhakikisha wanajiridhisha na uhamisho ambao haujafuata utaratibu na kufikisha taarifa hiyo Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ili hatua ziweze kuchukuliwa na kudhibiti uhamisho wa walimu na watumishi wengine ambao wanatoka vijijini kwenda mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi, na Serikali imeendelea kujenga nyumba za walimu katika maeneo yote ya mijini na vijijini, na zoezi hilo ni endelevu ili kuweza kuboresha

mazingira ya walimu kuishi, na pia kufanya kazi katika maeneo hayo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu zinazochangia kufifisha ufaulu wa watoto wetu ni umbali mrefu wa kufika shuleni. Ni kweli shule za kata zimejengwa nyingi, lakini kwa uhalisia wake ziko mbali sana na makazi ya wanafunzi. Hali hii husababisha wanafunzi kutumia muda mrefu njiani; wanapofika darasani wanakuwa wamechelewa, na wanaporudi nyumbani wanakuwa wamechoka kiasi cha kushindwa kufanya marejeo ya masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujua, ni mpango gani wa Serikali wa kuhakikisha ujenzi wa mabweni, hususan katika Jimbo langu la Tarime Mjini, katika Shule za Sekondari za Nyandoto, Nyakisese, Kenyamanyori pamoja na Kongole, ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi hawa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Esther Matiko kwa kazi nzuri anayoifanya kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Tarime Mjini, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli ziko shule za sekondari za kata ambazo baadhi ya wanafunzi wanaishi mbali kutoka kwenye shule hizo na wanasoma kutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo imekuwa ni changamoto, lakini kwa mujibu wa sera na miongozo yetu ya elimu kwa sasa, mabweni yanajengwa kwenye shule za kidato tano hadi cha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maeneo ambayo yana changamoto kubwa zaidi za jiografia, Serikali imeendelea kuelekeza kupitia, kwanza, halmashauri, kuona uwezekano wa kujenga hosteli kwa ajili ya wanafunzi. Pia, Serikali Kuu imekuwa

ikifanya kwenye maeneo *exceptional* kuhakikisha kwamba wanafunzi wanapata fursa nzuri ya kuishi karibu na shule na kupata fursa nzuri ya kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa shule hizo ambazo amezitaja tutaendelea kufanya tathmini. Dhamira ya Serikali ni njema, kuhakikisha watoto wetu wanapata fursa nzuri ya kusoma. Tutashirikiana na Halmashauri ya Mji wa Tarime na Serikali Kuu kuona jambo zuri la kuboresha mazingira ya usomaji kwa wanafunzi wetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ninakushukuru sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, Mbunge Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 41

**Usajili wa Wawekezaji Kupitia *TISEZA***

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kusajili wawekezaji wote nchini kupitia *TISEZA* ili kuwa na kanzidata sahihi ya wawekezaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Dodoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi *(TISEZA)* imeendelea kutekeleza jukumu la

kusajili miradi ya uwekezaji kutoka kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kulingana na vigezo vilivyowekwa vya uwekezaji wa mitaji. Hadi sasa Serikali imesajili jumla ya miradi ya uwekezaji 14,209 ambayo imepewa vyeti vya utambuzi na *TISEZA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutumia fursa za teknolojia ya kidigiti, *TISEZA* imekamilisha ujenzi wa Mfumo wa Kanzidata ya Taifa ya Uwekezaji wa Sekta Binafsi utakaounganisha mifumo ya taasisi mbalimbali zinazohusika na usajili wa kampuni za wawekezaji nchini. Mfumo huu unalenga kuboresha upatikanaji wa takwimu sahihi za uwekezaji wa sekta binafsi hususan mitaji iliyowekezwa na ajira zinazozalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa sasa inaendelea na kampeni ya kuhamasisha uwekezaji wa ndani kupitia wazawa. Zoezi hili linaenda sanjari na kutoa hamasa ya wawekezaji wote ambao bado hawajasajiliwa na *TISEZA* na tayari wapo kwenye wilaya zetu wafanye hivyo ili Serikali ipate takwimu sahihi za kiasi cha uwekezaji uliopo nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Neema Majule.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tukizingatia kwamba ukuaji wa uchumi unategemea sana uwekezaji aidha wa ndani au wa nje na tunatia moyo wawekezaji hawa kuweza kuwekeza katika nchi yetu, swali langu ni hili hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, *TISEZA* imeweka vigezo gani vya kuwafanya wawekezaji wengi zaidi waweze kujisajili ili waweze kunufaika na fursa hii? Siyo hivyo tu, ili na hasa kuwapata wale wawekeza wadogo na wa kati ambao ndio wengi sasa hivi wamechipukia, wengi wao wakiwa ni wanawake na vijana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, swali la pili ni kwamba *TISEZA* wameweka vivutio gani vya kuwafanya wawekezaji wengi zaidi waweze kujisajili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Majule ni Mjumbe wa Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria na amekuwa na michango mikubwa sana hususan kwenye masuala ya uwekezaji wa nchi hii na ndiyo maana leo amekuja na swali mahsusi la kujua ni kwa kiasi gani nchi imeweza kuwekeza katika kusajili wawekezaji ili tuweze kukidhi ile haja ya Dira yetu ya 2050 ya kufikia shilingi trilioni moja ifikapo 2050, lakini kuhakikisha kwamba 70% inachangiwa na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ninaomba nijibu maswali mawili kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kigezo kikubwa ambacho tumekiweka katika kusajili hawa watu ni ukubwa wa mtaji. Tuna wawekezaji wa aina nne Tanzania. Tuna wawekezaji wazawa wa aina mbili. Mwekezaji mzawa wa kwanza anatakiwa awe na mtaji wa angalau dola 50,000 takribani shilingi milioni 125, na mwekezaji wa kimkakati wa ndani anatakiwa awe na dola angalau milioni 50 ambapo kimsingi tutam-*term* kama mwekezaji wa kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, wawekezaji wa nje wapo wa *category* aina mbili. Tuna mwekezaji wa kawaida wa nje anatakiwa awe na dola 500,000 za Kimarekani. Huyu naye tutam-*term* kama mwekezaji wa kawaida. Mwekezaji wa kimkakati anatakiwa awe na angalau Dola milioni 50 za Kimarekani, huyu atakuwa ni mwekezaji wa kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, tuna vivutio mbalimbali ambavyo tumeviweka. Vivutio hivyo ambavyo ni vya kikodi na ambavyo siyo vya kikodi. Ninaomba nitoe wito kwa wawekezaji wote nchini hususan wazawa. Tuna kituo chetu cha pamoja pale *TISEZA* ambacho kimsingi tunatoa maelekezo na ufafanuzi mbalimbali wa vivutio gani wa kikodi na ambavyo siyo vya kikodi ambavyo wanaweza kuvipata kwa ajili ya kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe, aulize swali lake.

Na. 42

**Ujenzi wa Ghala Baridi za Kuhifadhia Zao la Parachichi – Rungwe**

**MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa maghala Baridi mawili ya kuhifadhia zao la parachichi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana. Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026 imeendelea na ujenzi wa Kituo Jumuishi cha Huduma ya kuhifadhi na kuongeza thamani ya Mazao ya Bustani baada ya kuvuna kwa maana ya *Common Use Facility* katika Kata ya Nkunga - Wilaya ya Rungwe wenye thamani ya shilingi bilioni 2.995 ili kukusanya, kuchambua, kupanga madaraja, kufungasha na kusafirisha mazao ya bustani ikiwemo zao la parachichi kwa lengo la kupunguza upotevu wa zao hilo baada ya kuvuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kituo hicho umefikia 25% na ujenzi unaendelea. Aidha, ili kurahisisha upatikanaji wa parachichi, Wizara inajenga vituo sita vya kukusanyia parachichi kwa maana *collection center* katika Wilaya ya Rungwe ambapo ujenzi umefikia wastani wa 17% na unatarajia kukamilika ifikapo mwaka wa fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anton Mwantona.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nitoe shukrani zangu za pekee sana kwa Serikali kwa ujenzi wa haya maghala pamoja na vituo vya kukusanyia mapato, hizi *collection centers*. Swali langu lilikuwa linasema maghala mawili, kwa mujibu wa ahadi ya Mheshimiwa Rais, nilikuwa ninapenda nijue hilo ghala lingine ujenzi wake unaanza lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, wakati Serikali inaendelea kujenga maghala na *collection center,* Serikali inapanga bei za ununuzi wa parachichi kwa bei elekezi, lakini kwa mwaka huu kidogo tumepata shida kwamba bei elekezi inatolewa na kule kwenye *site* wananunua kwa bei ya chini. Sasa Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba bei elekezi ambayo inatolewa na Serikali inasimamiwa ipasavyo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpongeze Mheshimiwa Anton Mwantona, Mbunge wa Jimbo la Rungwe. Kiukweli ni moja ya ahadi yake na alipambana sana kuhakikisha kwamba inatokea. Nimthibitishie tu ujenzi wa ghala lingine unaanza katika mwaka wa fedha unaokuja 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusu bei elekezi, sisi kama Serikali tutasimamia kuhakikisha ile bei ambayo inapangwa inatekelezeka na tutatuma wataalamu huko chini kuhakikisha bei ile inafuatwa ili iweze kumnufaisha mkulima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ninakushukuru sana kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Tuna swali la Mheshimiwa Marirta Gido Kivunge, Mbunge wa Viti Maalum, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Sylvia Sigula.

Na. 43

**Huduma za Dawa na Chanjo Muhimu kwa Mifugo**

**MHE. SYLVIA F. SIGULA K.n.y. MHE. MARIRTA G. KIVUNGE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa huduma za dawa na chanjo muhimu ili kuboresha afya na kuongezea thamani ya Mifugo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, ninaomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Marirta Gido Kivunge, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Arusha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa chanjo katika kudhibiti magonjwa ya mifugo nchini. Kwa msingi huo, Utekelezaji wa Mpango wa Chanjo na Utambuzi wa Mifugo wa miaka mitano, wenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 216, unatekelezwa kuanzia mwaka 2024/2025 hadi mwaka 2028/2029 na ambao ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 16, Juni, 2025 Bariadi Mkoani Simiyu na huu ni ushahidi wa dhamira ya Serikali ya kuboresha Afya ya mifugo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2024/2025, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitenga kiasi cha shilingi

bilioni 61.2 kwa ajili ya kuendesha Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo nchi nzima kwa lengo la kuchanja na kutambua ng'ombe milioni 19, mbuzi na kondoo milioni 17 na kuku wa asili milioni 40. Hadi kufikia mwezi Machi, 2026 uchanjaji umefikia 64.5% kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara inapanga kuendelea na Awamu ya Pili ya Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo nchi nzima ambapo, jumla ya shilingi bilioni 30.8 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza zoezi hilo kwa maeneo mbalimbali nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sylvia Sigula.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninaipongeza Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Moja kati ya magonjwa yanayodhoofisha afya ya mifugo katika Wilaya zote za Mkoa wa Arusha ni pamoja na homa ya midomo na miguu kwa mifugo. Sasa nilitaka kufahamu, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha chanjo ya homa ya midomo na miguu inawekwa kuwa kipaumbele?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa kwenye bajeti ya fedha kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitengwa zaidi ya shilingi bilioni 61 kwa ajili ya kuendeleza kampeni ya chanjo na utambuzi wa mifugo, katika zoezi hilo kwenye sera, Wenyeviti wa Serikali za Vijiji nchi nzima walipaswa kufanya hilo pamoja na wataalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalamu wale walishalipwa malipo ya fedha ile, lakini Wenyeviti wa Serikali za Vijiji nchi nzima mpaka leo bado hawajalipwa fedha hizo, na Serikali inajiandaa kwenda kwenye Awamu ya Pili kabla ya kulipa fedha za Wenyeviti wa Serikali za Vijiji kwa Awamu ya Kwanza. Je, ni ipi kauli

ya Serikali kuhakikisha inawalipa Wenyeviti wa Serikali za Vijiji kwa kazi ambayo waliifanya kwenye Awamu ya Kwanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwanza nianze kwa mpongeza sana Mheshimiwa Sylvia Sigula kwa maswali yake mazuri ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kuhusiana na ugonjwa wa madonda ya miguu na midomo almaarufu kama *FMD*, Wizara imeshafanya tathmini ya magonjwa 13 ya kipaumbele ambayo tutakwenda nayo kwa awamu ya pili ya chanzo, na ugonjwa huo wa *FMD* ni moja ya magonjwa haya ya kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba mpaka sasa Wizara iko katika hatua ya kuchambua ni aina gani ya Kirusi cha *FMD* tulichonacho hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaainisha, tunazo aina nne za virusi hivi ya *FMD*. Hatua tuliyopo kwa sasa Mheshimiwa Mbunge ni kuhakikisha tunaangalia ni aina gani ya chanzo ambazo tutakwenda kuzitoa kwa kila mkoa. Kabla ya kufikia kwa mwezi Mei mwaka huu 2026 Wizara itatangaza aina za chanjo za *FMD* ambazo zitakwenda kwenye kila mkoa kulingana na aina ya kirusi kitakachokuwepo kwa kila mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la pili, ni kweli katika mwongozo wetu wa mwaka 2024/2025 wa zoezi la uchanjaji nchi nzima na utambuzi wa mifugo, wadau mbalimbali wakiwemo Wenyeviti wa Serikali za Mitaa walipewa majukumu mbalimbali ya kuisimamia ikiwemo zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza wadau hawa kwa sababu wamefanya kazi nzuri sana, hata hizi 64.5% ambazo tumefikia za uchanjaji ni kwa sababu ya juhudi ambazo Wenyeviti

hawa wamefanya. Fedha za uhamasishaji zimepelekwa katika halmashauri zetu nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwamba halmashauri zetu basi ziwafikishie wadau hawa fedha za malipo ya posho zao kadiri ya bajeti zilizopelekwa katika halmashauri zao na kazi nzuri waliyofanya. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mvita Ali, atafuatia Mheshimiwa Ussi Pondeza maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. MVITA MUSTAFA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la nyongeza linakwenda kwa kupitia Wizara ya Ardhi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha matumbawe au mazalia ya samaki kwa kutokana na uchafuzi mkubwa ndani ya Bahari, maziwa pamoja na mabwawa? Serikali ina mpango gani wa kuanzisha matumbawe hayo ili kuwe na mazalia makubwa sana ya Samaki? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nimpongeze pia Mheshimiwa Mbunge swali zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mikakati ya Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi ya kuhakikisha tunakuwa na uvuvi endelevu katika Bahari Kuu ni kuhakikisha kwamba tunalinda mazalia yaliyopo, lakini kuanzisha matumbawe au kuweka matumbawe kwa ajili ya kuwa mazalia mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara inaendelea kufanya tathmini na tafiti na katika kila sehemu ambayo inaonekana ina uwezo wa kuwekwa matumbawe haya kadiri ya upatikanaji wa fedha, basi tutaendelea kufanya hivyo ili kuendelea kukuza uchumi wa buluu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ussi Pondeza.

**MHE. AMJADI USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa na swali moja ninaomba nimwulize Waziri wa Mifugo. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuviongezea uwezo viwanda vya ndani ili viweze kuchakata nyama hapa nchini badala ya kusafirisha mifugo hai ili iweze kuongeza ajira na vilevile kuweza kuingiza fedha za kigeni kwa kusafirisha nyama badala ya mifugo ambayo iko hai? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Serikali kwa sasa imejikita zaidi katika kuhakikisha tunaiwezesha sekta binafsi kuendelea kuwekeza katika sekta zetu hivi ikiwemo sekta ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya vitu ambavyo tunaviangalia kwa ukaribu ni kuhakikisha kwamba tunafanya kazi kwa karibu ikiwemo kuendelea kutatua changamoto mbalimbali za kikodi au kimifumo kwa wawekezaji hawa waliowekeza katika viwanda vya nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tutaendelea kuboresha malighafi kwa maana ya mifugo tuliyonayo ikiwa ni pamoja na zoezi hili la chanjo ili kuendelea kuongeza ubora wa nyama ambayo tunazalisha nchini na kuongeza masoko yetu ya Kimataifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kija Ntemi.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba na mimi nimwulize swali Mheshimiwa Waziri. Kwa namna ilivyo sasa, magonjwa haya ya miguu na kwenye midomo ya ng’ombe yameshamiri sana kwa sababu ya hali ya hewa na mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, mkakati huo unaosema kwamba utafikiwa mwezi wa tano kwa ajili ya kugundua au kutoa

dawa kwa ajili ya kusaidia wafugaji kutibu ng'ombe wao, je, hamwoni kwamba kuna haja ya kuingia mtaani kufanya tathmini huu ugonjwa unasababishwa na nini kwa sasa kwa hali ya mvua ilivyoongezeka katika maeneo yetu na kuwasaidia wafugaji hawa kuondokana na jambo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi ni mfugaji pia, na ni Mhanga wa haya mambo. Hata sasa ninavyozungumza hivi, kuna ng'ombe wangu yupo chini ana vidonda miguuni na mdomoni na hawezi kutembea. Mna mkakati gani kuwafikia wafugaji ili waweze kupata huduma kwa wakati, kuwasaidia na kuwaondolea adha ya mifugo yao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwanza nianze kwa kumpa pole sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ameeleza wazi kwamba naye ameathiriwa na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya awali, kwamba Wizara ilikuwa katika harakati za kufanya utafiti na tayari tumeshagundua *strands* au aina ya virusi tulivyonavyo vya *FMD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *FMD* ni ugonjwa ambao una aina mbalimbali za virusi, siyo kirusi cha aina moja. Kwa hiyo, ni muhimu kufanya tafiti kugundua kwamba katika maeneo yetu tuna aina ipi ya ugonjwa huu wa *FMD* ili kuipatia dawa mahususi. Hatua tulizonazo ni kwamba tulishagundua kwa kufanya tathmini nchi nzima kwamba sisi tunazo aina nne za ugonjwa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoahidi hapo mwanzo, niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kabla ya mwezi Mei mwaka huu 2026 na sasa hivi tupo mwezi Aprili tutatoa majina ya kila mkoa ni ina aina gani ya virusi hivi na dawa ipi iweze kutumika kwa ajili ya kutibu mifugo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Wizara tunafuatilia kwa ukaribu na kufanya tathmini nchi nzima katika hali ya mifugo inayoendelea na tunafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha tunaendelea kuzuia magonjwa haya na kuzuia vifo vya mifugo ambavyo vinatokana na ugonjwa huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 44

**Gari la Zimamoto, Mbulu**

**MHE. YUSTINA A. RAHHI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka gari la Zimamoto katika Wilaya ya Mbulu?

**MWENYEKITI:** Majibu ya Swahili hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na jitihada za kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini. Katika Wilaya ya Mbulu Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepeleka gari jipya la zimamoto na uokoaji aina ya *IVECO* 189, lenye ujazo wa maji lita 5,000 na lita 500 za *foam*. Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri, lakini naipongeza Serikali, wananchi wa Mbulu tumefurahi mno. Nimepokea hilo gari wiki iliyopita pamoja na Mkuu wa Wilaya. Wananchi wa Mbulu wamepata faraja kubwa sana kwa sababu, majanga ya moto yalikuwa mabaya sana katika Wilaya ya Mbulu, ikiwepo kwisha kabisa nyumba ya UVCCM ya Wilaya ya Mbulu, pamoja na jengo mashuhuri sana pale katika Mji wa Mbulu, nyumba ya Guam, lakini nina maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, kikosi cha zimamoto pamoja na uokoaji wanawashinikiza au wanatembelea vikundi mbalimbali vya watu, wakiwepo wafanyabiashara, taasisi mbalimbali pamoja na wamiliki wa vyombo vya moto kufunga ile mitungi ya *fire extinguisher,* lakini watu hao wanaofundishwa hawajui vizuri matumizi ya vifaa hivyo. Sasa ni kwa kiasi gani basi Serikali imeelimisha vikundi hivi vinavyolengwa matumizi na tahadhari ya kujizuia na moto kabla ya kuwafungia vifaa hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Imeonekana mara nyingi madhara ya moto katika majengo yamesababishwa na hitilafu ya umeme. Sasa ni kwa kiasi gani kikosi cha zimamoto na uokoaji kimeshirikiana na *TANESCO* kuwasaidia wananchi wetu kuchukua tahadhari, ili majanga yanayosababishwa na hitilafu ya umeme yasijirudie mara kwa mara? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Yustina kwa maswali yake mawili ya nyongeza, ambayo ni muhimu kwa mustakabali wa Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianzia na swali lake la kwanza la kwa namna gani Serikali, kupitia Kikosi cha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, imeweza kutoa elimu kwa wananchi, ili kuhakikisha kwamba, wananchi wanakuwa na elimu ya vifaa vile vya kuzimia

moto endapo majanga yanatokea; ninapenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni jukumu la Zimamoto na Uokoaji kuendelea kutoa elimu ambapo kwa sasa kazi ya utoaji wa elimu inaendelea katika maeneo mbalimbali wakiwemo wataalamu wanaofundishwa, kwa maana ya *Fire Volunteers* nchi nzima, ambao hao wanaisaidia Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuhakikisha kwamba, elimu inawafikia wananchi kwa kadiri hali inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa upande wa shule, tuna *Fire Clubs* katika shule mbalimbali na vilevile kupitia vyombo vya Habari, vikiwemo *mass* na *social media,* tunaendelea kuelimisha wananchi. Swali hili kwa kweli, wakati najibu swali la msingi la kwanza katika Bunge hili, nilitoa tathmini ya hali ya utoaji wa elimu kwa wananchi na tulisema kwamba, tumefikia wananchi kwa kiasi kikubwa hasa kupitia vyombo mbalimbali vya habari, lakini hata hivyo utaratibu uliopo katika suala la elimu kwa wananchi ni kwamba, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linahakikisha kwamba, wale ambao wananunua hivi vifaa vya kuzimia moto kupitia kwa ma-*dealers* mbalimbali wanapewa elimu kabla ya kupewa vifaa vyenyewe vya kuzimia moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo linaendelea kufanyika katika maeneo mbalimbali nchi nzima. *Dealers* hawa waliopo kwenye mikoa mbalimbali kabla ya kufanya kazi ya kuuza vifaa vya zimamoto na uokoaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linafanya jitihada za kuhakikisha kwamba, linawasajili na linawaelimisha, ili nao wawe na uwezo wa kutoa elimu hiyo kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa pili wa miundombinu ya umeme kuwa, mara nyingi imekuwa ikitajwa kuwa ndiyo chachu ya chanzo cha moto katika majengo mbalimbali. Napenda kumwarifu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wakati wa ujenzi wa majengo yote, hasa yale makubwa, ambayo yanahitaji mifumo ya zimamoto na uokoaji ni moja kati ya taasisi ambayo inatoa ushauri kupitia vibali vya ujenzi vinavyotolewa na wajenzi mbalimbali na kuweza kutoa maelekezo wakati ujenzi unafanyika. Kupitia maelekezo hayo, miundombinu mingine, ikiwepo

miundombinu ya umeme, pia maelekezo ya msingi yamekuwa yakitolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mbali na utoaji wa maelekezo hayo, baada ya jengo kukamilika ujenzi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limekuwa likifanya jitihada ya ukaguzi wa mwisho na hatimaye kutoa ithibati, kwa maana ya *certificate* ya kuhakikisha kwamba, jengo hilo limekidhi vigezo na kuzingatia hali ya miundombinu ya zimamoto na uokoaji katika jengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namjibu tu Mheshimiwa Mbunge, na nitoe rai kwa ujumla kwamba, ninawaomba sana wale wote ambao wanajenga au wanatumia vifaa vya zimamoto na uokoaji ama kupitia majengo au magari au vyombo vingine vya moto, basi kabla ya kuweza kuondoka na vifaa hivyo katika maduka yao, wawe wamepata elimu ya namna ya matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salum Salim.

**MHE. SALUM KHAMIS SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itajenga Ofisi ya Uhamiaji katika Wilaya ya Hujee Mjini Unguja?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri la msingi na namna anavyozingatia wananchi wake kwa kuomba ujenzi wa Kituo cha Uhamiaji, maana sikufahamu kuwa Zimamoto na Uokoaji ni Uhamiaji. Pengine haikuendana na swali la msingi, lakini namjibu tu kwamba, kwa sasa Serikali inaendelea na jitihada za kuhakikisha inafikisha Ofisi za Uhamiaji nchi nzima katika kila wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa baadhi ya maeneo ambayo yana uhitaji maalum, tutahakikisha kwamba, tunafikisha huduma za uhamiaji na kuweka Kanda Maalum kwa mujibu wa mahitaji ya eneo husika. Kwa hiyo, namwomba tu awe na subira kwa sababu, ujenzi huu unaenda hatua kwa hatua, na kwa kweli, uhitaji ni mkubwa. Kwa hiyo, avute subira, tunaendelea na utaratibu na tutajenga ofisi ya uhamiaji pia katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ibrahim Shayo.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Moshi ni Makao Makuu ya Mkoa, Jengo la *fire* limejengwa kuanzia Mwaka 1954. Je, lini Serikali itajengea Jengo la *Fire* Moshi Mjini?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuendelea kumjibu Mheshimiwa Ibrahim, Mbunge wa Moshi, kama ambavyo swali lake ameliuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Moshi Mjini ni moja kati ya maeneo muhimu na ya kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa jengo la zimamoto na uokoaji katika eneo la mkoa ule. Ni kweli kwamba, ninayo ahadi na Mheshimiwa Ibrahim kwamba, tutakapofanya ziara katika Mkoa wa Kilimanjaro, basi tuweze kufika na kuona eneo lake na kuweza kujengwa kwa jengo, kama ambavyo ameliuliza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuwekeza miundombinu na vifaa katika Jeshi hili la Zimamoto na Uokoaji, ikiwemo ujenzi. Kwa mwaka wa fedha uliopita tunaoendelea nao wa 2025/2026, zaidi ya shilingi bilioni 18 zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo 10 vya zimamoto na pia, maeneo ya chuo cha zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha ujao tutaendelea kutenga fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa vituo

hivyo. Kwa hiyo, tutafanya mazingatio ya hali ya Moshi na uhitaji wake, ili kusudi tuweze kujenga jengo hilo kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameuliza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mwandabila.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatamani kufahamu, ni upi mpango wa Serikali kuhakikisha Ofisi za Zimamoto kwenye wilaya zetu na mikoa wanakuwa na yale magari ya usimamizi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge. Niseme tu, kwa wakati huu, kama nilivyoeleza awali kwamba Serikali kwa kipindi hiki kwa mara ya kwanza imetenga fedha zaidi ya dola milioni 100, fedha ambazo moja kati ya eneo ambalo lilisukuma ilikuwa ni upande wa vitendea kazi yakiwemo magari ya usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa takriban Wilaya zote za upande wa Tanzania Bara, zina magari ya zimamoto, isipokuwa wilaya zile ambazo zina uhafifu wa baadhi ya miundombinu na vitendea kazi muhimu, ndizo ambazo hazijafikiwa, nazo hazizidi wilaya sita. Kwa hiyo, tutaendelea kusambaza vifaa hivyo au magari haya na vitendea kazi katika maeneo ya wilaya kadri tutakavyopokea kwa sababu, bado baadhi ya magari hatujayapokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna magari karibu 237, ambayo ni ya zimamoto pekee, kati ya hayo 153 ni ya zimamoto, 78 ya uokoaji na magari sita ni *mobile workshop*. Kwa hiyo, magari ya usimamizi yataendelea kusambazwa kadiri tutakavyoyapokea na kuweza kuyafikisha katika maeneo yenye uhitaji.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunamalizia na Wizara ya Maji. Sasa Mheshimiwa Charles Jacob Sungura, Mbunge wa Handeni, aulize swali lake.

Na. 45

**Upatikanaji wa Maji Safi na Salama, Mkata**

**MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka Maji Safi na Salama kutoka Mto Wami katika Mji wa Mkata?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wizara ya Maji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Jacob Sungura, Mbunge wa Jimbo la Handeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Mkata kwa sasa unapata huduma ya majisafi na salama kupitia chanzo cha maji cha Mto Wami kufuatia kukamilika kwa mradi wa kutoa maji tenki lililopo Kijiji cha Tengwe kwenda matenki ya Mwamizi na Mkata Sekondari yaliyopo katika Mji wa Mkata, Wilayani Handeni, Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo ulihusisha pia ulazaji wa mabomba kutoka Tengwe hadi Bwauni, Mkata, umbali wa kilomita nne, ambapo unahudumia zaidi ya wananchi 35,000 wa Mji wa Mkata na viunga vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwenye Mji wa Mkata, Serikali inaendelea na zoezi la uchimbaji wa visima virefu katika maeneo matano ya Vitongoji vya Nkulimba, Chang'ombe, Kwafuta, Kwamwamwizi pamoja na Negero, ili kuongeza uzalishaji wa maji yatakayotosheleza wananchi. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Jacob Sungura.

**MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la pili litakuwa na sehemu (a) na (b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali la kwanza; kwa kuwa, Mradi wa Maji wa Miji 28 katika Jimbo la Handeni umefikia asilimia nzuri tu, 78%, je, Serikali inaweza kutoa kauli rasmi sasa, ni lini mradi huu utakamilika kwa lengo la kutoa huduma kwa wananchi ili kutimiza kusudi la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kumtua mama ndoo kichwani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili (a). Mradi wa Maji wa Segera, Kabuku wa shilingi bilioni 25 ni mkombozi wa vijiji vingi, utanufaisha takribani kata nane, lakini kasi yake ya 60%, maana sasa hivi upo 60%, hailingani na mahitaji makubwa ya maji. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa dharura wa kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huu ili ukamilike ndani ya mwaka huu wa fedha 2026/2027?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili (b).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ni maswali mawili tu na umeshauliza mawili. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Charles Jacob Sungura, Mbunge wa Handeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri tangu amechaguliwa kwa kuendelea kuwasemea wananchi wake wa Jimbo la Handeni, kwa ufuatiliaji na kwa ushirikiano mzuri sana anaotupatia sekta ya maji katika kuhakikisha kwamba, tunawafikishia wananchi huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa miji 28 ambao Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imewekeza zaidi ya shilingi bilioni 171 unapita katika Miji ya Handeni, Korogwe, Muheza pamoja na Pangani. Utakapokamilika zaidi ya wakazi 850,000 watakaopitiwa na bomba kuu, kilomita 12 kushoto na kulia na katika chanzo cha maji ambako yanatolewa, wananchi wanaozunguka katika maeneo hayo pia, watapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninawapongeza sana Wanahandeni na Wanatanga kwa mradi mkubwa huu ambao Mheshimiwa Rais ameona kwamba, unaenda kukamilika ifikapo Oktoba, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali la pili, Mradi wa Segera Kabuku, ni kweli kabisa mradi huu umefikia 60% na una gharama ya shilingi bilioni 25, ambapo Mheshimiwa Rais alielekeza kwamba, wananchi wa maeneo hayo wapatiwe huduma ya majisafi na salama. Kwa umahiri kabisa Mheshimiwa Waziri wetu alihakikisha kwamba, mradi huu unakuwa *designed,* ili uwanufaishe wananchi wa maeneo hayo katika shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo madai ya mkandarasi ambayo takribani shilingi bilioni saba. Sasa tumekamilisha mchakato wa kupeleka Wizara ya Fedha, ili aweze kulipwa na atakapolipwa, tutahitaji kuona kazi ambayo itaendana na fedha ambazo atalipwa. Lengo ni kwamba, mradi huu ukamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtoa hofu Mheshimiwa Mbunge, hakuna mradi utakaosimama, miradi yote itakamilika. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Licha ya Mkoa wa Morogoro kuwa na mito mingi, lakini wananchi wa Jimbo la Manispaa ya Morogoro katika Kata za Mkundi, Kingolwira, Tungi na Kiegea hawana

majisafi na salama. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha wananchi hawa wanapata maji?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kuwasemea wanawake kwa sababu, maji ni huduma ambayo inawagusa sana akinamama na tunasema kwamba, kila mwananchi ana haki ya kupata huduma ya msingi ikiwemo maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na upatikanaji wa vyanzo vingi vya maji ikiwemo mito kama ambayo Mheshimiwa Mbunge amesema, lakini pia, tuna Bwawa la Mindu ambapo Serikali inaendelea kuwekeza na kuliboresha zaidi kuhakikisha kwamba, wananchi wote wanaozunguka katika Manispaa ya Morogoro wanapata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtoa hofu, Serikali imewekeza fedha nyingi na tunaendelea kukamilisha miradi mingi. Itakapokamilika tutafanya tathmini na kujiridhisha wapi bado wana changamoto kubwa ili Serikali iweke utaratibu mwingine wa kwenda ku-*cover* katika maeneo ambayo yatakuwa yamebaki. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Moses Kaegele.

**MHE. MOSES L. KAEGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Wampembe na vijiji vyake kwa muda mrefu sana wananchi hawana majisafi na salama. Je, upi mpango wa Serikali wa kupeleka majisafi na salama katika kata hiyo na vijiji vyake?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kaegele ameendelea kulisemea hili suala, na kimsingi tunamshukuru sana. Pia tulikuwa na mradi wa vijiji vinne katika Makao Makuu ya Tarafa ya Mwampembe ambapo mradi

huu ulikuwa unatekelezwa kwa msaada wa *USAID,* lakini kwa bahati mbaya kulingana na mabadiliko ya kiuongozi, mradi huo ulisitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunafahamu kwamba maji yakipatikana, vijiji vinastawi, na vijiji vikistawi, Taifa linastawi. Kama sekta ya maji na Wizara ya Maji tumeweka mpango mkakati mwingine wa kuhakikisha kwamba mradi huo uliokuwa unatekelezwa kwa msaada wa *USAID,* Serikali inaenda kuukamilisha, na jana tuliongea na Mbunge tukakubaliana tukutane leo baada ya vikao vya Bunge ili tuweke mpango ambao utaenda kutatua changamoto kwa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Mayenga.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Moja kati ya kazi kubwa sana ambayo Rais wetu kipenzi ameifanya katika Wilaya yetu na Jimbo langu la Kishapu ni usambazaji wa maji kutoka kwenye mradi mkubwa wa Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa maji wa Ziwa Victoria wananchi wameufurahia sana, lakini kama ambavyo Wizara hii inafahamu, zipo changamoto ndogo ndogo ambazo hazikuweza kumalizwa ambazo zimesababisha wananchi hawa wengine kufaidika zaidi na wengine kutokufaidika kabisa na hasa ikizingatiwa kwamba kwenye Jimbo hili na Wilaya hii changamoto namba moja ni maji, mbili ni maji na tatu ni maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Wizara hii itakuja kwenye Jimbo hili la Kishapu kufanya tathmini ya kina kuangalia zile changamoto ndogo ndogo ambazo zimebakia ziweze kumalizwa ili wananchi wote waweze kufaidika na maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na nimshukuru dada yangu Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mbunge mahiri. Akiwa Mbunge wa Viti Maalum alipambana na alishiriki katika kuhakikisha kwamba mradi mkubwa wa Ziwa Victoria umefika mpaka Shinyanga. Sasa ni Mbunge wa Kishapu ambapo anatambua kwamba kweli Serikali imefanya uwekezaji mkubwa na sasa anakiri kabisa kwamba changamoto zilizobaki ni kidogo ambazo zinahitaji tathmini ili tuweze kuzimalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Maji kumwelekeza mara moja *Regional Manager* Mkoa wa Shinyanga, yeye na timu yake leo hii waende Kishapu wakaanze kazi mara moja, na baada ya siku saba tupate majibu ya nini kinatakiwa kufanyika kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi wa Kishapu hawahitaji shida ndogo ndogo, wanahitaji maji, nasi Serikali tumejipanga kutatua changamoto hizo, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khalid Nsekela.

**MHE. KHALID M. NSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ukarabati wa mradi wa maji wa Kigorogoro, Lulama na Kashani? Ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru sana Mheshimiwa Nsekela kwa kuongelea kuhusu hili eneo. Kama nilivyosema, kila mwananchi ana haki ya kupata huduma za msingi ikiwepo maji, lakini kila mwananchi anao wajibu wa kulinda vyanzo vyetu vya maji na miundombinu yetu ya maji. Kwa upande wa mradi aliosema Mbunge, Serikali ilichimba kisima, wananchi wakaenda kuweka mawe, mradi ukaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikapeleka tena fedha kwa mara ya pili, wananchi wakaenda wakafukia kisima hicho.

Wataalam wetu wakaenda kutoa elimu, kwa sababu ya tofauti zao za kisiasa, Serikali imeendelea kupata hasara katika eneo hilo. Serikali haitapeleka fedha kwa sasa mpaka tupate *commitment* ya wananchi kwamba watakuwa sehemu ya kulinda miundombinu ya maji ambayo Serikali inaenda kuwekeza katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni wajibu wa Watanzania wote, tunapoharibu miundombinu, hizi ni fedha ambazo zinatokana na kodi zetu sisi wenyewe. Lazima tushiriki kwa pamoja ili kuhakikisha kwamba fedha hizi ziwe na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mbunge sana, lakini nitapenda kwamba yeye pamoja na wananchi wake, wakae wakubaliane tupate *commitment* kwa maandishi, ndipo tulete fedha kwa ajili ya mradi huu. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Serikali ilituletea shilingi bilioni 3.39, tukajenga mradi wa Kikafu, lakini bado kuna changamoto ya maji eneo la Bomang'ombe hasa kipindi cha mwezi wa Tisa, Mwezi wa Kumi na Mwezi wa Kumi na Mbili. Tumefanya *feasibility study* tukapata shilingi bilioni kumi, ambazo zinahitajika ili kuondoa tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini sasa Serikali itatuletea fedha hizi ili tuondoe changamoto ya maji hasa eneo la Bomang'ombe na viunga vyake? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kupokea swali la Mheshimiwa Saasisha Mafuwe, Mbunge wa Hai. Kwanza, ninakiri kabisa kwamba ni moja wa Wabunge ambao tunashirikiana vizuri sana, na amekuwa akituletea changamoto za wananchi wake, na anafuatilia kwa ukaribu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hili tunalipokea, tutaenda kulifanyia kazi, na tutamshirikisha kwa hatua zote ili kuona namna ambavyo tutatatua changamoto ya maji katika maeneo ya Bomang'ombe pamoja na maeneo mengine yanayozunguka eneo hilo. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Waziri kwa majibu hayo ya Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekwisha kwa siku ya leo. Ninaomba niendelee kusisitiza maswali yaweze kuwa mafupi kwa mujibu wa Kanuni zetu ili Wabunge wengi wapate fursa ya kuuliza maswali kwa mujibu wa Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Waheshimiwa Mawaziri tunaomba majibu yawe yamenyooka, pia yawe kwa kifupi. Nafikiri tukifanya hivyo, basi Wabunge wengi watapata kuuliza maswali kuhusu Majimbo yetu na Serikali itaweza kutoa majibu. Tukisema tuongee kama tunahutubia, watu wengi au Waheshimiwa wengi hawatapata fursa ya kuuliza.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni wakati wa matangazo. Tunayo matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wapo wageni saba wa Waziri Mkuu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, ambao ni Laigwanani na wafugaji kutoka Wilaya za Longido, Monduli na Ngorongoro Mkoani Arusha.

Waheshimiwa Wabunge, pia yupo Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge Mstaafu wa Jimbo la Longido; Ndugu Joseph Ole Sadira, Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Longido; Ndugu Kiaro Kubany, Laigwanani; Ndugu Metui Shaudo, Laigwanani; Ndugu Nookiropil Moko, Laigwanani; Ndugu Natuli Letema Leiyo, Laigwanani; Ndugu Mepukori Naisikie, Laigwanani. Karibuni sana wafugaji wetu kutoka Wilaya hizo za Longido, Monduli na Ngorongoro Mkoani Arusha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine ni wa Waheshimiwa Wabunge. Kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, Mbunge na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ambaye ni Ndugu Issa Kargbo, Afisa wa Ubalozi wa Tanzania Nchini Uingereza zaidi ya miaka 30. Karibu sana. Mgeni mwingine wa Mheshimiwa Kairuki ni Ndugu Ahmed Kaubebe, Katibu wa Waziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia, tunao wageni 17 wa Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa, Mbunge ambaye ni Naibu Waziri wa Madini, Madiwani kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Longido Mkoani Arusha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 45 Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo, Mbunge ambao ni wanafunzi na walimu kutoka Chuo cha Ushirika Moshi Mkoani Kilimanjaro. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Chuo hicho cha Ushirika Mkoani Moshi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vilevile wapo wageni 24 wa Mheshimiwa Dkt. Evaline Wilbard Munisi, Mbunge ambao ni familia yake, viongozi, na Chama cha *NCCR*-Mageuzi na viongozi wa Taasisi ya *Women in Leadership* kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tanaye mgeni wa Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya, Mbunge, ambaye ni Ndugu Joseph Rezahuya, Katibu wa CCM Wilaya ya Mbozi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vilevile wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Allan Thomas Mbano, Mbunge. Hawa ni Mkuu wa Wilaya ya Kakonko na viongozi wa halmashauri kutoka Kakonko Mkoani Kigoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe ambao ni watoto wake kutoka Zanzibar. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, Ndugu An-nour Athuman na familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wanafunzi 35 kutoka chuo cha *TAG* Kiomboi *Student Center* cha Mkoani Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wafanyakazi 37 kutoka Taasisi ya Mlezi *Foundation* ya Jijini Dodoma. Karibuni sana wageni wetu wote ambao mmetutembelea leo hii katika Bunge letu. *(Makofi)*

Katibu tuendelee.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu kwa hoja ya kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. Tutaanza na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas na Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo wajiandae.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninatumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hotuba yake aliyotoa jana. Kwa kweli hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa jana imefilisi sehemu ya hotuba yangu, imenipa funzo, na imenipa nafasi ya kutambua mambo kadhaa ambayo nitakuja kuyaeleza hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninamshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunajadili tunajadili bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini tuna Waziri Mkuu ambaye anatengeneza bajeti ya kwenda kutekeleza masuala ambayo tayari tumeshaona njia na namna ambayo anakwenda kutekeleza shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemshuhudia Waziri Mkuu kwenye ziara zake amefanya kazi kubwa ya kurejesha imani ya Watanzania kwa Serikali yao. Waziri Mkuu amefanya kazi kubwa ya kuonyesha umuhimu wa taasisi ya watumishi wa Halmashauri zetu kuwatumikia wananchi na kuweka kipaumbele kuwahudumia wananchi na siyo vinginevyo. Ninamshukuru na ninampongeza sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli watu wa Tanga baada ya ziara yake tumejifunza kwamba kumbe hata mambo ambayo tulikuwa tunaamini, hayawezekani, yanawezekana, na tena yamewezekana kwa muda mfupi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano mmoja, Waziri Mkuu wakati amekuja kwenye ziara Mkoa wa Tanga, ni jambo ambalo mnaweza kudhani ni jepesi, na siku zote nilikuwa nikisimama hapa nikizungumzia namna ya kwenda kuona changamoto za wananchi wanaoishi pembezoni Wilaya za pembezoni katika Mikoa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alienda kulala Kilindi katika Wilaya ambayo tangu imeumbwa hakuna Waziri Mkuu aliyekwenda kulala. Nalizungumzia hili kama mfano ili wale ambao wanawajibika, yaani watumishi wa Serikali walioko chini yake, waone kwamba kuna umuhimu wa kuwasaidia akina mama, wazee, watoto walioko vijijini kwa kwenda kuona kwa kushuhudia. Wazungu wanasema, kuona ni kuamini. Kwenda kushuhudia zile changamoto ambazo wanazipitia kwa kwenda kufanya ziara. Kwa kweli kabisa ninamshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu baada ya kwenda kule aliona shida kubwa ya maji kule Kilindi na alitoa maelekezo. Magari, mitambo ya kuchimba visima vya maji, yote ilikwenda. Mpaka tunavyozungumza, leo inachimba visima vya maji katika Wilaya ya Kilindi, Wilaya ambayo iko pembezoni na habari ya maji kwao imekuwa ni jambo kama vile mtu anahemea maziwa na asali kumbe ni maji ya kunywa na maji ya kutumia. Waziri Mkuu tunamwombea maisha marefu, Mwenyezi Mungu ambariki, dhamira yake ya kuwatumikia na kuwasaidia Watanzania iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Mawaziri wote walioko katika ofisi hii, lakini wakati ninataka kusimama kuchangia hoja yangu, nilipitia maandishi kadhaa. Mmoja wa wataalam anasema ukitaka kuwa mhutubi mzuri, lazima hotuba yako izingatie masuala manne. Suala la kwanza ni lazima hotuba yako isikike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza na kumshukuru sana Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa marekebisho na ukarabati wa vipaza sauti ndani ya ukumbi huu. Kwa kweli Bunge letu limekuwa la kisasa, unaongea kwa sauti ndogo, lakini sauti inasikika kila pahali. Ni mapinduzi makubwa, na ni dhamira ya kusaidia kwamba wawakilishi ndani humu tuweze kuzungumza na kusikika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nililojifunza, hotuba yako lazima iendane na wakati. Wakati tulionao sasa ni wakati wa kidharura kiuchumi. Tumeona namna ambavyo dunia inahangaishwa na suala zima la upungufu wa mafuta kutokana na vita ambayo inaendelea duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumepata mwongozo na dhamira ya Serikali imeonesha namna ambavyo inakwenda kubana matumizi kwa ajili ya kustahimili kuendana na dharura iliyopo nchini na katika dunia yetu. Pia hii imetolewa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na ninampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitamani sana leo nizungumzie masuala ya ajira. Nilitamani nizungumzie masuala ya kiutumishi. Nilitamani sana nizungumzie masuala ya mishahara na posho za watumishi, lakini kwa sababu ya wakati, kwa sababu ninajua tuko kwenye hali gani, tuko kwenye dharura za kibajeti za uendeshaji wa shughuli za Serikali na miradi yetu, ninajua tuko kwenye dharura ya namna gani, sitazungumzia masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitazungumzia masuala ya kiutumishi wala mishahara wala posho, nitajikita katika kuonesha yale maeneo mafupi ambayo kama tukiyashughulikia kwa udharura wake angalau tutapunguza makali kwa wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunazungumzia udharura wa upungufu wa mafuta kwamba unashindwa kujaza gari yako mafuta, unashindwa kufanya hiki na kile, wako wananchi vijijini tunakotoka, haya maisha ya dharura kwao ni maisha yao ya kila siku. Hana uwezo wa kufanya hicho ambacho wewe unajibana kukifanya wakati huu wa dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hao ni wananchi wa Korogwe Vijijini, Kata ya Magoma wapo maeneo ya Mkalamo. Wakati tunapitisha sheria kwa ajili ya kuanza kutekeleza Bima ya Afya kwa Wote, hatukufuta utaratibu, na ile sera ya kuwahudumia akina mama, wazee na watoto chini ya miaka mitano kuwapa matibabu bure. Hatukusema kuanzia sasa, kwa sababu tunakwenda kwenye bima ya afya, basi mwanamke aliyepo Mkalamo akienda kujifungua atozwe shilingi 200,000 mpaka shilingi 170,000, hatukusema hayo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyozungumza na wewe, hayo mambo yanatokea. Yanawatokea kwa akina mama katika maeneo ya vijijini. Ninakupa mfano, Mkalamo, Korogwe Vijijini, jana nimepokea hapa *message,* mwanamke hakuhudumiwa mpaka ndugu zake wamechangishana imefika shilingi 170,000/= ndipo akahudumiwa kwa ajili ya kutolewa mtoto tumboni. Ni jambo la ajabu, la kusikitisha, la kufedhehesha, halifai kuonekana katika ulimwengu tunaokwenda nao sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anapambana kuleta huduma ya afya kwa wote, wako watumishi kule chini wazembe tu, kwa *interest* zao tu, wameamua kutokumhudumia mwanamke kwa kuhakikisha kwamba wanalipwa kwanza fedha taslimu shilingi 170,000 ndipo wamhudumie mama mjamzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo halikubaliki. Ninaomba Wizara watakapokuja kutoa majibu kuhusiana na suala la huduma za afya, hasa huduma ya afya ya msingi, kule chini, kwa akina mama kule, waje na majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tupo kwenye kuhama kwenda kwenye utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, hawa ambao bado wapo kwenye *transition* hii, wanakuwa wanahudumiwa namna gani kabla hawajafika kwenye hatua ya kupata hiyo huduma ya afya kwa wote? Hawa akina mama wa kijijini wanahudumiwa namna gani? Je, zile sera, sheria na utaratibu wa mwanzo unakuwa umesitishwa au unaendelea? Huduma zao zinakuwa za namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la miundombinu ya shule. Hapa ninaomba nikupe mfano. Kwanza kiujumla katika utengaji wa bajeti zetu, ningeshauri tujikite katika kukamilisha ile miradi ambayo ni ya siku nyingi, ya zamani, miradi viporo, kwa sababu, haileti maana sana tukianzisha miradi mipya ilhali bado kuna miradi inayohitaji fedha haijakamilika, haijaanza kutoa fedha, huku bajeti kila siku tunatenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano. Kuna Shule ya Msingi Hemkeyu, ipo Lushoto. Hii shule imeanzishwa mwaka 1995. Tangu imeanzishwa haijakamilika hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku tunatenga bajeti, hivi huyu mwananchi wa Kijiji cha Mgwashi kilichopo Malindi pale ambaye anaiona shule ya tangu mwaka 1995 haijakamilika, mpaka leo ina upungufu wa vyumba vya madarasa, mpaka leo watoto hawana matundu ya choo, ilhali wakati sisi tunatenga fedha, tunajenga shule mpya, tunakarabati shule nyingine, huyu hajafikiwa. Hivi

anatumia busara na hekima gani kuielewa Serikali yake? Atumie hekima ipi kuielewa Serikali yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali, na kwa sababu tunajadili bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa, kwa kuwa bado Bajeti Kuu ya Serikali haijaja, wakati wanatuletea Bajeti Kuu ya Serikali, Serikali itusaidie, kipaumbele cha bajeti ya mwaka huu tuleteeni kukamilisha miradi ambayo imeshaanzishwa kwanza. Miradi hii ikikamilika, itatupa namna ya kwenda kuangalia miradi mingine mipya wakati hii ambayo imeanza imekamilika na wananchi wameanza kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo zahanati na vituo vya afya ambavyo vimejengwa vya kimkakati. Kwa hini kimkakati? Kwa sababu imefikia mahali Serikali imefanya kazi kubwa ya ujenzi wa vituo vya afya, zahanati zimejengwa kwa wingi, lakini bado kuna maeneo ambayo mwananchi hawezi kupata huduma ya afya kama hajatembea zaidi ya kilomita 50, 60 na 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano, Kituo cha Afya Ngwelo katika Jimbo la Lushoto Mjini, mwananchi ili afike Ngwelo, tena katika kipindi hiki cha mvua, inabidi atembee kwa miguu, hata pikipiki haiwezekani, na ni umbali wa kilomita 76 kutoka ilipo Hospitali ya Wilaya ya Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuulizane, wakati tunaangalia mazingira ya dharura ya kwenda na bajeti ya kidharura kwa kubana matumizi, huyu ambaye hapati huduma ya afya kabisa pale Ngwelo, ambaye barabara yake ni mbovu hawezi kufika kwenye kituo cha afya, ni kwa nini tusikamilisha ujenzi wa kile kituo akapata huduma pale ili mama mjamzito akajifungua pale, na mtoto chini ya miaka mitano akatibiwa pale, na hatimaye apunguziwe huo mlolongo wa kwenda tena kwa miguu na kuokoa vifo vya watoto na kina mama; kuokoa vifo vya wagonjwa vya jinsia zote katika maeneo hayo kwa kuwapatia angalau huduma ya afya ili wakati tunatafuta fedha za kujenga barabara na vitu vingine, tuwe tumeshaokoa maisha ya watu wa namna hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha kwamba bajeti inayoletwa ya Serikali iende kwanza ikatatue zile changamoto ambazo ni za lazima kwa wananchi wetu. Bajeti iende ikajibu matatizo ya changamoto za maji vijijini; bajeti ikajue changamoto za afya vijijini; bajeti ikajibu changamoto za elimu vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo mengine ya shughuli na miradi mikubwa ya maendeleo tutaendelea kutenga kadri inavyowezekana, lakini kwanza tuwaondolee dharura za kudumu wale watu wa vijijini wakati sisi tunapambana na dharura za kupita katika maeneo ya mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko. Tunaendelea na Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo ajiandae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kulihutubia Taifa langu la Tanzania kutoka Bungeni Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze na hadithi ya Mtume Muhammad *(S.A.W)* kama ilivyonukuliwa na Imam Tirmidhi. Hii ni hadithi namba 1954, na ninaomba niisome kwa kiarabu vile vile ilivyoandikwa; *lā yashkurun-nāsa lā yashkurullāh*. Kama hautamshukuru binadamu mwenzio ama watu, basi hata Mungu hutaweza kumshukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza na hilo kwa sababu ninataka kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hasa Mheshimiwa Rais. Hili nimetumwa na wananchi wa Kinondoni kwamba nije nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanyia Kinondoni ndani ya kipindi cha miaka mitano iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kazi iliyotukuka ambayo haijawahi kufanyika kwenye historia ya jimbo lile au wilaya ile. Hivyo, ninaomba hiki kitu kimfikie Mheshimiwa Rais mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, tunamshukuru kwa sababu ya nini? Tunamshukuru yeye na wasaidizi wake wote kwa sababu katika kipindi ambacho tumepata shida sana ya mafuriko katika Jimbo la Kinondoni, sasa tumepata mradi mmoja mkubwa ambao utaboresha na kubadilisha sura ya Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mkubwa sana ambao tulikuwa tumeuzungumza, Daraja la Magomeni, Daraja la Kigogo, Daraja la Mkwajuni, vyote hivi vinaonyesha kwamba haya ambayo yanafanyika ndani ya kipindi hiki hayajawahi kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tumeshuhudia miradi mingine mingi ya elimu. Katika jimbo langu lile hapakuwahi kuwa na *high school,* lakini safari hii tumekuwa na *high school* na watoto wanasoma pale. Barabara zimejengwa kwenye kila kata. Ingawa kwa udogo wake, lakini kazi kubwa imefanyika, na Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ninapenda vilevile nimpongeze Mkuu wa Mkoa, Albert Chalamila, kule tunamwita Aboubakar. Huyu bwana amefanya kazi nzuri. Vile vile, Mkuu wa Wilaya, ndugu yangu Saad Mtambule; Mstahiki Meya wa Kinondoni, Mheshimiwa Songoro Mnyonge; na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa, huyu dada anaitwa Hanifa Hamza. Hakika dada huyu ni kitu kingine; na mimi kila nikiswali ninapiga rakaa mbili kumwomba Mwenyezi Mungu asimwondoe pale Kinondoni abaki pale pale. Anatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kabla sijakwenda kwenye hoja, ninaomba uniruhusu niiombe Serikali igeuze na ilete macho yake pale Kinondoni. Tuna shida katika mito midogo midogo ambayo ipo ndani ya jimbo la Kinondoni. Kule Tandale, Ndugumbi, Kijitonyama, Mzimuni, na pale Mwananyamala kuna bonde la Msisiri, maji yanakuwa yanajaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo basi, tungeomba kazi hizo pamoja na ujenzi wa *fence* katika *secondary school* zetu, tuna sekondari inaitwa Salma Kikwete pale kijitonyama na sekondari nyingine iko Tandale inaitwa Tarimba Abbas, tunaomba sana Serikali itusaidie kutujengea uzio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nitumie muda wangu mwingi kuzungumzia Dar es Salaam. Sote tunakubaliana kwamba Dar es Salaam ni mkoa ama eneo ambalo ni kitovu cha uchumi katika Taifa letu. Ni mahali ambapo zaidi ya 80% ya mapato ya Serikali hukusanywa pale Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, hata kwenye mchango wa pato la Taifa, zaidi ya 17% inatoka pale Dar es Salaam. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba, endapo tutaisaidia Dar es Salaam itatuletea maendeleo, hasa sasa tukijua kwamba Dar es Salaam ni moja ya majiji yanayokua kwa kasi sana Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam ni jiji la tatu kwa kukua kwa kasi Afrika. Vilevile, katika dunia ni jiji la tisa ukuaji wake, na hata watu wanavyoongezeka, asilimia za ukuaji na za wingi wa watu, Dar es Salaam iko zaidi ya wastani wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wastani wa Taifa ukuaji wake ni asilimia mbili nukta nane kwa mwaka, lakini Dar es Salaam tunazaana sana, tuko asilimia nne nukta tisa. Watu wanazaana sana Dar es Salaam, wanaongezeka sana. Sasa watu wanavyozidi kuongezeka maana yake ni nini? Yawezekana kuongezeka kwa watu na kupanuka kwa jiji ni neema kwa namna nyingine, kwa sababu watu ndio wanaosaidia kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbukeni, watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora, hivi vitu tunavyo. Watu wanaongezeka, hivyo tutumie Dar es Salaam kuipa yale ambayo pengine yakipatikana kwa urahisi yatasaidia hata katika maeneo mengine; na kwa hapa ninajikita kwenye shughuli ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa sana imefanyika na nchi hii, na Serikali yetu imejitahidi sana kuweza kufanya kazi za

kuiletea maendeleo Dar es Salaam na Taifa letu. Dar es Salaam pale tulikuwa na miradi ya *DMDP I* na *DMPD II* katika kuboresha masuala ya miundombinu ikiwemo ya barabara. Kiukweli hali ile, na juhudi zile, pamoja na kwamba ni nzuri na bora, zinabadilisha jiji, lakini ukweli bado tunahitaji zaidi barabara Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nitumie takwimu za pale Kinondoni. Katika Jimbo Kinondoni tuna mtandao wa barabara wa kilomita 198.34. Hata hivyo, barabara ambazo zimetengenezwa kwa lami na zege nii kilomita 58, sawasawa na 29% tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti na ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, wenzangu pamoja na Serikali, siyo hesabu mbaya, ni hesabu nzuri. Juhudi kubwa sana zimefanyika, kilomita 58, lakini ukiangalia kipindi ambacho sisi kama Taifa, uhai wetu, utaifa wetu, tumetumia miaka 64 au 65 kufikia hapa tulipo. Sasa ukifanya hesabu, siyo kwamba ninabeza kazi ambayo imefanyika, hapana, ninajaribu kuangalia hesabu. Wanasema hesabu zinatuambia, kwamba katika kipindi cha miaka 64 tumejenga kilometa 58.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua hata maeneo mengine kazi kubwa sana imefanyika, lakini ukipiga mahesabu ya wastani unaona kama ni *less than a kilometre*. Ni chini ya kilomita moja kwa mwaka, sasa hiyo siyo hesabu nzuri. Ukionyesha hivyo, ni kwamba huu ni mji ambao ndiyo unatakiwa utupe tozo ya mafuta. Watu wanywe mafuta mengi, gari zitembee sana ili mafuta mengi yale tozo yake iende ikasaidie mikoani huko na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ukiangalia fedha ambazo Serikali huziingiza katika ujenzi wa barabara, pamoja na kwamba kumekuwa na ongezeko kubwa, sasa hivi bajeti inakwenda kuwa shilingi trilioni 1.2, bado haitatosheleza kwa sababu fedha hizo pia zinategemea sana tozo ile wanaita ya *Road Fund*. Fedha zile hata zikikusanywa, kuna tabia sasa hivi ya Serikali kutokuzipeleka zote zile huko mikoani na majimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kupitia Bunge hili isimamie kwa ukamilifu na tuheshimu sheria zinazopitishwa na Bunge hili, kwamba kama fedha ni *ring fenced,* basi zitumike kwa majukumu yale yaliyokusudiwa. Kwa wale ambao wanakaa katika Kamati mbalimbali, wanazo kumbukumbu kwamba fedha hizi hazifiki kwa idadi inayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ningeomba kwenye hili suala la kutafuta fedha kwa minajili ya barabara, lipewe kipaumbele kwa sababu barabara ndiyo moja ya nyenzo muhimu sana ya kutupatia maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, nilikuwa nina jambo ambalo tumelizungumza kwenye Kamati ya Fedha pale Manispaa. Nilipata nafasi ya kwenda kwenye Kamati ya TAMISEMI wakati Mkoa wa Dar es Salaam ulivyokuwa unapeleka hoja zake pale, nilipata nafasi ya kusimama na nikazungumza. Nilivyokuwa nimezungumza, nimeomba yafuatayo: Kwamba ni kweli fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya barabara hazitoshi, lakini kwa Kinondoni…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba unipe angalau dakika moja. Kwa Kinondoni tumelizungumza kwamba je, hatuwezi tukakopa benki na sisi tunakopesheka? Halmashauri yetu kwa mwaka inatenga shilingi bilioni nane kwa ajili ya barabara. Kama tunaweza tukakopa fedha sawa na kujenga kilomita angalau 100 kwenye Wilaya ya Kinondoni, hata kama ni kwa kulipa kwa miaka 10, halmashauri ina uwezo huo. Hivyo, tunaandika andiko na kulileta Serikalini kuomba idhini na Serikali ituruhusu tuweze kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Kinondoni tuko tayari, tuwe mfano mwema ili halmashauri nyingine ziweze kuiga, kuboresha na kuisaidia Serikali katika ujenzi wa barabara za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuweza kulihutubia Taifa langu hili la Tanzania. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Ahmed Shabiby na Mheshimiwa Patali Shida Patali, wajiandae.

**MHE. DKT. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mola ambaye ametufikisha katika Bunge hili la Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninaomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana, sana, sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na hasa hotuba yake ya jana imetuonyesha nini maana ya kiongozi makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa mambo mazuri ambayo jana alitoa maelekezo kama kuonyesha *leadership* katika upande wa mafuta. Mimi nina imani tutatoka salama katika eneo hili, na nchi yetu itazidi kusonga vizuri. Kwa hiyo, tumwombee sana Mheshimiwa Rais ili apate nguvu, na pia Mungu azidi kumlinda katika kutimiza majukumu yake ya kikazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ambayo imekuja hapa; pamoja na wasaidizi wake wote walio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwona hapa *mate* wangu Mheshimiwa Prof. Shemdoe. Hakika anaitendea haki Wizara ya TAMISEMI. Hongera sana na aendelee kuchapa kazi, ninamwamini, hakuna litakaloharibika. Songa mbele, chapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunajadili hotuba hii, ninaomba tufanye rejea. Mwezi Machi, 2021, bajeti ya TAMISEMI kupitia *TARURA* ilikuwa ni wastani wa shilingi bilioni 273.6. Katika kipindi ambacho Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliposhika haya Madaraka, leo hii tunazungumzia bajeti ya karibu shilingi trilioni 1.2. Hii ni *outstanding performance*. Tuna kila sababu kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa maono yake haya makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunawaomba TAMISEMI, na mimi ninawaomba, kule kwangu Kisarawe nina Barabara ya Mzenga – Gwata sasa hivi haipitiki, hali ni mbaya. Barabara ya Msimbu – Homboza – Masaki; Barabara ya Msanga – Visiga – Maluwingwata na Barabara ya Chole – Kisangiri – Kihale – Vikumburu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri wa TAMISEMI, watu wake wa *TARURA,* ninajua kule *engineer* wetu wa *TARURA* anafanya kazi vizuri. Seff anafanya kazi vizuri na timu yake, waje kule watie nguvu kufungua maeneo hayo, watu wapite vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, tuhame sasa tuanze utaratibu wa kutengeneza barabara za zege katika baadhi ya maeneo. Katika maeneo korofi utakuta barabara ni ya kilomita 100, lakini inawezekana watu wanashindwa kupita katika eneo la wastani wa kilomita moja au 1.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo hayo tuyaainishe, tutengeneze zege ili wananchi wetu waweze kupita, na ninaomba ikiwezekana jambo hilo mje kulianzia pale Kisarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa leo nimekuja kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, kwanza Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa, toka alipoingia amekuwa Rais wa mfano. Watu waliopata ajira kipindi cha Mama Samia haijawahi kutokea. Amejitahidi sana kutoa ajira, na hata hivi juzi juzi naambiwa kwamba vijana wengine wanaenda kufanya *interview*. Hii ni kazi kubwa, tuendelee kumwomba na mwendelee kumwombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninataka kuwashawishi Waheshimiwa Wabunge, mimi nimedhamiria katika kuunga juhudi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, nimedhamiria kuja na hoja binafsi hapa Bungeni ya kusaidia vijana wa Kitanzania angalau tuweze kuwa na programu maalum ya hata *part time payment* ya miaka mitatu. Hoja hii nitapitisha utaratibu ule wa hoja binafsi kuweza kuiwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu ikikupendeza inawezekana ukalichukua wazo hilo kabla ya hoja binafsi. Mpango wangu mkubwa ni kwamba, leo hii ukienda, utakuta vijana wa bodaboda wote ni *graduates,* wengine wana *masters*. Siyo hivyo tu, Waheshimiwa Wabunge hapa ninyi wote kila mtu katika familia yake ana ndugu ambaye hajapata ajira, ni changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kulishawishi Bunge hili, tuje na mpango wa ajira. Kuanzia sasa tunapotengeneza suala zima la *vision 2025* tuhakikishe tunakuja na programu ya *Part Time Employment* kwa vijana wetu, ambayo hii tutaweka katika *categories* mbili, wale wa *diploma* na wale wa *degree*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu achukue wazo hili, kila mwaka tuchukue vijana 50,000 wale wa *diploma*, tuweke walau *allowance* ya kulipa shilingi 500,000, na wale wa digrii tuwalipe shilingi 700,000 ambapo wapate *contracts* za miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hesabu hiyo ukichukua, wa diploma tuchukue wastani wa 20%, na 80% wawe wa *degree* na kuendelea ambapo vijana 50,000 maana yake tutahitaji vijana 10,000 kwa mwaka na vijana 40,000 kutengeneza idadi ya vijana 50,000 ambao mahesabu yake katika eneo hilo ni sawasawa na shilingi bilioni 396.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii, kama Waheshimiwa Wabunge, hatuwezi kushindwa kufanya maamuzi ya vijana wetu ambao wako mtaani kuhakikisha kwamba wanapata ajira za mikataba za miaka mitatu mitatu. Vijana hawa tuweze kuwa-

*groom* vizuri ambapo wataweza kupata maarifa ya kazi na tutaondoa *frustration* kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu akiridhia, endapo jambo hilo litaridhiwa, kipaumbele, tutaanza na vijana wale wa bodaboda ambao ni *graduates,* wako mtaani, na vijana wengine ambao ni walimu wanaojitolea katika vyuo vyetu, manesi na madaktari. Sasa hivi tunafanya uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya afya, elimu na sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili litatusaidia sana kuhakikisha vijana wetu wanapata ajira. Mpango huo, wale ambao watapata ajira watakuwa wanaondoka, tuna-*enroll* vijana wengine kila mwaka. Tukiwa na *guarantee* ya kuchukua vijana 50,000, tutakuwa tumemsaidia sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwasaidia vijana wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alichukue, au kama asipolichukua, nitaleta hoja binafsi hapa Bungeni. Lengo kubwa ni kuwasaidia vijana wetu wa Kitanzania. Hii itakuwa ni dhana ya kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kazi kubwa anayofanya ya kuajiri vijana wetu. Tukifanya hivi, tutasaidia Taifa letu hili, tutawasaidia vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili litasaidia na nitaomba katika eneo hilo, Kamati za Bunge zile *oversight committees* (Kamati ya *LAAC* na Kamati ya *PAC)*, mapato haya ya vijana wetu angalau tutoke 10% katika *own source*. Tunafahamu *TR* kila mwaka, *dividend*, sasa hivi tumeweza kukusanya zaidi ya shilingi trilioni moja. Angalau huku watoe 10% katika eneo hilo kusaidia mfuko huo ambao utahitaji shilingi bilioni 396 kusaidia jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo jambo kama nilivyosema, nitakuja na hoja binafsi, lakini ni imani yangu kubwa Mheshimiwa Waziri Mkuu atalichukua hilo, na mimi nitawasilisha *proposal* hii mezani kwake leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupa *copy* ya *proposal* na Waheshimiwa Wabunge nitatuma *proposal* hii katika *group* la Wabunge kuona mawazo haya tuyafanye vipi? Tuwasaidie vijana wa Kitanzania. Tutakuwa tumefanya jambo kubwa la kithawabu na hakika Mwenyezi Mungu atatulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, tukifanya hivyo, tutaonesha *leadership* yetu kama ni viongozi ambao tunaona tatizo, tunatafutia majawabu ya tatizo. Bila kufanya hivyo, tutakuwa na vijana ambao wanalalamika, lakini bila kufanya hivyo, tutakuwa hatuungi mkono juhudi za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kila mwaka anatoa ajira kwa vijana. Sisi kama Waheshimiwa Wabunge tuwe na mkono wetu kiasi kwamba tunaweka misingi mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo naomba lisiwe katika utaratibu ule wa kawaida wa vibali vya Ofisi ya Rais, Utumishi. Likija kupita, maana yake liwe katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, katika halmashauri, vijana waweze kupata ajira katika halmashauri zao. Itasaidia hata wale vijana wengine wa Kakonko, wa Kisarawe, wa Buhigwe, wa Nyasa waweze kuajiriwa maeneo yao hayo hayo wapate ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tutaweza kuondoa *discrimination* ambayo ni namna ya kusaidia vijana wengi wa Kitanzania kupata ajira. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu achukue wazo hilo. Hata hivyo, nitaangalia kama Mheshimiwa Waziri Mkuu akiona bado, nitaleta hoja binafsi, lakini imani yangu kubwa, nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu achukue hoja hiyo na *proposal* hii nitaiwasilisha kwa Ofisi ya Waziri Mkuu na wasaidizi wote, pamoja na Kiti chako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawasilisha katika Kamati na *group* letu la Wabunge tuweze kusaidia jinsi gani kuona kwamba wazo hili tuwasaidie vijana wa Kitanzania ambao hakika wanatutegemea sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu libariki Bunge hili, Mungu mbariki Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo. Nilimtaja Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Patali Shida Patali, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga na Mheshimiwa *Eng.* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge wajiandae.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi kuwa mmoja wa wachangiaji katika Hotuba ya Waziri Mkuu. Ninajua kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu huwa tunaogelea kwa sababu yeye ndiye Mtendaji Mkuu wa Serikali, kwa hiyo tunaongea chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kutoa pongezi ya kwanza kwa sababu leo tumeona nchi jirani yetu mafuta hawana kabisa. Kwa hiyo, natoa pongezi kwa Serikali, leo hii nchi yetu ina mafuta na sisi wengine kama tulivyosema ni wachunguzichunguzi tunajua mpaka ya Mei yapo. Pia, ninawapongeza kwa kutafuta mafuta mpaka Ulaya kwa sababu najua kuna meli zinazokuja sasa hivi zinatoka nchi za Ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninapongeza hivyo ila ninawashauri tu kwamba waendelee kuchakata kwenye hizi baadhi ya tozo watoe ili kidogo iwaletee Watanzania nafuu. Hiyo nataka kutoa pongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kama walivyojikita wenzangu, akina Mheshimiwa Tarimba na wasemaji wengine waliopita kuhusu habari ya barabara. Kwenye barabara zote *TANROADS* pamoja na *TARURA,* kwanza watendaji wao wakuu wanafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *TARURA* na *TANROADS* na watumishi wote wako vizuri ila kwenye upande wa kesi imekuwa shida. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aangalie hiki kitu, leo tunazungumza tu kwamba kuna hiki na kuna hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua nchi yetu imetoka kwenye chaguzi mbili za Serikali za Mitaa pamoja na chaguzi kuu, kuna shida ya fedha, lakini tukiangalia wananchi hawajui hilo, wanachotaka kuona ni barabara zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kama kule jimboni kwangu kwenye hii mvua, madaraja mengi yameondoka, barabara nyingi zimekatika. Ukiangalia kwenye upande wa *TANROADS*, Daraja la Matale sasa hivi limeshakuwa shida na lile linaunganisha kati ya Gairo na kata nyingi pamoja na Kilindi. Kwa hiyo, Daraja la Matale limekuwa shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo huko tu, ukienda hata kwenye barabara kuu Dodoma – Morogoro imekuwa shida, ukienda Dar es Salaam – Lindi imekuwa shida, ukiangalia Singida – Nzega shida, ukiangalia Katesh kwenda mpaka pale Babati ni shida. Sasa kama tumekaa na hakuna ufumbuzi wa aina yoyote, itakuwa ni shida tukisema kwamba tungoje sijui kodi za mafuta, tungoje hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu, Mheshimiwa Tarimba pale alisema kama inawezekana Serikali ikope. Kama kuna mikopo nafuu, ikope itengeneze hizi barabara. La sivyo, zitaongezeka. Mwisho Serikali itashindwa kutengeneza barabara zote kwa sababu tuna kilometa zaidi ya 15,000 za lami. Sasa barabara zote zikianza kufa kufa zitatengenezwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tujikite humu tuangalie kama kuna mikopo nafuu, Serikali ichukue, tuache habari hiyo ya kuogopaogopa hivi vitu. Ilimradi tu ni kwamba hii mikopo haina ufisadi, iko salama, tukope barabara hizi zitengenezwe. La sivyo, nchi nzima itakuja kwisha barabara zote kwa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza kuhusu habari ya majengo. Hata kuna dada yangu hapa alizungumza alikuwa wa kwanza. Haya majengo mengine yamejengwa na wananchi. Mwananchi kaamua kujenga nyumba ya mtumishi kwa sababu

wanawapenda watumishi wao huko vijijini, wameamua kujenga darasa, wameamua kujenga labda zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kama pale Magoweko Kata ya Gairo, watu wamejenga zahanati iko muda mrefu kwenye lenta, lakini zikija fedha zinatafuta miradi mipya badala ya kumalizia ile. Mngekuwa mnatoa hii miradi ya kumalizia hizi zahanati na haya madarasa na vitu vingine. Mwaunge mkono wananchi, wapate nguvu hata siku nyingine waendelee kujitolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna lingine la bandari kavu. Hili naona sasa tulikaa hapa Bungeni tukajadili, na mimi labda ndiyo nilikuwa mtu wa kwanza saa nyingine kwenye kuzungumzia kuweka bandari kavu pale Kwala, kwa sababu pana reli ambayo inaunganisha na ile bandari, ile reli ya kwenda Arusha. Bandari ile kavu ilikuwa imejengwa kwa lengo moja tu la kupunguza foleni kwenye Jiji la Dar es Salaam na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari ile imefunguliwa na Mheshimiwa Rais na mara ya kwanza miaka minne nyuma, wale watu wa bandari wenyewe walinunua vichwa vya treni viwili. Baadaye wakavikabidhi kwa watu wa reli *(TRC)* kwa ajili ya kuchukua tu makontena pale bandarini kuleta kwenye bandari kavu ya Kwala ambayo hamna foleni wala nini kupanda treni. Pia, juzi tumemsikia Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi tena, anasema wana vichwa vitano vya treni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, haya maneno yamekuwa hadithi, bado kuna swali mimi najiuliza. Je, huu mpango kuna rushwa inatembea? Kwa sababu leo ukienda Dar es Salaam, ukienda Mwenge, ukienda hata maeneo ya Jeshi, hata ukienda pale Jangwani, kila kona ukienda, Temeke, ni makontena tu bandari kavu. Kwa hiyo, mnazidi kuongeza foleni kwenye lile jiji kwa sababu unapotoa bandarini kwenda kwenye *dry port* za mjini, unatumia magari, hamna reli pale. Kwa hiyo, mnaongeza tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ile bandari kavu ina mahekta na mahekta pale Kwala. Kwa nini watu hawataki kutumia ile

bandari kavu? Kuna kitu gani? Wanataka tu kutumia zile bandari kavu za watu binafsi. Kuna nini hapo? Hii bandari kavu ambayo watu wa bandari wenyewe hawaitumii, kwa hiyo, kuna foleni, *accidents* nyingi. Jiji la Dar es Salaam lina foleni nyingi, na sasa tena mmeongezea, maana yake sasa hivi mnatoa vibali kina kona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenge bandari kavu, ukienda sijui mpaka Bunju bandari kavu, ukienda wapi bandari kavu na hakuna *logistics* zozote za kupeleka hivyo zaidi ya kutumia barabara. Kwa hiyo, badala ya kupunguza, sasa mnaongeza tena foleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na ninamwamini kwamba aangalie hivi vitu, kuna kitu gani? Hizi bandari kavu tumezungumza muda mrefu sana, sasa kuna haja gani ya kuweka Bandari ya Kwala?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi hapa mkija, watu wana mipango mipya, unasikia sasa hivi tunajenga bandari kavu Dodoma. Yaani tayari ile iliyoko pale imejengwa, imeisha, ina vifaa, haifanyi kazi. Mnapanga mpango wa kwenda kujenga bandari kavu tena nyingine. Kwanza hii ianze kazi, halafu ikitoka pale ije sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, na tunamwamini, afuatilie hivi vitu kwa sababu unajua vitu vingine siyo mpaka uwe mtaalam, uende ukasomee. Hivyo, hata vitu vya kusomea hapa kwamba kuna ulaji, unaliwaliwa hapa, mpaka uende shule! Si hata kwa macho unajua tu hapa tayari! Ndiyo maana yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi ukaweka bandari kavu; pale Kwala ipo, imegharimu na kila siku watu wanaenda wanajisifu tuna hiki, tuna hiki, kazi haifanyiki, foleni iko pale pale. Ile inaweza ikachukua hata mlete meli 100, kwa sababu wana eneo kubwa mahekta kwa mahekta. Nini kinachosumbua mpaka ile bandari kavu isifanye kazi? Ukiambiwa inafanya kazi, ni vikontena vidogo tu vya kufurahisha furahisha watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Jiji la Dar es Salaam limekuwa na foleni za kutosha, na lazima tuishukuru sasa hivi *NSSF* kwa kukubali kujenga barabara sita kutoka Dar es Salaam mpaka pale Chalinze. Pia, tuwashukuru bandari wenyewe wako kwenye mazungumzo, nao wakubali, hata walazimishwe kujenga barabara ya kutoka Chalinze – Morogoro iwe barabara sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine, taasisi kama hizi zilazimishwe kutengeneza barabara huko mikoani. Kuna foleni kwa mfano ile ya kutoka, (maana yake mimi ni *transporter)*, kutoka pale Tunduma kuja mpaka Mbeya. Pale siyo pa barabara nne, hii barabara sita zimeimbwa miaka na miaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi utakuta tu madereva wanapiga picha, wanakula ugali, wanasonga ugali maana yake mtu kutoka Mbeya mpaka aje afike pale Tunduma ndani ya nchi moja tu anatumia siku nzima au siku mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi taasisi za Serikali zenye fedha zilazimishwe kufanya vitu kama hivyo, siyo kila kitu tutumie wageni tu. Tunangoja sijui *PPP*. *PPP* wakati tuna taasisi zenye fedha, tunaweza tukafanya nazo *PPP,* siyo mpaka tungoje aje Mchina, aje nani, haiwezekani kitu kama hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sikuwa na mengi ya kuzungumza. Nakushukuru sana, na ninaunga mkono hoja. Nafikiri Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo hapo, lakini huko alipo naamini atakuwa amenisikia.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ahmed Shabiby. Nilimtaja Mheshimiwa Patali Shida Patali, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mheshimiwa Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge na Mheshimiwa Sara Msafiri wajiandae.

**MHE. PATALI S. PATALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii uliyonipa nami kupata machache ya kuongea juu ya Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu. Naomba kumpongeza

Mheshimiwa Waziri Mkuu, na hapa ninapongeza ziara anazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo utekelezaji wa zile ziara bali ninachokipongeza ni mtazamo mpya tunaoupata juu ya utawala bora kwenye nchi yetu. Kwenye vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2026/2027, mapendekezo ya vipaumbele yako Matano, na cha kwanza ni kuimarisha utawala bora, demokrasia, amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utawala bora nafikiri ndicho hiki kinachofanyika na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hili jambo litupe somo kuona kuna haja ya kufumua *SOP* za utendaji wa Serikali. Tunapoona Mheshimiwa Waziri Mkuu wananchi wengi wanamkimbilia kwa ajili ya kupeleka matatizo yao, maana yake mfumo mzima wa Serikali kuanzia ngazi za vijiji mpaka huku juu kiutendaji ume-*relax*. Hii ndiyo hoja yangu ya pongezi juu ya ziara anazozifanya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kuchangia mchango wangu madhubuti kwenye eneo la kwanza hapo hapo kwenye vipaumbele, mapendekezo ya vipaumbele kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2026/2027 Na. 05 ambavyo ni vichocheo vya mageuzi, ndani kwake kuna nishati na miundombinu. Nami najikita kwenye miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana hapa kwa sababu ya muda, nitaenda haraka haraka kidogo. Mwanafalsafa mmoja amesema *"Where a road passes, development follows."* Hatuwezi kulitenga Taifa letu, hatuwezi kujitenga na maendeleo tunayoyahitaji bila kuwa na miundombinu madhubuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shabiby ametoka kuzungumza hapa juu ya miundombinu hasa barabara. Naomba kujikita kuzungumzia barabara moja muhimu sana Nyanda za Juu Kusini ambayo ni barabara ya *TANZAM*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kihistoria, Mkoa wa Mbeya, na hapa tunamshukuru Mheshimiwa Rais, ametupatia fedha shilingi

bilioni 138 kwa ajili ya utengenezaji wa barabara nne Mkoa wa Mbeya. Kwetu hili ni jambo kubwa, na tunaamini linaenda kufungua uchumi wa Mkoa wa Mbeya ikiwepo kumaliza foleni ambazo zimekuwa kero kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango wa njia nne *lot* ya tatu, itaanzia Igawa mpaka Tunduma karibia kilometa 218. Hoja yangu ni nini hapa? Naomba niishauri Serikali itazame matengenezo ya barabara hii kwa njia ya dharura. Barabara hii ndiyo barabara pekee ambayo ni mlango wa zaidi ya nchi tano za *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inahudumia nchi ya Zambia, Malawi, *DRC* Congo, na Botswana. Barabara hii kupitia *transit* inahudumia mpaka *South Africa* na ni barabara yenye mchango mkubwa kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza hivi sasa, barabara hii imechakaa na ipo hali mbaya. Ukipita barabara hii lazima utakutana na magari yasiyopungua matano mpaka sita yaliyoharibika. Sasa nini ninachotaka kusema? Kwa umuhimu wa barabara hii ambayo 70% mpaka 75% ya mizigo ya *transit,* unaoshuka Bandari ya Dar es Salaam unaelekea kwenye hizi nchi za *SADC,* maana yake kuna *risks* ambazo tunazitengeneza kama nchi bila kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wastani wa siku moja, magari 1,500 mpaka 2,000 yanatumia hiyo barabara; hayo ni yale ya *transit* ukiacha yale ya kila siku yanayosafirisha mizigo. Naziona *risks* ambazo ni muhimu tuanze kuzi-*address* mapema. Moja ya *risk* kubwa, tunatoa fursa kwa bandari shindani za nchi zetu kuanza ku-*take over* kwenye soko la usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Bandari ya Beira ambayo ipo Mozambique, hii bandari ni mshindani mkubwa wa bandari yetu ya Dar es Salaam. Sasa magari yanayoanza kuharibika, kama mtu anaagiza gari kwa gharama ambazo ni *fixed,* zinafika Dar es Salaam anakomboa, gari linaharibika matairi, gari linaharibika rimu, maana yake tunamwongezea gharama huyo mwagizaji wa

hilo gari na kuanza kufikiria mara ya pili atakapoagiza ni njia ipi atakayotumia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna bandari nyingine ya Durban – *South Africa,* hii inatulazimisha, nayo inawalisha Kongo, inawalisha wenzetu wa *Mozambique*. Hii inahatarisha kusababisha wale ambao wateja wetu wanaoagiza magari kupitia Bandari ya Dar es Salaam waanze kufikiria kuagiza magari kutumia hiyo njia hasa kutumia Bandari ya *South Africa* ambayo ni Durban.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya ninayoyasema, natambua kuna makubaliano ambayo yanaenda kuboresha bomba la mafuta ambalo linatoka Dar es Salaam mpaka Zambia. 70% ya mafuta ya dizeli yanasafirishwa kwenye hili bomba la mafuta ni 20% mpaka 25% mpaka 30% tu ambayo yanasafirishwa kwenye haya magari makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kihatarishi kingine kama nchi, ni kwamba haya makubaliano yakianza kutekelezwa ya marekebisho ya hilo bomba, maana yake yale mafuta ambayo yalikuwa yanasafirishwa kwa hilo bomba, na kwa sababu Zambia inategemea haya mafuta kwenye uendeshaji wa nchi, yatalazimika kusafirishwa kwa magari. Serikali, imejiandaa vipi kisaikolojia kupokea mabadiliko ya wakati wa matengenezo wa hilo bomba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa hivi barabara hiyo bado inashindwa ku-*accommodate* magari yaliyopo kwa sababu ya uharibifu uliopo, likiongezeka na hili, maana yake inaweka changamoto kubwa ambayo itasababisha msongamano mkubwa wa magari hasa kwenye mpaka wetu wa Tunduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe kwa hoja hii kuiomba Serikali kuja na mpango wa dharura wa ukarabati wa barabara hii ili kuendelea ku-*maintain* soko letu la usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nimesema nitajikita kwenye miundombinu. Ninaomba nizungumzie *TARURA*. Hapa naomba nizungumzie Jimbo la Mbeya Vijijini. Jimbo la Mbeya

Vijijini lina kilomita 1,033 za mtandao wa barabara, bajeti ya *TARURA* ni shilingi bilioni 2.7 tu ya utekelezaji za matengenezo na marekebisho ya hizo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara muhimu sana ambazo ni msaada mkubwa kwa ukuaji wa Jimbo la Mbeya Vijijini, wananchi wake kiuchumi tuna barabara ya Mbalizi – Shigamba kilometa 52, tuna barabara ya Isonjye – Kikondo, tuna barabara ya Mbalizi – Chang'ombe. Tunaomba sana zile barabara zote ambazo zipo chini ya *TANROAD* kama hizi nilizozitaja, tuone kwenye bajeti hii inayokuja kupitia Wizara ya Ujenzi zimekuwa *contained*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile ambazo ni za *TARURA*, tuombe kaka yangu Mheshimiwa Profesa Shemdoe, Wizara ya TAMISEMI kuona uwezekano wa ku-*provide* bajeti inayotosheleza Jimbo la Mbeya Vijijini. Hivi ninavyozungumza, kata zaidi ya sita hazina mawasiliano wala hazipitiki. Ukitoka Ilembo kwenda Kata ya Shizuvya hakufikiki kwa sababu barabara imevunjika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka Igoma kwenda Kata ya Ilungu, hakufikiki kwa kuwa barabara imekatika, yote haya inatokana na ufinyu wa bajeti ambayo ipo chini ya *TARURA* kwa ajili ya kutekeleza matengenezo na maboresho ya hizi barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka naomba nizungumze kidogo kuhusiana na suala zima la sekta ya kilimo. Mbeya Vijijini 85% mpaka 90% ya shughuli yetu ni kilimo, shughuli za kiuchumi. Bado tuna uhaba sana wa masoko ya mazao tunayozalisha, tuione Serikali kupitia bajeti hii ikiweka vipaumbele vya ujenzi wa masoko hasa Jimbo la Mbeya Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbeya Vijijini ndiyo Jimbo pekee ambalo linaongoza kwa uzalishaji wa viazi, lakini hivi tunavyozungumza, hatuna mahali pa kuuza viazi, ndiyo Jimbo pekee ambalo linazalisha pareto kama zao la biashara nchi nzima lakini hivi tunavyozungumza bado *stability* ya soko la *pareto* haijakaa vizuri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzunguzaji)*

**MHE. PATALI S. PATALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ione katika namna ya mapambano, huku tunakoelekea kujenga uchumi wakati wa juu ione namna ya kuanza na kuboresha masoko ya mazao kwa wafanyabiashara. Kuna jambo moja nilikazie, nilifurahi Hotuba ya Waziri Mkuu akizungumza na kukemea kupiga marufuku hivi vitu vinavyoitwa lumbesa. Moja ya jambo kubwa ambalo linatesa sana wakulima ni lumbesa. Hapa niishauri Serikali, hili alilosema Mheshimiwa Waziri Mkuu lisiishie kwenye maneno, liletwe hapa Bungeni tutunge sheria ambayo inatoa katazo la lumbesa kwa wakulima. Hii ndiyo njia pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo huja na kupita. Litapita kama mengine yanavyopita, lakini ikiwepo sheria, maana yake miaka yote itakuwa ikidumu kuwalinda wakulima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana, kengele ilishalia muda mrefu.

**MHE. PATALI S. PATALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naomba kuunga mkono hoja... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, naomba tutambue wageni ambao wapo Bungeni muda huu ambao ni wageni wanafunzi 169 na walimu 14 kutoka Shule ya Awali na Shule ya Msingi Feza ya Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika wanafunzi hawa, tuna wanafunzi ambao ni watoto wa Waheshimiwa, tuna Lisa Stephen, mtoto wa Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Bunge, Mheshimiwa Cecilia Paresso, pia tuna Jolin Kafulila, mtoto wa Mheshimiwa Jesca Kishoa; tuna watoto wawili, Jensen na Jallen, watoto wa Mheshimiwa Juliana Shonza, karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Shule ya Feza ya Awali na Msingi ya hapa Dodoma katika Bunge letu kwa ajili ya mafunzo. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea, nilimtaja Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi

Ulenge, Mheshimiwa Sara Msafiri na Mheshimiwa Festo Sanga wajiandae. *(Makofi)*

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hii Hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na uzima nimeweza kusimama hapa leo ndani ya Bunge la Kumi na Tatu nikiwa Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini katika vikao vya Chama na kuweza kuniteua kuwa mgombea wa Jimbo la Tabora Mjini. Ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Tabora Mjini kwa kuniamini na kunipa kura za kishindo kuja kuwawakilisha katika Bunge hili la Kumi na Tatu. Ninawaahidi sitawaangusha, nitafikisha yale ambayo wanataka niyafikishe katika Bunge hili na kwa Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na wachangiaji wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, na pia kwa Hotuba yake ya jana. Kwa kweli ukiisikiliza kwa umakini, basi utajua kwamba tunaye kiongozi wa namna gani kwenye Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutuletea fedha nyingi katika Jimbo la Tabora Mjini kwa ajili ya ujenzi wa shule za msingi pamoja na ukarabati. Pia tumeletewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa zahanati katika Kata ya Ikomwa, lakini bado kuna fedha nyingine ambazo zimeletwa katika miradi mbalimbali katika Jimbo la Tabora Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Rais, mama yangu mpenzi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuliona Jimbo la Tabora, na Mkoa mzima wa Tabora. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuuona Mkoa wa Tabora na mikoa mingine ya pembezoni ambayo tumekuwa tukizungumza mambo mengi, na tangu ameingia, ameweza kuyatendea haki kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika hii Hotuba ya Waziri Mkuu, nami nitajielekeza kwenye Wizara ya TAMISEMI. Nilikuwa nataka kufahamu, na hili suala ninaomba sana Serikali iweze kutupa majibu sahihi na majibu ya uhakika ili tuweze kuwa na majibu kwa wananchi wetu, lakini kwa viongozi wetu ambao tumekuwa tukifanyanao kazi kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimekuwa ni kilio kikubwa sana kwa Wabunge wengi katika Bunge hili kutaka kujua mustakabali wa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa katika maeneo yetu. Sisi ni Wabunge, tunafanya kazi kwa kushirikiana na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, lakini tunafanya kazi kwa kushirikiana na Madiwani kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Wenyeviti wa Serikali za Mitaa limekuwa kama lina kigugumizi kidogo. Viongozi hawa, wako kisheria kwa sababu tunafanya uchaguzi kila baada ya miaka mitano kuchagua Wenyeviti wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutambue kwamba Wenyeviti kwenye mitaa yetu, kwenye vijiji vyetu, kwenye vitongoji vyetu ndio watu wa kwanza wakilala wanalala na wananchi wao na wakiamka nao kwenye changamoto na matatizo yao. Wamekuwa wakipokea kero na changamoto nyingi sana kabla hata sisi Wabunge hazijatufikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI waje na majibu ya kutupa sisi Waheshimiwa Wabunge ili wenzetu kule wakituuliza, tuwe na majibu sahihi ya kuweza kuwaelezea kuhusiana na suala zima walau na wao pia kuweza kupatiwa hata posho za kufanya kazi katika kipindi ambacho wanafanya kazi wenyeviti wetu hawa kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hili linakuja moja kwa moja pamoja na Madiwani wetu ambao kwa kweli Wabunge tumekuwa tukizungumza hapa kwa muda mrefu. Madiwani hawa nao wamekuwa wakifanya kazi kubwa, tunasaidiana nao katika mambo mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kumekuwa na kakigugumizi katika kujua hizi posho zao ni lini basi Serikali inaweza kufanya jambo ili na wao basi waweze kutabasamu wakiwa wanatekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jambo hili naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, wakati mnahitimisha kama Mheshimiwa Waziri hatakuja na majibu sahihi, nitashika shilingi yake, nitaondokanayo. Aje na majibu sahihi na sisi tupate majibu sahihi ya kuwaeleza wenzetu huko ambako tunafanyanao kazi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie suala la hii mikopo ya 10%. Nakumbuka Bunge lililopita nilizungumza kuhusina na suala la mikopo ya 10% na tulishauri sana kuhusiana na jambo hili. Mikopo hii ilisimamishwa na ikarejeshwa tena. Hivyo, bado changamoto kwenye mikopo hii ni zaidi pengine ya zilizokuwepo huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko yamekuwa mengi, wananchi wanalalamika, hawaoni tija kwenye mikopo hii na hususan ni wale walengwa ambao wanatakiwa kupewa mikopo hii. Tayari inaonyesha kumekuwa na upendeleo mkubwa sana kwenye utoaji wa fedha hizi, na akina mama wengi ambao wanastahili kupata mikopo hii wamekuwa hawapokei mikopo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda kwenye kampeni. Tunajua ni kwa namna gani akina mama wengi wamejitokeza katika kampeni za Chama cha Mapinduzi kumuunga mkono Mheshimiwa Rais, mama yetu. Hata hivyo, tumekuwa tukiahidi kwamba tutakapofanikiwa, tutahakikisha na wao wananufaika na mikopo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali, lazima tuangalie upya nini ambacho tunaweza kuwasaidia akina mama wanaofanya biashara ndogo ndogo na hususan za kuuza mboga mboga za kuuza matunda. Hawa akina mama wanaonekana kwamba mitaji yao ni midogo, lakini ndiyo maana hawapewi mikopo hii, lakini hatuwatendei haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali ije na mpango mahususi ambao utawashirikisha wanawake hawa ambao wanauza mboga mboga na hususan wanawake wangu wa Jimbo la Tabora Mjini ili waweze kufanya biashara zao, na wao wakue sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa mama huyu ataendelea kuwa na mtaji wa shilingi 10,000/= kila siku, atakua lini? Naomba nitoe mfano mmoja na ninampongeza sana Waziri wa Vijana, ndugu yangu Mheshimiwa Nanauka, alifika katika Jimbo la Tabora Mjini. Alipofika, hakulala, alikwenda kutembea mtaani, alikutana na wanawake, mmoja ni kati ya mabinti ambaye alikuwa anafanya biashara ya kuchoma mahindi. Mheshimiwa Nanauka alimuuliza wewe dada leo unachoma mahindi, nini unachokifikiria baada ya wewe kuchoma haya mahindi huko mbele?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule binti alimwambia Mheshimiwa Nanauka, nina mpango mzuri, na akamweleza nini ambacho ataweza kukifanya? Mheshimiwa Nanauka alimpa shilingi 300,000/= ili aweze kufanya kile ambacho alikifikiria aondoke pale kwenye biashara ya kuchoma mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili kama sisi sote tukilifanya kwa ufanisi, tutawasaidia wanawake kama huyu binti, kwani wapo wengi kwenye maeneo yetu, na wanachohitaji ni kufikiwa na kuwezeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawezeshwaje? Lazima TAMISEMI kupitia Wizara ya TAMISEMI, kaka yangu Mheshimiwa Prof. Shemdoe na wenzake, ninawaamini sana, najua wana uwezo wa kufanya kazi vizuri sana, lakini bado kuna malalamiko mengi sana ya wanawake hawa na vijana ambao hawawezi kupata hizi fedha za 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukae tuone ni namna gani tunawasaidia hawa hawa wadogo wanaouza mboga mboga ndiyo wamekuwa *support* kubwa katika sisi wanawake ambao tunafanya siasa, hata ninyi wanaume huko kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusiana na suala zima la haya maboma. Maboma imekua ni kero, na haya mambo Bunge la Kumi na Moja, Bunge la Kumi na Mbili, Bunge la Kumi na Tatu tunazungumza suala la maboma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumza kuhusu suala la maboma. Naiomba Serikali na nitoe mfano mmoja tu hai, wakati tunafanya ziara, tumefika kwenye Mkoa mmoja wananchi wamejichangisha, tena ni jamii ya kifugaji, wamejichangisha fedha, wamejenga shule ya sekondari. Wameanzisha maboma yao na Serikali ikaona kwamba hawa wana nia thabiti ya kuhitaji shule, wamepeleka fedha, matokeo yake fedha zimekwenda kujenga shule nyingine pale pale penye maboma ya wale wananchi, halafu maboma yao wameyaacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linawaumiza wananchi wetu, wanaona kwamba kumbe hawahitajiki kufanya wanachotakiwa kufanya na ndiyo maana Serikali ikija, inakuja na mpango wake bila kujali nguvu ambayo wananchi hawa wameiwekeza huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sana Serikali, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ninafahamu utendaji wake, amekuwa Katibu wa TAMISEMI. Waende wakaangalie hawa wananchi waliojitolea nguvu zao. Hawa wananchi ni maskini, wanajichangisha fedha zao kidogo kidogo, na mwisho wa siku wanapata fedha, wanasaidia na wao watoto wao waweze kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho lakini siyo kwa uhumimu ni kuhusiana na suala zima la afya ya msingi. Hili ninaomba niwaambie watu wa TAMISEMI kwamba pamoja juhudi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Rais wetu, bado kuna changamoto kubwa sana kwenye afya ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya ya msingi ni zahanati pamoja na vituo vya afya. Huko ndiko wananchi wetu wanapoanza kupata huduma za afya. Kama kukidorora huko, huyu mtu mpaka

aje kufika hospitali ya rufaa ina maana hali yake imekuwa mbaya kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niishauri Serikali, lazima tuboreshe huduma katika zahanati zetu na vituo vya afya ili wananchi wetu waweze kupata huduma bora kuanzia kwenye maeneo yao badala ya kusubiri mpaka tufike hospitali za rufaa ndiyo tukutane na vifaatiba, ndiyo tukutane na dawa, haiwezekani. Kwenye wananchi ni huku chini kwenye zahanati na vituo vya afya. Ninaiomba Serikali yangu iweze kuboresha huduma kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, ninaomba sana nikushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Mwaifunga. Tunaendelea na Mheshimiwa *Eng.r* Mwanaisha Ng'azi Ulenge halafu atafuatia Mheshimiwa Sara Msafiri.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote, ninamshukuru Mungu, Muumba wa Ardhi na Nchi, ambaye ameniwezesha kusimama katika Bunge hili Tukufu, nami kuweza kuweka mchango wangu katika hotuba hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii pia kutoa pole kwa Wabunge wenzangu kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu, Mzee wetu Mheshimiwa Lukuvi. Pia, ninapeleka salamu za pole kwa wananchi wa Jimbo la Ismani. Hakika sisi sote ni wa Mungu na kwake tutarejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri iliyosheheni maono ya ufuatiliaji wa shughuli za kila siku za Serikali kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 52 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza wenzangu ambao wametangulia kulizungumzia suala la ufuatiliaji na tathmini, kama ambavyo leo Mheshimiwa Mbunge ameuliza swali kwa Waziri Mkuu. Tunapoizungumzia Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini, au tunapozungumzia suala zima la ufuatiliaji na tathmini, mimi ninaamini ile ndiyo *instrument*, ndiyo nyenzo muhimu ya kumhakikishia Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutekeleza majukumu yake ipasavyo ya kufuatilia shughuli za kila siku za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu Tukufu imeweka malengo mazuri ya kufikia Dira ya 2050 tukiwa Taifa lenye Uchumi wa Kati wa Juu na kuliongeza pato la mwananchi mmoja mmoja kufikia shilingi 7,000/=. Bila kuwa na nyenzo hii muhimu ya kufuatilia kwa umakini shughuli za kila siku na Serikali, suala zima la nchi yetu kufika kwenye Taifa la Uchumi wa Juu ni jambo ambalo litaishia kwenye makaratasi na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo na timu yake nzima iliyoandaa Dira ya 2050, bila kuweka mkakati madhubuti wa kuhakikisha tuliyoyaweka katika maandishi yanakwenda kutekelezwa ipasavyo na wananchi wanakwenda kunufaika na rasilimali ambazo Mungu ametubariki kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninazungumza hivi? Tangu awamu iliyopita, Bunge hili nikiwemo na mimi tulisimamia ajenda hii ya ufuatiliaji na tathmini. Bila kupepesa macho, tuipongeze Serikali. Tunaona hatua ambayo imechukua dhidi ya jambo hili kwa kuhakikisha vitengo vimeanzishwa kwenye kila ofisi ya Serikali, na tumeshuhudia pia kwamba mwongozo wa ufuatiliaji na tathmini umeanzishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la msingi la kujiuliza, kama ambavyo tumeshuhudia wengi, Waziri wetu Mkuu alipofanya kazi yake ya Kikatiba ya kufuatilia shughuli za kila siku za Serikali, alivyoshuka kule chini, tuliona namna ambavyo changamoto zinazotokana na watu walioaminiwa kutotekeleza majukumu yao ipasavyo, zimekuwa ni nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani sasa miongozo ile iliyoandaliwa na Ofisi hii ya Waziri Mkuu tuhakikishe inafika kule kwenye Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwa namna ninavyojaribu kulifuatilia jambo hili, miongozo ile haijafika chini. Miongozo ile haijakuwa *disseminated* katika *Local Government Authorities. This is the fact that should not be denied*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba kule ambako ndiko tabasamu la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anatamani lifikiwe kwa wananchi, miongozo ile ya ufuatiliaji na tathmini haijafika. Kwa hiyo, kile tunachokitamani kitokee kwa wananchi wapate tabasamu, bado halitawezekana kama miongozo ya ufuatiliaji na tathmini haijafika kule chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ma-*DED* miongozo hii haijafika. Nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anajibu swali lake, nimemsikiliza akizungumzia suala zima la mfumo wa kidigitali kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini. Mfumo ule unaokwenda kutengenezwa utakuwa jumuishi kiasi gani? Anayetoa kero ni mwingine, halafu anayeingia ndani ya mfumo ni mfanyakazi mwingine ambaye labda na yeye ndio mtekelezaji wa shughuli kule chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani mfumo unaokuja wa ufuatiliaji na tathmini uwe jumuishi ambao kweli mtoa kero na yeye atapata nafasi ya kuweka kero zake ili kutatua changamoto za wananchi mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka vizuri tangu awamu iliyopita, Serikali hii pendwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mara ya kwanza ilianzisha hivi vitengo vya ufuatiliaji na tathmini kwenye kila ofisi ya Serikali. Serikali hii hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tunaamini ilianza mchakato wa Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatamani kusikia Waziri Mkuu atakapokuja ku-*windup* hoja yake, atuambie sera hii imefikia wapi? Tunahitaji kuiona. Mama huyu wa matokeo makubwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan analitekeleza jambo hili

haraka iwezekanavyo kwa awamu yake hii ya pili, ili yale malengo yaliyowekwa kwenye Dira ya 2050 yaweze kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuiona sera inakuja hapa Bungeni ya ufuatiliaji na tathmini ili kero za wananchi kule chini ziweze kutatuliwa. Bila ufuatiliaji na tathmini, hatuwezi kuongeza *compliance* katika utekelezaji wa majukumu, hatuwezi kuzuia ubadhirifu, hatuwezi kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa haraka, na hatuwezi kuhakikisha programu za maendeleo zinafanyika kwa *speed* ya hali ya juu bila kuwa na Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini, ambayo hii ni *instrument* muhimu kwa huyu aliyepewa majukumu Kikatiba ya kufuatilia shughuli za kila siku za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu huyu, yaani kwa mujibu wa namna ambavyo anatekeleza majukumu yake, bila kutengeneza mfumo na sera na sheria madhubuti ya ufuatiliaji na tathmini, hataweza kutekeleza hili jukumu ipasavyo. Tunaomba sera ije mapema hapa Bungeni, tuipitishe na ili tuje na sheria baadaye kuweza kuhakikisha huyu Mheshimiwa Waziri Mkuu ana-*relax* katika kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika ninaunga mkono hoja, lakini tunaomba sana hayo yafike Bungeni katika awamu hii ya Mama wa matokeo makubwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge. Nilimtaja Mheshimiwa Sara Msafiri, Mheshimiwa Festo Sanga, Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati na Mheshimiwa Hamisi Taletale wajiandae.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuisimamia, na ninampongeza kwa ziara yake ambayo ameifanya ambayo Wabunge wenzangu wametoka kumpongeza kwa jinsi anavyosikiliza kero za wananchi na kuzipatia majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, sisi Wabunge tuko nyuma yake kwa sababu jambo hili linasaidia sana kupunguza uzembe kwa watendaji wetu kule kwenye halmashauri, lakini inatoa fursa ya viongozi na watendaji kujitathmini kwenye nafasi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii kutoa pole kwa wananchi wangu wa Jimbo la Mvomero kwa mafuriko makubwa ambayo yamelikumba Jimbo la Mvomero tangu tarehe 26 mwezi wa Pili. Hali inaendelea kuwa mbaya, kaya zinazidi kuongezeka kutoka kaya 78 mpaka sasa ni kaya 2,000 tumezihamisha kwenye mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali, wamekuwa wakitukimbilia kipindi chote hiki cha mafuriko. Tumepokea misaada mbalimbali kutoka Serikalini hasa ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumepata vyakula na tunapata huduma mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kipekee pamoja na kwamba bado changamoto za mafuriko zipo, lakini tunaona kabisa juhudi ya Serikali katika kusaidia zile huduma za kibinadamu za kwanza zile za dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya, lakini kwa kutembea kwenye maono yake na pale zinapotokea changamoto za kidunia anavyoweka mikakati ya kukabiliana nayo ndani ya nchi na kupitia mahusiano ya Kidiplomasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hotuba yake ya jana, ameweza kupunguza gharama za uendeshaji wa ofisi yake hasa kwenye masuala ya matumizi ya magari kutokana na changamoto za uhaba wa mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini taasisi zote za Umma na hata na sisi wananchi tutachukua hatua sasa za makusudi kuhakikisha tunapunguza maumivu haya ya gharama za maisha zinazotokana na changamoto za mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite kwenye Jimbo langu la Mvomero. Sisi kule ni wakulima na ni wafugaji. Kama nilivyoongea awali, tumekuwa na changamoto za mafuriko haya hasa kuanzia mwaka 2002, na kuna mto unaitwa Mto Mbulumi. Mto huu umeanzia Mkoa wa Arusha, Mkoa wa Manyara, unakuja na Mvomero, na mwisho maji haya ndiyo yanaenda kwenye vyanzo vya maji kule Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Jimbo la Mvomero tumekuwa chanzo kikubwa sana cha vyanzo vya maji kwenye mikoa hii ya Pwani na Morogoro ambapo na Dar es Salaam, ndiyo kuna viwanda na matumizi makubwa ya kiuchumi kule. Changamoto kubwa tunayoipata kwenye Mto huu Mbulumi hasa kipindi cha mafuriko, maji haya yanahama njia kwenye mto, na mwaka 2000 kaya 78 tu ndiyo ziliathiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi kubwa zimefanyika na Serikali, hasa ngazi ya wilaya na mkoa, tumetafuta maeneo mapya kwa kaya 78 zilizoathirika mwanzo, na tumekuwa na programu mbalimbali za kutunza vyanzo vya maji na kupanda miti, lakini athari imekuwa ikiongezeka, hadi sasa ni kaya 2,000 ambazo hazina makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalamu wa Bonde la Mto Ruvu walifanya tathmini, ili mto ule usihame, zinahitajika shilingi bilioni 4.7. Kwa heshima na taadhima kabisa tunaomba Serikali itusaidie tuweze kupata fedha hizi kwa ajili ya kudhibiti mto huu kuhama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu athari ya mafuriko haya ni kubwa sana. Ipo miundombinu mikubwa Serikali imewekeza kwenye Jimbo la Mvomero. Tuna skimu za umwagiliaji nane ndani ya Jimbo la Mvomero, na fedha nyingi za Serikali zimetumika kuweka miundombinu kwenye skimu hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi ya barabara, umeme, na miradi mingine yote inatekelezwa. Sasa, kwa sababu tumejielekeza kuhakikisha thamani ya fedha za miradi zinaonekana, na tunatunza miradi yetu, athari ile ya mafuriko haiishii tu hivyo, sasa hivi shughuli za mifugo, mashamba, na kilimo zinasimama, lakini hata ule uwekezaji wa fedha nyingi za Serikali kwenye miundombinu hii hata kwenye Skimu za Umwagiliaji, sasa inaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba Serikali kuwe na mpango wa pamoja wa taasisi zote, *TANESCO*, Maji, na miundombinu mingine yote waweze kukaa kuona kipande hiki cha kilometa mbili kinacholeta athari kubwa za mafuriko kiweze kujengewa kwa fedha hizo za shilingi bilioni 4.7 ili kukomesha mafuriko Jimbo la Mvomero, na kulinda mashamba, mali za wananchi, na uwekezaji wa miundombinu mingine kama nilivyoitaja, iweze kuendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo tutakuwa tunafanya kama walivyotoka kuongea Wabunge wenzangu, kwamba tunawekeza fedha nyingi kwenye miundombinu, lakini hatuwezi kuilinda miundombinu hii. Kwa hiyo, Serikali inarudi tena kutenga fedha kwa ajili ya kwenda kufanya miundombinu ile ile ambayo tulishaiwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro ndiyo mkoa wa vyanzo vikuu vya maji. Tunajivunia Bwawa la Mwalimu Nyerere, Bwawa la Kidunda, viwanda vilivyokuwa Dar es Salaam na Pwani, lakini nishati ya maji, watunzaji wakubwa ni Mkoa wa Marogoro. Kwa hiyo, tunapopata mafuriko tunataka kuona Serikali inatukimbilia kwenda kuimarisha miundombinu hii, na mimi sina wasiwasi kabisa na Serikali hii ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amefanya Mkoa wa Lindi leo hii mafuriko yamekuwa historia. Sasa, kama Bwawa lile la Mwalimu Nyerere tunalihitaji, Mradi wa Kidunda tunauhitaji, viwanda ambavyo vinaleta uchumi na mchango mkubwa wa pato la Taifa vilivyokuwa Dar es Salaam na Pwani tunavihitaji, basi twende

tukaimarishe mifumo ya miundombinu kwenye mito hii, hasa Mto Mbulumi ambao umekuwa ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka niseme, Jimbo la Mvomero lina tarafa nne. Tarafa hii ya Turiani ambayo ina mafuriko makubwa ndiyo tarafa yetu ya kimkakati ya uwekezaji. Ndiyo tarafa yenye viwanda, ndiyo tarafa ambayo Mheshimiwa Rais anaenda kutujengea mtambo wa kufua umeme wa *kilovolt* 220 kwa ajili ya kuongeza viwanda. Kwa hiyo, tunalihitaji eneo hili sasa liimarishwe kwenye mifumo ya miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sara Msafiri. Tunaendelea na Mheshimiwa Festo Sanga, Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Jambo la kwanza ninaipongeza Serikali na ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa ambayo inaonesha mwelekeo wa Serikali yetu pamoja na Wizara ambazo ziko chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hotuba ya Mheshimwa Waziri Mkuu, na ziara ambayo amekuwa akiifanya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kweli tunampongeza, kwa sababu, kama Watanzania, tunaona wazi kwamba kuna eneo kuna changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye nchi yetu inatafsiri kubwa sana kwa sisi ambao tunafuatilia. Tafsiri ya kwanza ni kwamba, huko chini kwenye halmashauri na maeneo mbalimbali kwenye Serikali yetu kuna ombwe la utumishi ndani ya Serikali. Kwa sababu, kuna matatizo madogo unayakuta kabisa, ambayo ni *level* ya watu wa chini kuyatatua, yanamsubiri Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tafsiri yake ni kwamba, watu wamegeuza kuajiriwa na Serikali kama ni *security*

tu, yaani ni kulinda ajira zao, lakini siyo kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni muhimu Serikali tuangalie kama wenzetu wamekuwa na *mentality* hiyo, watumishi wa umma wamekuwa na *mentality* kwamba, mimi nikiajiriwa na Serikali niko salama, sitafukuzwa, nitahamishwa kituo. Sisi, kama Serikali, tunakuja na mbinu gani? Tunakuja na tafsiri gani katika eneo hilo, ili kuondokana na hicho ambacho watu wamegeuza ni kichaka kwa sasa? Kwa sababu, kwa kweli, inatia aibu kuona Waziri Mkuu anaenda kutatua mambo ambayo yanatakiwa yatatuliwe na Mtendaji wa Kata au mambo ambayo yanatakiwa yatatuliwe na Mtendaji wa Kijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa Shemdoe, kaka yangu Sangu, ni watu ambao ninajua *brain* zenu ni kubwa. Angalieni ni namna gani tunaenda kutoa hicho kitanzi ambacho Watanzania na watumishi wa umma wamejificha kwamba, hawawezi kufukuzwa kwenye Serikali ndiyo maana mikwamo inakuwa ni mingi. Licha ya Serikali kukusanya fedha nyingi zinaenda kupotelea huko kwa sababu, usimamizi upo chini, usimamizi upo hovyo, watu wanawaza kupiga *deal* tu na kuanza kupiga *issue* nyingine za kutengeneza fedha, lakini siyo kutatua matatizo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara ya Waziri Mkuu ni lazima itupe taswira na mwenendo mpya wa jinsi gani tunaenda kuendesha nchi yetu. Ndiyo maana waliosisitiza wote kitengo cha *monitoring and evaluation* ni muhimu sana, kama hatutakuwa na *monitoring and evaluation,* Waziri Mkuu atapita, ataondoka, matatizo yatabaki palepale. Kwa hiyo, ni muhimu *monitoring and evaluation* kila Waziri yale ambayo Waziri Mkuu amepita ameyaangalia au kwenye utekelezaji wa bajeti yamejitokeza au kwenye ziara yamejitokeza, ni vyema tukapata majibu kwamba, nini kimeendelea kwenye matatizo hayo, ili tuweze kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo pia, lipo hata hapa kwenye Bunge letu kwa sababu, Wizara hii inahusika kwenye mambo ya Sera na Uratibu wa Bunge. Sisi, kama Wabunge, hapa ndani

tunauliza maswali, unaweza ukauliza maswali mara 18, mara 20, hayapati majibu; tafsiri yake ni *monitoring and evaluation* hata ndani ya Bunge haipo. Kwa hiyo, ni lazima sisi kama Wabunge tuangalie je, *thinking* yetu imeishia hapo? Tukiuliza maswali tusijibiwe kwa mara 16?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ester kasimama asubuhi, kauli, ameuliza mara 16 swali lake kuhusu stendi, hadi leo halijapata majibu. Tafsiri yake ni kuna eneo lazima twende mbele zaidi kwenye kutatua matatizo ya Wabunge kwa sababu, kama mimi nimeuliza maswali mara 16 Bungeni kuhusu Barabara ya kwenda Mbeya haijapata majibu, tafsiri yake ni wananchi wa Makete wote hawajapewa majibu na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Serikali ijue namna ya kwenda mbele au Bunge tutafute namna ya kwenda mbele. Kila Waziri hapa ni lazima awajibike kutokana na maswali anayoyajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mawaziri hapa watakujibu leo kwamba, mkandarasi anatafutwa, kesho kutwa atakwambia mkandarasi kafika *site*, likija Bunge lingine atarudi palepale atasema mkandarasi anatafutwa, yaani ni nenda rudi, nenda rudi. Ni lazima pia, hata sisi, kama Bunge, tuwe na uwezo wa kufanya tathmini ya maswali ya Wabunge hapa ndani kinaendelea nini? Kinafanyika nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ndivyo tutatatua matatizo kwenye nchi yetu, tofauti na hapo wakisema hili Bunge ni la 14 sijui, la 13, siyo Bunge la 12!  Watakuwa wanawaumiza wananchi, hatumuumizi Mbunge kwa sababu, mimi ninawakilisha wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vyema pia, Wizara ya Bunge, Sera na Uratibu waangalie ni namna gani Wabunge matatizo na maswali yao yanapatiwa ufumbuzi kwa sababu, yamekuwa yakiulizwa mara nyingi na hayapewi majibu. Waziri anaona kuja kujibu tu na kuondoka amemaliza kesi, anaendelea na shughuli zake, amemaliza. Tunataka tutatue changamoto za

Watanzania, tunatatuaje changamoto za Watanzania kama majibu halisi hayaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima *brain* yetu tuifungue, kama hatujaifungua *brain* Bunge letu litaendelea kuwa na ukomo wa kwamba, Bunge letu limeishia hapa, kuuliza maswali, hayajajibiwi, basi. *No* hili Bunge lazima liwe na meno, liwe na uwezo wa kuleta na kutatua hoja za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ni mchango wangu kwenye eneo hilo la *monitoring and evaluation*. Serikali isiyokuwa na *monitoring and evaluation* ni Serikali ambayo haitarajii kuwa na matokeo chanya, ni Serikali ambayo haitarajii kuwa na matunda kwa Watanzania kwa hiyo, ni vyema tukaimarisha kitengo hicho. Mheshimiwa Rais anatoa matamko kila siku, Waziri Mkuu anatoa matamko kila siku na Mawaziri wanatoa matamko kila siku, je, ni nini kinaendelea baada ya hayo matamko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiishie tu kutoa matamko, lakini tuishie kwenye kuhakikisha kwamba, utendaji unafanikiwa na hayo mambo yanafanyika kwa sababu, ukienda huko watasema aah! Yule ni mwanasiasa tu ameongea. Lazima tuondoke kwenye hilo eneo twende kwenye kutatua changamoto kwa hiyo, sasa Mheshimiwa Shemdoe lazima tulifanyie kazi hilo eneo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye eneo la wananchi wa Makete. Sasa niweze kujadili wananchi wa Makete kuhusu barabara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo, Mheshimiwa Waziri amesimama.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa tu ndogo.

**MWENYEKITI:** Profesa Kitila Mkumbo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa tu ndogo kwa mchango mzuri sana wa mwanafunzi wangu, kwamba, kuhusu suala la *monitoring and evaluation*, ninataka nimhakikishie kwamba, Serikali inao mfumo kamili wa Ufuatiliaji na Upimaji wa Utendaji wa Serikali na ipo katika Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini pia, ipo kwenye kila Wizara na Idara za Serikali, ipo ndani ya Tume ya Taifa ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kuboresha, lakini siyo sahihi kuweka hoja ama kupeleka taswira kwamba, Serikali haina kabisa mfumo wa upimaji, ufuatiliaji na la mwisho kwa mfumo wa Bunge, ambavyo unafanya kazi. Maswali ambayo Wabunge wanauliza ndani ya Bunge hili na katika Kamati zake, Serikali lazima itoe mrejesho ndani ya Kamati na katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa Taarifa.

**MWENYEKITI:** Naamini Mheshimiwa Festo umepokea Taarifa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na-*declare interest*, ni Mwalimu wangu wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam kwenye *Political Science,* kwa hiyo, ninamheshimu. Ninatambua alichokisema na ninapokea hoja yake, lakini ninachokisisitiza ni usimamizi. Ninaweza nikawa na sheria, lakini usimamizi wake haupo katika umakini. Kwa hiyo, ninachokitafsiri, ninachokiomba hicho Mheshimiwa Profesa Kitila katika michango yake, ambayo anachangia mingi inaonesha kwamba, kuna udhaifu wa usimamizi. Moja kati ya mchango aliochangia juzi alikuwa anaonesha kwamba, ndani ya Serikali kuna vitaasisi vingi sana… *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** …ambavyo vinakwamisha mambo kwenda. Ninataka nimsisitize kwenye hili kwamba, Sheria tunayo ya *Monitoring and Evaluation* chini ya Serikali za Mitaa kwa ma-*RAS,* lakini usimamizi wake haujawa na meno makali kuhakikisha kwamba, hayo madhaifu ambayo Waziri Mkuu amekutana nayo.

**MHE. MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Festo Sanga. Muda wako umekwisha.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aaah!

**MWENYEKITI:** Ile Taarifa haingii kwenye hesabu ya muda wako.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja tu, dakika moja. Namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa ajili ya eneo la Makete, Eneo la *TARURA,* barabara, tunamwomba sana atuongezee fedha, ili barabara yetu iweze kujengwa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Festo Sanga. Nilimtaja Mheshimiwa Ritta Kabati. Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale atamalizia.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Ninaomba kumtanguliza Mwenyezi Mungu katika mchango wangu, lakini vilevile ninawashukuru Wabunge wote waliotukimbilia katika msiba wa Mheshimiwa Lukuvi, Mbunge wa Jimbo la Isimani. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge hili, kama Mbunge wa Jimbo la Kilolo, ninaomba kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu na pia, ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kilolo kwa kumpa kura nyingi sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan lakini pia, kunichagua na mimi kuwa Mbunge wa Jimbo la Kilolo. Kwa mara ya kwanza mwanamke ninakuwa Mbunge wa jimbo na mimi nimeandika historia. Ninawashukuru pia, kwa kuwachagua Madiwani wote wa Chama Cha Mapinduzi, kwa hiyo, ninaomba wananchi wote wa Kilolo wawe na imani na mimi, sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri wetu Mkuu kwa kuwasilisha bajeti yake hapa Bungeni, lakini pia, ninampongeza kwa kazi nzuri. Toka amekuwa Waziri Mkuu amekuwa akienda katika mikoa yote na ninamkaribisha pia, hata katika Mkoa wetu wa Iringa, hususani katika Wilaya ya Kilolo, tunamsubiri na tunamkaribisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana pia Waziri wetu wa TAMISEMI, Profesa Shemdoe. Kwa kweli, tuna imani naye sana kwa sababu, hiyo Wizara ameiishi kwa hiyo, tuna imani atatusaidia sana pamoja na watendaji na Mawaziri wake wote wa Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe pongezi nyingi sana kwa Mkuu wetu wa Mkoa, Kheri James. Tumepata Mkuu wa Mkoa mtendaji, ni Mkuu wa Mkoa ambaye, sisi kama hatupo yeye anakwenda jimbo kwa jimbo; ametokea Kilolo na kulikuwa kuna upungufu pale katika zahanati, tayari ninaona TAMISEMI wamepeleka. Kwa hiyo, tuna bahati, Kheri James afanye kazi, Iringa tunaringa tupo na yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba vilevile kwa sababu, ninaanza kuchangia *TARURA*, ninampongeza sana Mtendaji Mkuu wa *TARURA, Engineer* Seff. Ni *Engineer* anayefanya kazi vizuri mwanzo mwisho, tunamfahamu, tunaomba aendelee

kushughulikia barabara zetu zote za nchi hii ikiwepo Kilolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimshukuru sana Meneja wa *TARURA* katika Mkoa wangu wa Iringa na pia, *TARURA* Wilaya ya Kilolo, *Engineer* Kidola. Ninawashukuru *TARURA* kwa sababu, wamekuwa wakishirikiana nami, barabara zote mtandao umeharibika Kilolo kwa hiyo, ninawashukuru. Muda wote ninawapigia simu na hawalali nyumbani kwao, kila siku wanalala kwenye *site* kwa sababu, barabara hazipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa kabisa katika Wilaya ya Kilolo ni, kwanza tumepata baraka ya mvua kwa hiyo, barabara nyingi hazipitiki. Kata zote, hata kutaja hapa sitaweza kwa sababu, nitatumia muda wote kuzitaja barabara za Kilolo, mtandao mzima wa barabara unakatika kwa sababu, mvua ni nyingi, zinahitaji madaraja ya kutosha, zinahitaji makalavati ya kutosha. Kwa hiyo, kwa kweli, wananchi wa Iringa, wa Kilolo, wanapata shida sana, wanapata mateso kwa sababu, sehemu nyingi ambazo barabara hazipitiki hakuna vituo vya afya, sehemu nyingi ambako barabara hazipitiki hakuna zahanati. Kwa hiyo, wananchi wanateseka kwenda kupata huduma za afya katika Hospitali ya Wilaya ya Kilolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pembejeo hazifiki kwa wakati kutokana na hizo barabara, vilevile magari hayapiti. Hapa ninapoongea kuna Barabara inayotoka Ilula kwenda mpaka Image, magari leo yamekwama, nyanya zinaoza pale, mazao hayafiki sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilolo ina mtandao wa barabara takribani kilometa 1,200, lakini ukiangalia kwa sababu hii, ni wilaya nzima jimbo moja. Ukiangalia Iringa *DC* pia, wao mtandao wao ni sawa na Kilolo, sasa wenzetu kwa sababu, wana majimbo matatu wanapata *1.5 billion.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine bajeti ina tozo ya mafuta, Kilolo bado tunapata shilingi milioni 500. Ninawaomba kwa sababu, wenzetu wote wana majimbo matatu, lakini Kilolo ina jimbo moja, halmashauri moja kwa hiyo, kwenye wakati wa

mgao unaona Kilolo tunapata shilingi milioni 500 tu, lakini mitandao ipo sawa na wilaya nyingine. Ninaomba wasiangalie jimbo, waangalie changamoto wanazopata wananchi, waangalieni mtandao wa barabara, wanagawaje hizi pesa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakiangalia jimbo tutaendelea kuteseka, wananchi wa Kilolo wataendelea kuteseka. Ninaomba iongezwe bajeti katika Wilaya ya Kilolo kwa sababu, Kilolo asilimia kubwa iko kwenye ukanda wa milimani. Pia, ninaomba kujua ni lini sasa utekelezaji wa Miradi ya *CRW, bottle neck* ile ya *World Bank*, itaanza kwa sababu, wataalam wamepita Kilolo, wamekagua na sasa hivi tayari mvua zimeanza. Kama wasipotoa kwa wakati maana yake ni barabara zile hazitatengenezeka na gharama zitakuwa juu. Kwa hiyo, maadam wataalam wamefika ninaomba wapite, walete pesa, barabara zitengenezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka kuzungumzia ni kuhusiana na elimu. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumepewa shule katika ujenzi wa shule za masomo ya sayansi kwa watoto wa kike Wilaya ya Kilolo tumejengewa shule na kwa kweli, ninafikiri wamenichagua mimi baada ya kuona ile shule imejengwa pale Kilolo. Kwa hiyo, ninaomba wajengewe uzio, watoto wetu wakae sehemu salama. Vilevile kuna changamoto kubwa sana katika Wilaya yetu ya Kilolo, tuna upungufu mkubwa sana wa walimu kwenye shule za sekondari, tunahitaji walimu zaidi ya 37 kwenye Masomo ya Sayansi na Hesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kwamba, bado majengo mengi sana, hasa maboma ambayo wenzangu wameyasema, tuna maboma mengi sana Kilolo, hayajajengwa. Ninaomba tuangaliwe upya kwa sababu, tuna upungufu mkubwa wa nyumba za walimu, uhaba wa maabara na majengo ya utawala, kwa hiyo, tunaomba Serikali iangalie haya majengo yaweze kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuna tatizo kubwa ambalo lipo katika usaili wa walimu. Walimu wetu wamekuwa wakijitolea kwa muda mrefu, miaka miwili, miaka mitatu, kuna

walimu wamejitolea Kilolo mpaka miaka sita. Unapokuja usaili hawa walimu wanaofanya vizuri, ambao wamekuwa wakisaidia watoto wanafaulu, hawachukuliwi, ni kwa nini? Lazima tuangalie, Sekretarieti ya Ajira ijiangalie upya tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, kuna wakaguzi wa elimu wanakwenda kule kuangalia hawa walimu wanafanya vizuri, wamefaulu vizuri, kila kitu wanacho, kwa nini hawachukuliwi? Kwa nini sasa wasipendekezwe waanze kuchukuliwa wale waliojitolea? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

**MWENYEKITI:** Tunamalizia na Mheshimiwa Hamisi Taletale.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. Mengine nitaleta kwa maandishi. *(Makofi)*

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu, Hadha wa Jallah, kwa kunipa uzima na mimi kuwepo hapa leo, lakini nina hoja zangu tatu tu kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza yule ndugu yangu, Mheshimiwa Mbunge Simai. Alikuja akasema kwamba, Bunge lingekuja na bendi, lakini mimi nikiwa kama meneja wa hiyo bendi nitamchagua Mheshimiwa Musukuma kwa sababu, yeye atafanya zile ngoma zao za mugobogobo, za Kisukuma, kama babu yangu atasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, turudi kwenye hoja. Sisi Wabunge wa vijijini tuna changamoto sana. Ndugu yangu na kaka yangu, Mheshimiwa Shemdoe, sisi tunamshukuru Mwenyezi Mungu

kwamba, kwenye mkoa wetu tuna mkuu wa mkoa na chenchi inabaki. Popote alipo kaka yangu Malima, tunampongeza sana, lakini ni suala la aibu kila siku mtu akisimama hapa barabara, barabara, mpaka mtu anajiuliza huyu kwake hakuna jambo lingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaletaje mambo mengine wakati miundombinu mibovu? Leo hii mimi hapa nikitaka kwenda Kidugalo, Barabara ya Kidugalo – Visalanga haipitiki, hakuna barabara. Yote ipo kwenye miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niongee kitu kimoja kwa nini nimemsifia Mheshimiwa Malima; ametuletea utaratibu wa kukuza bidhaa ya *spice* kwenye Mkoa wa Morogoro, leo hii sisi Morogoro tunakwenda kuipiga Zanzibar kwa kuuza *spice*. Hilo jambo sijui ametokanalo wapi Mzaramo wa watu yule, sijui kabila gani yule, Ndugu yangu Malima, ametuletea Morogoro. Leo hii sisi tumepanda kwa 80%, Zanzibar ambao ndiyo wakongwe tukizungumza tunasema marashi ya karafuu, lakini karafuu ya ukweli iko Morogoro vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hatuna miundombinu, kama hatuna barabara hata za ndani; juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumza vitu vingi hapa. Sasa tunashindwa kuelewa kinachotufanya tushindwe kusimamia vizuri suala la miundombinu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya kutoka Kibuko haipitiki. Waziri wa TAMISEMI yupo hapa, kaka yangu Mheshimiwa Shemdoe, labda niongee Kisambaa, "*nzeze*"! Shida ni nini kaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Kiroka haipitiki, njia ya kwenda Kinole, barabara ni mbovu. Daraja lile la Gwata – Ujembe limevunjika kwa sababu ya mvua, halafu watu wako wa TAMISEMI begi hawana, hela hawana, tuje hapa tuseme wewe utuambie, jamani eeeh, vitu haviendi huko kwa sababu, pesa ni ndogo. Hili ni Bunge, tunalia kwa sababu ya wananchi, tukiweza kuleta mabadiliko aje aseme pesa haitoshi, sisi tutamwongezea. Ana Rais msikivu, Rais mbeba maono, hawezi kukubali kuona

wananchi wa vijijini wanashindwa kutembea kwa sababu miundombinu siyo mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye miundombinu, ambayo ukizungumza sana ni lazima utazungumzia Barabara kubwa ya Bigwa – Kisaki; leo hii nikisimama hapa sijasema Bigwa – Kisaki, nikilala ninaumwa. Niponyesheni huu ugonjwa, ni aibu ya Taifa kuona mtu kila siku anasimama anazungumzia jambo moja ambalo uwezekano wa kutatuliwa upo, shida ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wameshindwa kusema, tunakuja hapa, Bunge linaloanza hili nitaondoka na shilingi na haniambii kitu mtu kwa sababu ya maslahi ya Morogoro Kusini Mashariki. Hatuwezi kuja kusimama miaka mitano imepita, nimekuja hapa ninaimba Bigwa – Kisaki, Bigwa – Kisaki. Leo hii ninakuimbia barabara za ndani miundombinu yetu mibovu, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa ametuletea wawekezaji wadau kwa sababu ya *spices,* hawawezi kuja wanateleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wa bodaboda wanashindwa hata kufanya kazi, kwetu udongo wetu ni utelezi. Basi wameshindwa kutuwekea lami kwenye barabara za *TARURA* tuwekeeni hata moramu tuweze kutembea vizuri, hakuna! Shida nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba kaka yangu Mheshimiwa Shemdoe akija, kama pesa aliyoomba ni ndogo aombe tumwongezee. Bunge lipo, kwa ajili yako, tutakupambania, yaani kitendo hicho kinachoendelea tunamwangusha Mheshimiwa Rais wetu. Mheshimiwa Rais, amesema anataka kufungua milango, milango ni kufungua miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudi kwenye suala la afya. Nilisimama hapa mwaka 2023 nikazungumzia Kituo cha Afya cha Kata ya Ngerengere, ni aibu. Kata ya Ngerengere Kituo cha Afya hakina jengo la mama na mtoto, ni kituo cha afya kikongwe sijui hata niseme nini nikaeleweka! Kaka yangu Mheshimiwa Shemdoe ametuletea pesa, kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Kinole, kwa ajili

ya Kituo cha Afya cha Mkulazi, namwomba baada ya Bunge hili au katikati ya Jumamosi twende jimboni kwetu akaangalie vile alivyovileta vilipoishia na aweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni tuna kituo cha afya chenye hali duni kwenye Kata yetu ya Kiroka, hakina sifa ya kituo cha afya kwa sababu, jengo la mama na mtoto hakuna, hakuna chochote. Namwomba ndugu yangu Mheshimiwa Shemdoe twende Jimboni Kusini Mashariki akaone, wanasema uhondo wa ngoma uingie ucheze, hakuna Mbunge hapa atakayesimama kumsifia leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kama mziwanda wa muda huu. Ninafunga hili Bunge kwa kusema kwamba, kaka yangu Mheshimiwa Shemdoe anatutosha na chenchi inabaki. Ana kitu ndani yake, atafika mbali, kama akiweza kusimamia maslahi ya Morogoro Kusini Mashariki. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamisi Taletale.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa mchana huu umefikia mwisho. Ninawashukuru kwa michango yenu na kazi yote tokea asubuhi kwa hivyo, ninawatakia mchana mwema na ninasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 Jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano ya hoja iliyo mbele yetu na nimuite sasa mchangiaji wa kwanza Mheshimiwa Muhsin Haji Ussi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas na Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma, ajiandae.

**MHE. MUHSIN HAJI USSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza kujadili bajeti katika eneo ambalo limegusa Serikali kwa upande wa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nichukue fursa hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye ametujalia kuweza kuwa na afya njema na leo hii tupo katika katika Bunge hili Tukufu kujadili mambo ya msingi yanayohusu mustakabali wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Malindi kwa kunipa heshima kijana wao kuweza kuwa Mbunge na kuwa sauti ya kuwasemea wananchi wa Jimbo la Malindi, nami ni ahadi yangu ya kwamba, daima nitakuwa sauti ya kuwasemea ndani ya chombo hiki muhimu kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na Wabunge wenzangu kumpongeza sana Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Rais ameonesha uongozi wa vitendo, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha kwamba yeye ndiye mzalendo nambari moja kwenye Taifa letu. Kwa hili hatuna shaka kipindi hiki cha miaka

mitano Taifa letu litaendelea kuweza kuvuna neema juu ya maono makubwa ya Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ninaomba binafsi nimpongeze wakati anazungumza jana kwenye hotuba yake, Mheshimiwa Rais anatambua dunia imekumbwa na changamoto ya uhaba wa mafuta kutokana na vita vinavyoendelea duniani. Yeye binafsi ameonesha moyo wa kizalendo, ameonesha ya kwamba kipaumbele ni kuhakikisha Watanzania wanapunguziwa gharama za maisha na kuongeza kwa mfano alitoa kauli ya kupunguza magari katika msafara wake ili kuhakikisha kuna anapunguza matumizi makubwa ya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ninaomba liwe funzo kwa viongozi wengine Serikalini. Waheshimiwa Mawaziri, Rais wetu ameonesha mfano, Wakuu wa Mikoa na watendaji wengine wote Serikalini tuungane na Rais wetu kuhakikisha ya kwamba tunapunguza mlolongo mrefu wa misafara ili kutumia kiwango kidogo cha fedha katika kipindi hiki ambacho Taifa na dunia kwa ujumla linapitia katika ukosefu wa mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na wenzangu kumpongeza Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, amekuwa Waziri Mkuu ambaye anafahamu changamoto za Watanzania, Wabunge amekuwa ni rafiki yetu, amekuwa ni mwenzetu, amekuwa akisikiliza changamoto za Wabunge. Hapa niseme ya kwamba kweli Mheshimiwa Rais hakufanya makosa alipoleta jina lake ili Bunge hili liridhie na kumpitisha kuongoza akiwa Msimamizi Mkuu wa shughuli za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nijikite mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeona Wabunge wengi waliosimama hapa, akinamama, akinababa na vijana wamezungumzia fursa za vijana kwenye Taifa letu, wamezungumzia namna gani vijana wa Taifa hili wanapaswa kupewa kipaumbele ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisoma kwenye utulivu hotuba ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 48, Waziri Mkuu anakiri na kutambua ya kwamba vijana ni nguvu kazi muhimu ya kujenga uchumi wa Taifa letu. Ninaamini kabisa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake ina dhamira njema ya kuhakikisha inawasaidia na kuwashika mkono vijana wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko mengi ya upatikanaji wa mikopo kwa vijana, akinamama na yale makundi yenye mahitaji maalum. Leo nilikuwa ninapitia Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, nikagundua Sura ya 290, Kifungu 37E ndicho kilichoanzisha wajibu wa Halmashauri ndani ya Taifa letu kutenga 10% kwa ajili ya kuhakikisha mapato yanayopatikana zile 10% zinakwenda kugusa wananchi moja kwa moja. Asilimia nne kwa vijana, asilimia nne kwa akinamama na asilimia mbili kwa wale wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu hiki 37E kimeweka msingi wa kisheria na kuipa mamlaka Halmashauri kutenga fedha hizo, lakini vilevile sheria inampa nguvu Waziri kuwa yeye ana mamlaka ya moja kwa moja juu ya kusimamia upatikanaji wa fedha na urudishaji wa fedha katika Halmashauri hizi. Ninaomba kunukuu: "Kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa itatenga sehemu ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Waziri mwenye dhamana (Waziri wa TAMISEMI) ataweka kanuni zinazoelekeza namna ya usimamizi utoaji na urejeshaji wa mikopo hiyo".

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nipeleke kilio changu kwa Profesa Shemdoe juu ya ukiritimba ambao unaendelea huko chini kwenye Halmashauri zetu. Ninafahamu Serikali ina dhamira njema, ninafahamu Wizara ina dhamira njema, lakini bado tuna changamoto huko chini kwenye Halmashauri zetu, tuna changamoto huko chini kwenye Kata. Maafisa wa Maendeleo wamekuwa ni kikwazo kikubwa sana kwa vijana wetu, akinamama na wale wenye uhitaji maalum kupatiwa fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema hivyo? Ukienda katika ofisi hizi za Halmashauri utawakuta Maafisa wamekaa ofisini kwenye viti vyao, wamekuwa *Desk Officers.* Wao wanalalamika ya kwamba vijana hawaji kuulizia juu ya namna gani wanaweza kupata fursa hii ya mikopo. Ninataka nijiulize, ikiwa wewe umeajiriwa kusimamia kazi ambayo uliiomba mwenyewe, unasubirije kijana atoke, aje akuulize badala ya wewe kutoka na kwenda kuwafuata vijana hao na kuwapatia elimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, mdogo, wako baadhi ya Maafisa wetu wa Maendeleo wanafanya kazi nzuri na hawa lazima tuwatambue. Ukienda kwa mfano, Kagera kuna Mwenyekiti wetu wa vijana kule alianzisha operesheni moja inaitwa Daka Fursa za Samia, alikuwa anazunguka kila Halmashauri kuona namna gani vijana wamepata hiyo mikopo ya vijana. Kwa hiyo, unakuta wako baadhi ya Maafisa wetu wameamua kutengeneza kliniki maalum, *mobile clinic* kuzunguka kwenye Kata, kuzunguka kwenye vijiji na vitongoji kuweza kuwapatia taaluma hii vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninaomba nitoe wito kwa Maafisa wa Maendeleo nchi nzima kwenye ngazi ya halmashauri, kwenye ngazi ya Kata, kuiga mfano huu mzuri ambao utakuwa ni chachu ya kuhakikisha vijana wanafikiwa. Ninatoa ushauri wanaposhuka huko chini waweze kuongozana na taasisi za kifedha benki zetu hizi *CRDB, NMB* ili vijana hawa waweze kupata elimu ya kutosha juu ya upatikanaji wa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii wakati tunapata uhuru mwaka 1961, tulikuwa tuna barabara chache sana, leo ukimsimamisha kijana ambao tunawaita vijana wa *Gen Z* ukimwambia kutoka Mwanza hadi Dar es Salaam ulikuwa unatumia wiki moja, hawezi kukuamini, kwa sababu Serikali imejenga miundombinu unatoka Mwanza – Dar es Salaam ndani ya siku moja umefika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijana mkulima wa kule Mwanza, mkulima wa kule Mara, mchimba dhahabu kule Geita akipewa fursa ya kupata mikopo hii wakikuza mazao yao watalima,

watavuna, ataweza kusafirisha kupeleka hadi kwenye soko kwa uharaka na wataweza kurudisha mikopo hiyo. Kwa hiyo, ndugu zangu Wabunge chombo hiki niwaombe sana kiwe ni chombo chenye meno kuweza kuhakikisha tunaacha historia, Bunge hili la Kumi na Tatu liache alama kuwafuta machozi vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na tabia ya kuwalalamikia vijana *Gen Z,* ninaomba nimalizie mwisho kabisa, vijana wa *Gen Z* huwa tunaambiana ya kwamba ni vijana ambao wana mihemko, mimi ninakataa vijana hawa wamezaliwa katika dunia yenye teknolojia, wamezaliwa kwenye dunia ya utandawazi wana uwezo wa kupata taarifa na *information* zote na ndiyo maana wanapoona kuna ukiritimba, wanapoona ya kwamba hawapatiwi zile fursa ambazo wanazijua namna gani ya kuzipata ndipo wanapoonekana ni wakorofi. Kwa hiyo, ninaunga mkono hoja hii, lakini niendelee, vilevile kwa msisitizo kuiomba Serikali na hasa TAMISEMI kusimamia kule chini kwa Maafisa wetu wa Maendeleo washuke kuwapatia elimu vijana wetu wapatiwe fedha ambazo Dkt. Samia amezitenga kwa Vijana wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga na Mheshimiwa Athumin Omary Mapalilo, wajiandae.

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, vilevile TAMISEMI. Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uzima, vilevile ninawashukuru Wapigakura wangu wa Jimbo la Mbulu Vijijini ambao ninaendelea kuwawakilisha, nami niwahakikishie kwamba wanaye mwakilishi ambaye halali na atawatendea haki ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutetea haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais, wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuwaletea tabasamu Watanzania kupitia miradi ya maendeleo, bila kumsahau Makamu wetu wa Rais, Dkt. Emmanuel Nchimbi na Waziri wetu Mkuu ambaye pia ni msimamizi wa shughuli za Serikali hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru kipekee Waziri Mkuu kwamba alitutembelea katika Wilaya yetu ya Mbulu na ndani ya Jimbo la Mbulu Vijijini, nina hakika alitutendea haki na wananchi walimpokea kwa furaha sana na ninapenda kuwasilisha shukrani za dhati kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hiyo Waziri Mkuu amejionea mambo mengi, moja ikiwa ni kusikiliza kero za wananchi, somo moja kubwa ambalo tunalipata ni kwamba tunaona iko changamoto katika Serikali zetu za Mitaa kwa maana ya watendaji kule chini. Ziko kero nyingi sana ambazo zingeweza kutatuliwa na watendaji wa vijiji, ziko kero nyingi sana ambazo zingeweza kutatuliwa na Watendaji wa Kata vilevile na Maafisa Tarafa, lakini zinakuja kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kipekee ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu achukue hatua ya kuweza kufanyia *reforms* kule chini ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaweza kuwasilisha kero zao katika Ofisi za Serikali na wanaweza kusikilizwa na kuweza kupewa majibu ya hakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya watendaji wachache kule katika vijiji vyetu na katika kata zetu hakika wamegeuka kuwa Miungu watu na hao ndiyo ambao wanaichafua Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi. Ninaomba TAMISEMI iweze kuchukua hatua za maksudi kuwajengea uwezo pia kuwaangalia kwa jicho kali hasa ili kuweza kuwatambua wachache wale ambao wanaichafua Serikali na hawawatendei haki wananchi wetu ili tuweze kuwaletea maendeleo wananchi wetu na kuwasikiliza wanapokuwa na kero katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba tunayo kero ya mafuta katika nchi yetu, nami ninaomba kwa kuwa Waziri Mkuu leo tunaijadili bajeti yake, nimeona Rais ametoa mfano jana wa pekee kwamba yeye anaanza na Ofisi yake. Ningependa kushauri Ofisi ya Waziri Mkuu iweze kuelekeza kufanya mapitio ya gharama za uendeshaji wa Serikali ili kupunguza gharama zisizo za lazima kwa kupitia mamlaka zetu za Mikoa, lakini na Wizara mpaka katika Serikali za Mitaa ili kuokoa gharama ambazo zitapotea kutokana na gharama za mafuta kupanda. Hii itatoa mfano wa kwamba Serikali inawajibika kwa wananchi wake ambao wameipa kura tarehe 29 mwezi Oktoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zetu katika maeneo ya vijijini hakika ndiyo moyo wa maendeleo na hasa katika usafiri wa wananchi kusafirisha bidhaa zao kutoka mashambani, lakini na shughuli za jamii. *TARURA* inafanya kazi nzuri sana na ninaomba nitambue mchango nzuri wa Mtendaji Mkuu, lakini pia na Meneja wangu wa Wilaya wa *TARURA* kwa kazi nzuri anayoifanya, japo wanakuwa na changamoto kubwa sana ya upungufu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba *TARURA* iongezewe bajeti, vilevile tumesikia kilio cha Wabunge walio wengi kutokana na baraka ya mvua, barabara nyingi na madaraja mengi yameharibika na wananchi wameshindwa kusafiri. Ninaomba *TARURA* iwe na kifungu cha dharura hasa kwa sababu tukijua masika siyo dharura, masika tunaitegemea kila mwaka itakuja, tunaomba *TARURA* iwe na kifungu cha dharura cha kuweza kusaidia barabara pale ambao inaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Mbulu Vijijini kwa mfano, iko Barabara Bashay- Yaedachini, Eshkesh kwenda Haydom, ni zaidi ya miezi mitano wananchi wale hawawezi kupita kwenda kwenye shughuli zao, kwenda kwenye matibabu na mvua inaponyesha hata watoto wa shule hawawezi kwenda shuleni. Ninaomba TAMISEMI iweze kufanya uharaka na namna ya pekee kuipa *TARURA* fedha ili marekebisho yafanyike kwenye barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo Barabara ya Bashay-Endamilay kwenda Haydom, Barabara ya Labay kwenda Maretadu pamoja na daraja lake, hizi hakika ni barabara muhimu sana ambazo zinasimamiwa na *TARURA* kwa uchache ambazo hakika zikirekebishwa shughuli nyingi za wananchi zitakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la afya, ninapenda kushukuru sana Serikali imefanya kazi kubwa sana, imetujengea vituo vya afya katika kata mbalimbal. Ninashukuru vilevile kwa ujenzi wa hospitali ya Halmashauri yetu ambayo hakika imefikia hatua ya mwisho, lakini bado tuna uhitaji wa kupata bajeti ya karibu shilingi milioni 300 ili kuleta njia kwa wodi kuweza kutembelea *walk ways*, lakini vilevile kumalizia wodi ya akinababa na akinamama ili hospitali hii iweze kufunguliwa na wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini waweze kupata huduma za matibabu katika hospitali yao ambayo Serikali imewapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa vituo vya afya tunashukuru kwa Kituo cha Afya Haydom, Eshkesh vilevile Masieda na Maretadu, ninajua Kituo cha Maretadu kimejengwa, lakini bado hakijakamilika hasa wodi ya akinamama vilevile hatuna sehemu nyingine, hapo tunahitaji karibu shilingi milioni 200 ili huduma ianze mara moja na wananchi waweze kupata huduma zile ambazo wamezingojea kwa muda mrefu sana. Ninaomba TAMISEMI itusaidie fedha hizo ili tuweze kukamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwamba kwa upande wa zahanati tunayo maboma 13 na tumewasilisha TAMISEMI; Vijiji vya Qamtananat, Getanyamba, Yaeda Ampa, Endahagichan hivi ni kwa uchache, ninaomba sana Wizara itusaidie ili tukamilishe ili wananchi waweze kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu, tunashukuru tumepata shule mbili za amali za sekondari na zimeanza kazi, lakini tunazo shule nne ambazo wananchi wamezijenga katika Kijiji ya Yaeda Ampa, Mangisa vilevile Haydarer, Qaloda na Getanyamba. Katika kila shule ya sekondari, kutokana na wingi wa watoto wananchi wamejenga madarasa mawili hadi manne.

Hapa tunaomba Serikali itusaidie angalau madarasa mawili mawili ili yaweze kufanya kazi na watoto wanaotoka umbali wa kilomita 12 hadi 15 na wakati mwingine kutembea usiku wapate shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kushukuru sana kwamba tunazo pia shule shikizi, nazo wananchi wamejitahidi; niiombe TAMISEMI itusaidie. Tunazo shule sita ambazo nazo wananchi wamezijenga, lakini wameshindwa kuzikamilisha kutokana na hali ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumza kwa uwazi kuhusu kuzuia matumizi ya lumbesa kwenye upimaji wa mazao ya kilimo ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi wananchi wanapima mazao kwa kilo, lakini katika masoko yetu wenzetu wanaotoka nchi jirani wanaingiza kwa lumbesa, hivyo kusababisha ushindani kuwa mdogo kwa wakulima wetu wa ndani. Kwa hiyo tunaomba usawa uwepo katika masoko; kwamba kila mmoja kama anapima kwa kilo, atoke nje, atoke ndani waingize kwa uzito ule ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ya stakabadhi ghalani ambayo wananchi wangu wanapata changamoto katika zao la dengu na zao lingine. Changamoto ya zao hili ni kwamba wananchi wengi wanatumia umbali mrefu sana kusafirishia mazao yao…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia, muda wako umekwisha.

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba jambo hili litazamwe kwa umakini. Ninaomba niseme kuwa ninaunga mkono hoja; na jambo hili la stakabadhi ghalani liangaliwe ili wananchi wapate bei sahihi na vilevile wapate fedha zao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Josephine Joseph Kakoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mheshimiwa Athumini Omary Mapalilo na Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija wajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote ninapenda kumshukuru Mungu kwa kutujalia uzima na kunipa siku hii ya leo. Kipekee kabisa ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kukosa usingizi kwa ajili ya wananchi wa Tanzania. Hotuba yake aliyoitoa jana imeleta matumaini makubwa sana. Ukiangalia hotuba ile na kuisikiliza unamwona kabisa moyoni mwake na machoni mwake anatamani kama Tanzania ingekuwa mtoto aipakate ainyonyeshe; lakini kwa sababu tumekomaa ametuacha tuendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. Kwa kweli mimi ndiyo mara yangu ya kwanza kuingia Bungeni. Nilivyokuwa ninawaona Mawaziri Wakuu zamani kabla sijaingia Bungeni nilikuwa ninajua kuwa ni watu wasiofikika; lakini kwa ziara ambazo wamezifanya kwa siku chache tumeona kabisa kuna mambo yanatendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, kwa kuwakilisha Wanamorogoro nilikuwa ninamwomba tukimaliza Bunge hili aanze na Morogoro kwa sababu tunamsubiri kwa hamu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii pia kuwapa pole ndugu zangu wa Morogoro na Watanzania waliokubwa na athari ya mafuriko. Kipekee kabisa kwa Morogoro watu wa Kilombero, Mvomero na Ifakara na Kilosa. Ninaendelea kuishukuru Serikali yangu kwa kuendelea kutukimbilia kila tunapopata maafa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba niende moja kwa moja katika kuchangia hoja ya Waziri Mkuu. Leo nitajikita moja kwa moja kwenye hitimisho la Hotuba ya Waziri Mkuu na nitaangalia sana eneo la msisitizo mosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msisitizo mosi kutoka kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu imeelezea kuanza utekelezaji wa dira ya mwaka 2020 - 2050. Sasa, nimekuwa nikiangalia kwa mapana suala hili kama tunataka kufika huko kwenye dira ya 2050. Sisi Morogoro ni kati ya mikoa ambayo tuna utajiri wa viwanda vingi sana. Viwanda hivi kimsingi havifanyi kazi kwa muda mrefu. Viwanda ambavyo havifanyi kazi ni kama vile *Moproco, Morogoro Ceramic, Morogoro Canvas, Morogoro Shoe* na *Morogoro Leather Goods*. Pia tuna kiwanda cha kusindika matunda ambacho kilizinduliwa na Hayati Lowassa na hakijawahi kufanya kazi tangu kimezinduliwa hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekaa ninatafakari, kama kweli tunataka kufika huku tunakotaka kufika, lakini tukiwa tuna rasilimali ya viwanda hivi ambavyo havifanyi kazi, kweli tunaweza kufika huku tunapotaka kwenda? Sasa ninaomba tu Wizara ya Viwanda kwa kushirikiana na Wizara ya Mipango na Uwekezaji, ifike muda sasa tuone Morogoro hii ya viwanda vilivyolala tunaifanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu tulikuwa tuna Kiwanda cha Tumbaku cha *TLTC* ambacho kilikuwa hakifanyi kazi, lakini miaka mitatu iliyopita kile kiwanda kilifunguliwa tena na kuchukuliwa na Mkwawa *Tobacco*. Tangu kimezinduliwa kimekwishaajiri wafanyakazi *permanent* wapatao 700 na wafanyakazi wa msimu wapatao 2,100. Pia tuna kiwanda cha Mazava kinachofanya kazi ambacho kimeajiri wafanyakazi zaidi ya 1, 500. Vilevile tuna kiwanda cha *Alliance One* cha *Tobacco* ambacho kimeajiri wafanyakazi *permanent* zaidi ya 300 na wa msimu zaidi ya 3,000. Kwa hiyo kwa jicho la karibu ukiangalia kabisa ni kwamba, hivi viwanda ambavyo vimelala vikifufuliwa utaona kabisa uchumi wa Morogoro unaenda kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho kinasikitisha zaidi, sasa hivi tuna Wachina wanaochukua yale mawe meupe Morogoro Vijijini kwenda kutengeneza *tiles* na ninadhani *cement,* kama sikosei. Hata hivyo, Morogoro tuna Kiwanda cha Morogoro Ceramic ambapo ile *process* ingeweza ikafanyika pale Morogoro *instead* ya kuchukua yale mawe na kuyapeleka mbali. Sisi watu wa Morogoro tukipata hivi viwanda hata hii kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja wa 10% hatutahitaji kwa ukubwa huo. Hii ni kwa sababu hivi viwanda vitatosheleza kutuletea ajira Wanamorogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kukuza ajira tu kwa Wanamorogoro, lakini pia uchumi wa mtu mmoja mmoja, uchumi wa mkoa na uchumi wa nchi. Si hivyo tu; kule Mahenge kuna mgodi ambao wawekezaji walishaingia; Mgodi wa Kinywe, mwaka 2025, lakini mpaka sasa hivi haujaanza kazi. Kwa mara ya mwisho kwa taarifa ambazo nilikuwa nimezipata ni kwamba, watu hawajapata fidia kwa ajili ya kupisha zile sehemu za mwekezaji kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa makadirio ya haraka huu mgodi ungefunguliwa ungetoa ajira si chini ya 4,500. Si tu ajira, ungeongeza kipato na uchumi kwa Ulanga, Mahenge na Mkoa wa Morogoro nzima. Sijui shida ipo wapi kwa sababu mwekezaji yupo tayari, ni wapi ambapo sisi kama Serikali tunashindwa kumpa ushirikiano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo. Mara ya mwisho alifanya ziara katika Viwanda vya Sukari Morogoro. Kwa kweli tumeona tija kubwa katika viwanda hivyo na katika uwekezaji. Katika ziara ile bado ninataka kuchelea kama wachangiaji wengine ambao wametangulia; kwamba tuna shida Morogoro ya miundombinu. Bila kuwa na miundombinu sahihi hatuwezi kufika katika hii *target* ambayo tunaitaka kwa sababu hivi vitu vina-*go hand to hand,* maendeleo yanaenda *hand to hand* na miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Morogoro ni kitovu cha uzalishaji, ni kitovu cha kilimo, ni kitovu cha viwanda. Sasa ninaiomba Serikali ituangalie Morogoro kwa jicho lingine, jicho la karibu sana. Tuna uhitaji mkubwa. Morogoro wakituwezesha katika miundombinu nina uhakika tuna uwezo wa kuilisha Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiomba Barabara ya Mlimba kwa muda mrefu, tumekuwa tukiomba Barabara ya Bigwa - Kisaki, tumekuwa tukiomba Barabara ya Malinyi, hizi sehemu zote ni *potential* kwa kilimo cha mchele na karafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na miundombinu mibovu wakulima inabidi wauze mazao yao kwa bei ndogo, lakini tungepata miundombinu ambayo ni sahihi ingekuwa rahisi wao kuyafikia masoko bila kutumia madalali. Kutokana na miundombinu kuwa mibovu kama gunia lilitakiwa liuzwe kwa shilingi 30,000 mkulima anauza kwa shilingi 2,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba Serikali, *TARURA*, *TANROAD* watuangalie kwenye suala miundombinu Wanamorogoro. Wananchi wa Morogoro wamenituma, hasa wanawake wa Morogoro wamenituma mimi kama mtumishi wao ninaomba Serikali ituangalie kwa jicho linguine. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Athumini Omary Mapalilo, Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija na Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo wajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kabla sijasahau ninataka kuungana na dada yangu hapa Josephine, kuunga mkono hoja yake ya kufungua mkoa wetu na kuendelea kuufanya Mkoa wa Morogoro kuwa ghala la Taifa la chakula. Tayari mkoa wetu wataalam wameshaandika *paper* nzuri sana, hivyo ninaomba sana Serikali ichukue iusajili ule Mradi wa 27/32 wa kuufanya mkoa ule

uendelee kuongoza katika kilimo cha mpunga, mambo ya pamba na miwa ya sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaanza kuchangia. Ninapenda kutoa shukrani kama wenzangu walivyosema kwa kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ndiye tunajadili bajeti yake hapa. Kaka yetu anafanya kazi nzuri sana, na sisi wadogo zake tuliokuwa naye katika chama tunafurahia sana. Aendelee kupiga kazi na Mungu ambariki sana. Hivi alivyoanza watu walidhani labda ni danganya toto. Sasa hivi ukitazama hata kwenye *comments* huko wanasema sasa tunaanza kumwelewa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu asije tu akasahau hiyo skafu siku moja, wataongea sana. Mungu ambariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikisimama mara zote hapa ninasema wananchi wa Kilombero wamenituma mambo mawili, kushukuru na kuomba tena. Awamu iliyopita hapa nilimpongeza Mheshimiwa Rais na kushukuru, nikasukumwa sukumwa takriban wiki nzima. Vilevile katika mchango nilioutoa Bunge lililopita Mheshimiwa Waziri Mkuu ninamshukuru sana, nilisema tu kuhusu kilio cha wakulima wa miwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo alikuwa Waziri wa Uwekezaji na Waziri wa Kilimo ilikuwa aje, lakini alipata dharura, ili kufuatilia malalamiko yale ambayo nimeyatoa. Tumemwona Mheshimiwa Rais amewaita wawekezaji wakubwa wa Ilovo kutoka Uingereza, wamekuja pale Ikulu amekaa nao kwa ajili ya utatuzi wa kero hizi za wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na haya tukimpongeza Mheshimiwa Rais kwa nini wengine wananuna? Mbona wao kila siku wanasema Kamanda tuvushe, wanamsifia kila siku Kamanda wao? Kwa hiyo sisi tunaendelea kusema kuwa tunampa sana *comfort* sana Mheshimiwa Rais. Tunamwomba Mheshimiwa Rais aendelee kuiongoza nchi yetu kwa bidii kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yanayotokea duniani yanatufundisha kutii viongozi wetu ilimradi wanatuambia mambo ya msingi siyo ya kumkufuru Mwenyezi Mungu; kuwatii. Tunaona mifano ya vita vinavyoendelea duniani, watu wanasalimika kwa sababu ya kuheshimu viongozi wao. Dunia tunayoenda sasa wanyonge wanaogopa hata kuungana dhidi ya bepari, kama mwalimu aliposema wakati ule; kwamba wanyonge wasipoungana watapigwa tu na watasambaratishwa. Kwa hiyo sisi tunaomba tumtii kiongozi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipo kisa huko nyuma enzi za Mtume *(S.A.W)* watu walikataa kumtii kiongozi wao katika maelekezo halali wakapata matatizo makubwa, walishinda vita, wakakaa mlimani akawaambia msishuke hapa, wakampuuza wakamdharau, wakashuka; wakapigwa sana. Kwa hiyo kwa kuwa viongozi wetu wa Serikali wanatuelekeza katika mambo ya msingi ni vizuri kuwatii na kuwafuata ili tuweze kupata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo ninashukuru sana viongozi wangu wa mkoa, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, Mkurugenzi wangu wa Halmashauri na katika Katibu Tawala za Mkoa kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hapa tunazochangia mimi ninataka kujikita kidogo katika TAMISEMI. Katika mpango wetu wa miaka 25 na miaka 50 utaona kuwa TAMISEMI imebeba mambo mengi sana. Waziri wetu wa Mipango na Uwekezaji alituambia hapa, kwamba nchi hii haiwezi kuendelea endapo hatufanyi ugatuzi wa madaraka, hatufanyi namna mbalimbali za kushusha mamlaka kule kwa Baraza la Madiwani na kule chini kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba Waheshimiwa Wabunge tuitazame TAMISEMI vizuri na hasa kule kwenye *TARURA*. Alikuja Mheshimiwa Rais kuhutubia Bunge hapa, Wabunge tulipiga makofi ya ishara ya kumwambia Mheshimiwa Rais tuna salamu kwenye *TARURA,* kama Wabunge wanakumbuka. Makofi yale yakamfanya Mheshimiwa Rais akatoa maelekezo, akasema kuwa hapa kwenye *TARURA* ninafikiri kuna tatizo, kwa hiyo

nitaangalia vizuri. Kwa hiyo wakati wa bajeti ndiyo huu, ni lazima watoe fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa *model* hapa; katika Bunge lililopita maamuzi mazuri ya Serikali yalifanyika katika Wizara ya Maji na Wizara ya Kilimo ya kununua magari ya uchimbaji visima, yanatusaidia sana mpaka leo. *Model* ile ya *TARURA* mpaka leo ninaendelea kuisisitiza. Watafute wilaya za kufanya mfano. Tumefanya tathmini itatutumia miaka 30 sisi kumaliza hata barabara zetu za mitaa tulizosaijili peke yake. Hivi, hatuwezi kuwa na greda, tipa, rola na eskaveta katika baadhi ya wilaya za mfano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kama sisi Kilombero tuna kifusi, Mbunge ukifanya juhudi halmashauri ikishafikisha mapato ya bilioni saba inatakiwa itenge takriban shilingi milioni 500 za barabara; wakanunue mafuta, wakatumie vifaa hivyo kuweka hata vifusi kwenye barabara za wananchi ili zipitike kwa muda wote. Vinginevyo hizi bilioni mbili tunazopewa kwa mwaka; mimi ninapewa bilioni mbili sijui na nusu; haiwezekani kumaliza changamoto hizi, changamoto kuhusu *TARURA* zimeshavuka mpaka. Barabara zetu zina hali mbaya sana;

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninataka niseme, kwa mfano sisi tuna madaraja ya msingi sana, kwa mfano, Daraja la Mkasu pale Kiberege, alikuja Waziri wa TAMISEMI wa wakati huo ametoa maelekezo pale ili mkandarasi aanze. Ameanza yule mkandarasi kumbe hana mkataba. Hadi leo wanamwambia kuwa hii iliyofanyika hapa ni siasa. Mtu ameshamwaga zege pale; kila siku analia kwa Mbunge, anakuja Dodoma hapa na video ya Waziri akielekeza ujenzi ule uanze ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Daraja la *Msolwa Station*, Funguo na Mang'ula, tuna barabara chafu na mbaya. Leo nilikuwa ninaongea na Diwani wa Mang'ula tunatafuta nguzo za kuweka Mang'ula B ili wanafunzi waende shule. Hali ni mbaya kwa hiyo tunasema, ikiwa tukifuata hii *model* ya kununua vifaa kwa kweli itatusaidia; vinginevyo tutatumia miaka mingi sana kumaliza barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ya Nyange kwenda Msolwa Station, tunaomba wtusaidie; kuna Barabara ya Mwaya kwenda Mwikoleko na hapa Mang'ula B niliposema; lakini kimsingi ni takriban kata zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna maboma, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengine wamezungumza. Tunaomba Wizara ya TAMISEMI itusaidieni angalau maboma 30 tu ya madarasa na angalau maboma 10 tu ya zahanati yamalizwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana TAMISEMI, nimepata Kituo cha Afya kipya cha Lumemo – Iyanga, ninawashukuru sana. Hata hivyo, ninaomba watusaidie kumalizia maboma haya ambayo wananchi wamefanya juhudi kubwa kuyajenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tumekutana nalo katika ziara yetu tulipopita huko linagusa pia TAMISEMI ni ushuru wa mazao ya mpunga. Nchi hii tuna Rais mmoja, akishaelekeza jambo linatakiwa lifanyiwe kazi. Mheshimiwa Rais alikuja mwaka 2024 mwezi Agosti pale akasimama Mang'ula mwenyewe akiongea na wananchi; nitakutumia *video*; akasema nimesikia mnatozwa ushuru unaowakera hapa. Mapato ya ushuru ni muhimu, lakini tutapunguza ushuru sio huo ambao mnatozwa mnaoulalamikia. Mpaka leo Geti la Idete wananchi wanalalamika kwa kutozwa ushuru mkubwa. Sisi tukizungumza tunaambiwa tunafanya siasa, lakini tunapita kule chini kwa wananchi tunaona hiyo ni kero kubwa sana. Tunaomba TAMISEMI watusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tupo katika mpango wa *TACTIC,* wananchi wa Ifakara Mjini wamekwishabomoa soko, wamehama katika soko la mjini pale, wamesogeza mabanda yao ili soko lijengwe na *TACTIC*. Vilevile tuna Mradi wa Stendi, tuna Mradi wa Lami; tunaomba miradi hiyo ianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni miongoni mwa majimbo ambayo yamepata kadhia kubwa ya mafuriko. Ninataka

kuishukuru Serikali katika Bunge lililopita tulijaribu kujenga tuta upande mmoja wa mto limezuia maji yale angalau pale Ifakara Mjini hayakufika; lakini upande wa pili imekuwa adha kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la mafuriko linahusu Wizara mtambuka; kama vile Wizara za Kilimo, Maji na Wizara ya Nishati; kwa sababu sisi katika Mto Lumemo tunajaza maji kwa kiasi kikubwa katika Bwawa la Mwalimu Nyerere. Tunaomba Wizara hizi zikae kwa pamoja zitafute namna ya kuweza kufukua mto unaopita Ifakara Mjini, mji ambao una wakazi takribani 100,000, kuufukua na kuendelea kuuboresha kama wazee wa zamani walivyokuwa wanaweka yale matuta ili kuhakikisha kwamba maji yale hayawagharimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pole sana kwa wananchi wangu kwa mafuriko waliyoyapata, ninaendelea kuomba wadau wote waendelee kuwasaidia na Mungu atubariki sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Athumin Omary Mapalilo, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, pamoja na Mheshimiwa Lutengano George Mwalwiba wajiandae.

**MHE. ATHUMIN O. MAPALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia kwenye Bunge hili Tukufu ninaomba nitoe shukrani kwa Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunifanya na mimi niwe miongoni mwa Wabunge katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa ninamshukuru Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuona ninafaa nami kuwa miongoni mwa Wabunge. Ninampongeza pia Mheshimiwa Spika kwa uongozi wake mahiri ambao anatufanya Wabunge tulioko humu tuendelee kutekeleza majukumu yetu vizuri pasipokuwa na changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee pia ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imesheheni mahitaji mazuri kabisa na kutatua changamoto za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Mtwara kwa kipekee kabisa kuona kuwa ninafaa na mimi kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu na kunipa kura za ndiyo nyingi sana, ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nijielekeze moja kwa moja kwenye kuchangia hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ajira kwa vijana limekuwa kubwa na linafahamika ni tatizo ambalo linakabili nchi zetu za kiafrika na Tanzania ikiwemo, lakini pamoja na kuwepo na changamoto hii ya ajira, bado ipo haja ya kama Serikali yetu kuona namna ambavyo tunaweza kuwasaidia vijana wetu. Ninaipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutatua na kuona umuhimu wa kwenda kutatua changamoto ya ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais na Serikali yake aliona bora kuanzisha *program* nzuri na mahiri ya uanagenzi, ambayo kwayo itawasaidia vijana wetu waweze kupata mafunzo ya muda mfupi ambayo itaweza kuwasaidia kupata soko la ajira kwa urahisi kulingana na mandhari ya teknolojia iliyopo kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo kwa elimu ya *VETA* ambayo inatoa taaluma kulingana na mitaala ambayo ipo, pia Serikali hii iliona ni vema sana kuanzisha hii *program.* Kwa kweli ni nzuri na ina tija kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uzuri huu, zipo changamoto kadhaa ambazo zinaifanya tasnia hii ya uwanagenzi waweze kuyumba kidogo katika kutekeleza majukumu yao. Ninapenda kushauri mambo kadhaa ambayo

Serikali ikiangalia kwa jicho lake la kipekee, inaweza kutengeneza tija ama inaweza kuleta tija kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na kutokana na hamasa kubwa ya vijana ya kuelewa umuhimu wa kwenda kujifunza masomo hayo ya muda mfupi, imetokea kuwepo kwa wimbi kubwa la vijana ambao wanapenda kwenda kujifunza na nafasi ni chache za kujiunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitolea mfano katika Mkoa wetu wa Mtwara, katika Chuo cha Wananchi Mtawanya, vijana ambao walijitokeza kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ni vijana 500 na ambao walipata nafasi ya kujiunga kwa mwaka huu ni vijana 130 sawasawa na 26% ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Newala kilichopo Mtwara, vijana 150 waliweza kujitokeza kuomba, lakini ambao wamepata nafasi hiyo ni vijana130. Utaona namna gani bado uhitaji ni mkubwa kwa vijana wetu lakini nafasi ya kupata ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni vifaa vya kujifunzia na kufundishia viko vichache na pia bado vipo kwenye teknolojia ambayo haiendani na muda wetu wa sasa hivi. Pia baadhi ya wahitimu wanapata changamoto ya kuajiriwa katika taasisi binafsi na makampuni na changamoto nyingine ni ukosefu wa mitaji. Ninayo maoni kadhaa ili kuweza kutatua changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu; kwanza ni kwamba, ninapendekeza Serikali sasa iweze kuongeza nafasi kwa vijana wetu, ili vijana wote ambao wanaomba wapate nafasi ya kujifunza na waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi mwingine ambao ninaupendekeza ni uwepo wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya kisasa, ambavyo vitaweza kuwasaidia kukabiliana na changamoto ya ajira na pia kukabiliana na *competition* ya ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza pia kuwepo na motisha kwa mashirika na makampuni ambayo yana uwezo wa kuwaajiri vijana wetu, inawezekana kwa sababu ni kozi mpya na wengi hawaifahamu. Kwa hiyo basi, kama tutawapa maelekezo na tukawafundisha tukatengeneza *awareness* kwa haya makampuni na mashirika kutambua umuhimu wa tasnia hii ya uanagenzi wanaweza kupata ajira na nafasi ya kuajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu ya kwamba vijana wetu ambao wanajifunza ni wengi na siyo vijana wote ambao wanaweza kupata nafasi ya kuajiriwa kwa mashirika na makampuni ambayo tunatamani waajiriwe. Hivyo basi, ili sasa waweze kujiajiri wenyewe vijana ni vema Serikali yetu sikivu iweze sasa kuona namna bora ya kuwapa mitaji vijana wetu. Mitaji hiyo inaweza ikawa vifaa au inaweza ikawa fedha na wanaweza wakapata mitaji hii kwa kupewa ruzuku, lakini pia kama ruzuku inakuwa haiwezekani ama ni ndogo, basi wanaweza wakazingatiwa kwenye mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninazungumzia mikopo ile ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, lakini pia mikopo ya wamachinga yaani wajasiriamali wadogo. Yale madawati yaelekezwe kwamba watoe kipaumbele kwa vijana wetu ambao wameshajifunza elimu hii ya uanagenzi na sasa waweze kupata mtaji na waweze kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu wakijiajiri itasaidia sana kwa kiasi kikubwa kupunguza *gap* la kuwa *jobless,* lakini pia itawasaidia kuajiri vijana wenzao. Vilevile, watajiongezea kupata kipato wao wenyewe na pia tutaongeza kipato cha nchi yetu kwa sababu tutakuwa na kundi kubwa la wafanyakazi, watendaji wa kazi na uzalishaji utakuwa mkubwa na utaongezeka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa siku ya leo na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako, nilimwita Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija, atafuatiwa na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo na Mheshimiwa Lutengano George Mwalwiba wajiandae.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi uliyonipa ili niweze kutoa mawazo yangu. Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kibali cha siku ya leo ya kuweza kusimama humu Bungeni. Kipekee nimshukuru sana Jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amewekeza fedha nyingi kwa Watanzania na hasa katika kuwaletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Nchemba, Mawaziri wote na Manaibu Waziri, watendaji wote wa Serikali kwa namna ambavyo wanaleta faraja kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina-*declare interest* kwamba, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI. Nimepita katika kuzunguka kwenye miradi mingi ya kitaifa inayoshughulika na mambo ya afya. Tumeshuhudia uwekezaji mkubwa wa Serikali uliowekezwa katika hospitali zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania hawa wengi walikuwa wanapata huduma za kibobezi nchi za nje, lakini leo uwekezaji tuliouona nchi yetu hakika Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan analo kusudi kubwa la kunusuru maisha ya Watanzania. Tumpongeze sana kwa kazi nzuri tulizozishuhudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niweke ushauri mchache kwa maeneo machache. Kwenye eneo la afya na hasa kwenye eneo la afya ya msingi. Taifa latu bado tuna changamoto kubwa ya watumishi wa idara ya afya. Nichukulie mfano Wilaya ya Kaliua yenye majimbo mawili, uhitaji wa watumishi wa afya wastani ni 895. Uhalisia wa watumishi tulionao ni 267 sawa na 29.8%. Kwa hiyo, bado mahitaji ni makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ningeendelea kuiomba Serikali kuendelea kuangalia uwekezaji kwa kupeleka watumishi kwenye maeneo ambako, Serikali imewekeza fedha kwa maana ya kuboresha afya za Watanzania. Tunavyo vituo vya afya vingi, mathalani Wilaya ya Kaliua tunazo hospitali za wilaya, lakini tunavyo vituo vya afya nane vinavyotoa huduma na zahanati 47. Hali hiyo ukienda kwenye uhalisia wa watumishi unaweza ukaona ni namna gani shida kubwa ya wananchi wanavyohangaika kuwapata watumishi. *(makofi)*

Msheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze namna ambavyo watumishi wanajituma kufanya kazi. Watumishi wanaingia mara tatu mpaka mara nne kwa siku. Jambo hilo linapunguza morali ya utoaji wa huduma katika huduma hizo za afya. Kwa hiyo, niendelee kuiomba Serikali yangu ione namna ya kuongeza watumishi kwenye vituo vya afya na hospitali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Ulyankulu lina vituo vya afya vinavyotoa huduma viko sita. Umbali wa kutoka Jimbo la Ulyankulu kwenda Makao Makuu ya Wilaya, ukitokea Kijiji cha Bulela ni kilometa 190 eneo ambalo kwa maana ya mwananchi mwenye changamoto ya rufaa, mara nyingi tunatumia gharama kubwa, lakini tunapoteza watu wengi kutokana na umbali wa upatikanaji wa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali yangu pendwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, la kwanza, kukipandisha hadhi Kituo cha Afya cha Ulyankulu, ili kiweze kuwa na hadhi sawa na hospitali ya wilaya, ili kupunguza umbali wa kusafirisha wagonjwa kwa kuwapeleka umbali wa zaidi ya kilometa 190. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka Ulyankulu kwenda Tabora ni kilometa 90, bado ni eneo la umbali sana kwa maana ya kwenda kupata huduma. Kwa wastani Kituo cha Afya cha Ulyankulu, kinatoa rufaa kuanzia wagonjwa 20 lakini chenyewe kinapokea wagonjwa 20 kutoka kwenye zahanati kwa wastani kwa mwezi. Kwa hiyo, tunaweza tukaona namna ambavyo kituo cha afya hiki kilivyo *busy* na hilo eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Ulyankulu lina wakazi 283,537; idadi hii bado ni kubwa. Kwa hiyo, ombi langu la kwanza ni hilo. Lakini niendelee kuishukuru Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, wiki mbili zilizopita tumepokea shilingi milioni 675.5 kwa ajili ya ujenzi na uongezaji wa majengo kwenye Kituo cha Afya cha Mwongozo. Ninashukuru sana, hongera sana kwa Serikali na Wizara kwa kutuona kwa hilo. Hata hivyo, hiyo haitoshi, bado ninaendelea kuiomba Serikali iangalie kukiimarisha Kituo cha Afya cha Ilege, Kashishi pamoja na Uyowa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nilete mawazo mengine kwenye vituo vyetu vya afya. Tuna changamoto kubwa ya maji na umeme. Niombe Serikali ikipendeza suala la maji na umeme kwenye vituo vya afya, liwe kipaumbele kabisa kuliko kubaki kama ilivyo. Wanaomba lakini umeme umechelewa kufika na muda mwingine maji hayafiki kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie hali ya barabara. Jimbo la Ulyankulu linalo changamoto kubwa ya miundombinu ya barabara. Bajeti yetu ya miundombinu inayoingia ndani ya Jimbo la Ulyankulu, tunayo bajeti ya shilingi bilioni 1.9 mtandao wa barabara ni kilometa 471 lakini 51% ndiyo zenye wastani wa kawaida, 49% ni barabara mbovu kabisa ambazo hazipitiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali pendwa ituongezee bajeti ili kuhakikisha kwamba maeneo haya yanaweza kufikika hasa Barabara hizi za Chemba, Ng'ande, Mwongozo lakini kwenda Kashishi na eneo la Ilege na Kashishi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuendelea kuiomba Serikali yetu, nina-*declare interest,* nimekuwa diwani kwa muda wa miaka 15. Tunavyozungumza uongezaji wa mapato, mchango wa Waheshimiwa Madiwani ni mkubwa mno. Kaliua ilikuwa na bajeti ya shilingi 4,000,000,000; leo tunazungumza tuna uwezo wa kukusanya shilingi bilioni 9.5 na kwa bajeti hii tunaikadiria tunaweza tukakusanya shilingi 11,000,000,000. Niiombe Serikali yangu pendwa, ijaribu kuona namna ambavyo

Mheshimiwa Diwani anaongezewa posho yake ama kutoka kwenye mapato yao ya halmashauri ama kutoka Serikali Kuu, hata hivyo iendane pia na kiinua mgongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madiwani wanafanya kazi kubwa sana. Muda wate kwenye majimbo ndiyo wanaotushikia, muda wote ndiyo wanaohamasisha. Tunawapa fedha nyingi, kama halmashauri inapewa zaidi ya shilingi 57,000,000,000 anayezisimamia pale ni Mwenyekiti wa Halmashauri na Baraza lake la Madiwani. Iko haja ya kuwaona hawa watu kuona namna ambavyo Serikali inaweza ikawa-*support*. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lufungija.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia tuwakumbuke pia Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji kwa namna yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nilimwita Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, atafuatiwa na Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo; Mheshimiwa Lutengano Mwalwiba na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi wajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Ofisi hii ya Waziri Mkuu kupitia hoja waliyoiwasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza nianze na ku-*quote* Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati akifungua Bunge. Anasema "*Hivyo basi ni lazima viongozi wa Serikali kuanzia ngazi zote (Mawaziri hadi Maafisa Tarafa) wawe karibu na wananchi ili kuweza kufahamu changamoto zao na kuwajibika kwao. Wananchi wanahitaji mabadiliko chanya*

*kwa maendeleo, watendaji msipobadilika kuendana na matarajio ya wananchi tutawabadilikia".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na Mawaziri Wakuu wengi katika Taifa letu, lakini tumekuwa tunakumbuka Waziri Mkuu mmoja na tarehe 12 ya mwezi huu, tutaadhimisha kumbukumbu ya kifo cha Edward Moringe Sokoine. Amekuwa kama ni nyota wa mchezo katika ligi ile ya Mawaziri Wakuu, ameendelea kushikilia chati hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu gani? Ni kwamba Hayati Sokoine ali-*play* kazi kubwa ya kuiendesha na kui-*coordinate* Serikali. Vivyo hivyo, katika kizazi chetu na katika nyakati hizi, Mheshimiwa ndugu yetu Dkt. Nchemba ameweza kupata nafasi hii ya kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio makubwa ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na lile alilosema kwamba Serikali atakayoiunda, lakini kiranja wa Serikali hiyo ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninataka niseme *coordination* ya Waziri Mkuu ndiye dereva mkuu wa nchi yetu tuweze kufika wapi. Sisi tuna matarajio makubwa kupitia kwa ndugu yetu Dkt. Mwigulu Nchemba kwamba ana uwezo wa kuweza kusimamia nchi yetu iweze kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona ziara zake, lakini maswali ya kujiuliza; inakuwaje Waziri Mkuu akienda anagundua uozo ndani ya halmashauri zetu, ndani ya mikoa yetu ilihali kuna viongozi wengi wako kule? Hii inaonesha kwamba bado hatujawa na *spirit* ya Serikali kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali inajiendesha kwamba kuna ziara ya kiongozi ndipo inapofanya vizuri. Kwa hiyo, kuna kazi kubwa ambayo inatakiwa Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kuja na *modality* kubwa zaidi ya kuweza kutoka hapa tulipo, nchi yetu iweze kutoa huduma kwa wananchi wake kupitia viongozi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nichangie maeneo mawili, lakini kubwa zaidi Serikali ya Rais Samia imefanya kazi kubwa kwa ujenzi wa madarasa, kwa ujenzi wa miundombinu ya afya na kupeleka umeme kwenye vijiji. Tatizo lililopo ni kwamba vijiji vyetu tunaishi kiholela. Sehemu ya kulima na sehemu ya kuishi watu wanaishi hapo hapo. Ile dhana ya ujamaa ya kupeleka makazi, wananchi wakae sehemu moja na huduma za afya ziende pale na huduma za elimu ziende pale ilikuwa ni jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa wameendelea na utaratibu huo. Ipo sehemu ya watu kuishi na sehemu ya kwenda kulima. Sasa baadhi ya maeneo na kama Mkoa wa Dodoma, Wilaya yangu ya Bahi, vitongoji vingi vimekuwa vinaibuka. Sasa ujenzi wa shule utaendelea kila wakati kwa sababu tuna makazi holela. Serikali kupitia Ofisi ya Mipango, Wizara ya Mipango iko haja ya kupima ardhi yetu, tuseme hii ni ardhi kwa ajili ya kilimo, hii ni ardhi ya ufugaji, hapa ni kwa ajili ya makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu tukitaka mwekezaji wa hekari 5,000 ni changamoto kubwa kuzipata. Hii ni kwa sababu hatuna ardhi iliyotengwa, kupimwa na kuwekewa utaratibu mahsusi wa matumizi. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye jambo hili la kupima ardhi yetu na mpango bora wa matumizi tulifanye miaka ijayo tutapata kazi kubwa kwa namna gani ya mpangilio wa matumizi yetu ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la elimu. Bado nchi yetu watoto wanakaa chini, kinachotushinda ni mbao na msumari kutengeneza dawati. Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba alibebe hili, zipo halmashauri zina bajeti ya bilioni 70, bilioni 68 kwa mwaka, lakini bado watoto wanakaa chini katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sisi ambao hatuna bajeti kubwa wala hatuna *excuse* ya kusema tunapata fedha ndogo kwenye halmashauri zetu. Aibu kubwa ambayo bado tunayo kwenye hii nchi ni watoto kukaa chini. Ifike mahali Serikali iseme tumejenga madarasa jambo kubwa, kwa nini kwenye madawati watoto wakae chini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ajenda ya watoto kukaa chini tuweze kuifuta, kwanza ni aibu na tunawaharibu kisaikolojia wale watoto tangu walivyokuwa bado Watoto. Mtoto anakaa chini na uzuri siku hizi madarasa yanajengwa yana *tiles*, yana *aluminium* lakini mtoto anakaa chini. Kama ni kipimo cha watendaji wa Serikali kiwe ni hicho. Hatuwezi kushindwa habari ya mbao na msumari nchi hii watoto wetu waendelee kukaa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni hali ya walimu wetu na watendaji wa afya ambao kwa ujumla ni wengi. Nilikuwa ninaangalia nchi nyingi za Asia wameanziasha Mfuko wa Kukopesha Watumishi hususani kada ya elimu na watumishi wa afya. Kwa maana gani, kama ambavyo Rais ametoa bilioni 200 kwa ajili ya vijana tunaweza tukatoa bilioni 200 kama *stimulus fund* kwa walimu wetu waweze kukopa kwa kiwango kidogo. Walimu wengi wana madeni wamechanganyikiwa wana-*frustrations* anaenda kukopa, anakatwa 18% kamshahara kenyewe kadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali ikiweka fungu la kukopesha walimu katika riba ndogo Mheshimiwa Waziri Mkuu jambo hili ni zuri, kwanza litaleta ahueni kwamba hawataenda kwenye kaushadamu. Walimu wengi harudi na mshahara ninaomba Serikali ilichukue jambo hili ni zuri tuweze kuliweka katika kusaidia walimu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nchi yetu imeheshimika sana katika miaka yote katika suala zima la diplomasia ya kimataifa. Sote ni mashahidi nami niipongeze nchi yangu imekuwa na msimamo thabiti, kinachotokea katika hata sasa bei za mafuta kupanda na uvamizi uliofanywa katika nchi ya Iran wote wapenda haki tunalaani hakuna *justification* yoyote ya uvamizi wa namna ile katika enzi hizi ambazo tuna Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama nilivyosema...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nollo, muda wako umekwisha ninaomba u-*windup*.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, atafuatiwa na Mheshimiwa Lutengano George Mwalwiba na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi na Mheshimiwa Moses Ludovico Kaegele wajiandae.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza ninapenda nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyenipa kibali cha kusimama katika Bunge lako hili. Haikuwa rahisi, lakini kwa uwezo wa Mungu hakuna kinachoshindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi ninaomba nianze kwa kuwashukuru viongozi wangu wa Chama Cha Mapinduzi kwa ngazi zote kuanzia Tawi, Kata, Wilaya, Mkoa hadi ngazi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda sana nitumie nafasi hii kumshukuru mama yetu kipenzi, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi wa Taifa, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya na sisi kama wanachama na viongozi tunaotokana na Chama Cha Mapinduzi jukumu letu ni kumtia moyo ili aendelee kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Makamu wa Rais ambaye tukiwa kwenye mchakato alikuwa Katibu Mkuu wa Chama chetu Cha Mapinduzi, wamefanya vizuri sana. Nami ninaendelea kuamini sote tuliopo humu hatukupita njia rahisi, wote tulioingia kwenye hili Bunge kila mtu anafahamu alipotoka na vile Mwenyezi Mungu amemjaalia hatimaye leo tumekuwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitatumia nafasi hii kumshukuru mama yetu kipenzi, mama

Chatanda: Mama Chatanda ni Mbunge mwenzetu katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pia ni Mwenyekiti wetu wa UWT Taifa, mama huyu amefanya kazi nzuri sana. Kwanza kuhakikisha anatenda haki kupitia vikao vyote ambavyo sisi Wabunge tumepita, alisimama na sisi akinamama wenzetu. Kwa kweli nilihisi sitotenda haki kama sitampongeza mama yangu hongera sana kwa kazi nzuri, Mwenyekiti wetu wa UWT tunamwamini sana na tunaahidi kumpatia ushirikiano mama yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajadili hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. Baada ya kujadili hapa kinachofuata ni kwenda kutekeleza, kukusanya mapato, lakini kwenda kutekeleza kile ambacho tutakipitisha hapa. Kama nilivyosema mwanzo kwamba mimi ni Mbunge ninayetokana na CCM ninafahamu Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi ambaye leo ndiye Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipita kwenye wilaya zetu, alipita kwenye majimbo lakini alipita kwenye mikoa yetu alitoa ahadi mbalimbali kutoka kwenye Chama Cha Mapinduzi. Tunafahamu ukiwa mgombea wa Chama Cha Mapinduzi unakabidhiwa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ambayo inaeleza miradi mbalimbali itakayotekelezwa kwenye ngazi husika, mama huyu ameahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sisi Wabunge tulioko humu ndani tumeahidi kwa wapigakura wetu iwe Mbunge wa Jimbo, iwe Mbunge wa Vijana, iwe Mbunge unayetoka Kundi la Wazazi na Wabunge wengine wote tumeahidi ahadi mbalimbali kupitia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo ninaomba niguse katika maeneo machache kupitia TAMISEMI. Bahati nzuri nilikuwa Diwani kwa vipindi vitano, nimeanza udiwani nikiwa ninapokea posho ya mwezi kwa shilingi 6,000 jamani siyo mchezo. Kwa hiyo, ninaomba niseme kwamba nina uzoefu kwa kiasi fulani kupitia TAMISEMI. Nimetaja TAMISEMI kwa sababu miradi tunayotekeleza; mara tu fedha zinapopitishwa hapa, hupelekwa katika halmashauri. Tuna miradi mbalimbali ambayo tumeahidi kuna miradi ya maji, barabara, vituo vya afya na ujenzi wa zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nitoe ushauri kwa Serikali yetu. Ninatoa ushauri kwa sababu nina uzoefu wa baadhi ya maeneo, tunaenda kujadili bajeti, lakini tuna miradi viporo kwenye maeneo yetu ambayo inawezekana kupitia Serikali zilizopita hiyo miradi iliidhinishwa, lakini haijakamilika haijapata fedha. Kwa hiyo, leo ninaomba niombe na nishauri Wizara ya TAMISEMI kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu twende tukatekeleze miradi viporo. Kufanyike tathmini ya kuangalia miradi iliyopo ambayo haijakamilika iende ikakamilishwe. Tuna ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, tumejenga madarasa, tumejenga hata ofisi za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine kwenye hii miradi ambayo ninazungumza, miradi viporo ni miradi ya nguvu za wananchi. Maeneo mengine wananchi wameamua wenyewe, maeneo ambayo hawana ofisi za Serikali wameamua kujenga kwa kuchangishana. Kwa hiyo, niombe twende tukawashike mkono, twende tukawatie moyo wananchi wetu ambao wana majengo na kule nyuma kulikuwa na kauli inatolewa kwamba wananchi wakijitolea, mwisho wa siku Serikali itawashika mkono kwa kumalizia majengo tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushahidi wa baadhi ya mejengo mbalimbali na kwa ajili ya muda nitapeleka ofisi ya TAMISEMI ili wayafanyie kazi. Ninaomba nisisitize nina ushahidi, hivi karibuni tukiwa katika hii likizo ya Pasaka, kuna ofisi za Serikali ambazo wamejenga kwa nguvu za wananchi, yaani inafika mahali Mtendaji wa Kijiji anatunza mafaili yake kwa kutembea nayo, kuja kwenye nyumba ambayo amepanga, lakini baadaye anarudisha nyumbani kwake kwa ajili ya usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa ukubwa wa Serikali yetu na chama chetu sioni kama hili jambo lina tija. Nilitamani leo nishauri kwamba tunapokwenda kutekeleza hii miradi tuangalie kwanza miradi viporo ambayo wananchi wamejitolea, majengo ya shule wananchi wamejenga shule. Mwenyewe hivi karibuni nimechangia kwenye shule moja, kuna shule ya Mtonya: shule ile haina hata nyumba moja ya mwalim,u lakini wananchi wameamua kujichangisha wenyewe, wamejenga jengo

hawajamaliza wanafika mahali wanaomba kwa viongozi wao. Kwa hiyo, ninaomba nisisitize kwenye hili eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende tuangalie miradi viporo, tuifanyie tathmini ili pesa zinapokwenda ziende kwanza zikamalize ile miradi. Wengine wamefyatua tofali kwa ajili ya ujenzi wa masoko, wengine wamefyatua tofali kwa ajili ya kujenga stendi na miradi mingine mingi tu ambayo inaendelea kwenye maeneo yetu. Kwa hiyo, nilitamani kwa siku ya leo kupitia Wizara ya TAMISEMI nishauri tuagize kwenye halmashauri zetu tupate ile miradi ambayo haijatekelezwa ili itekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo nilitamani kulizungumza ni suala la mikopo ya 10%. Tunafahamu kwamba hii mikopo kule nyuma ilikuwa inatolewa kupitia halmashauri. Ninapozungumza mikopo ya 10% ni ile mikopo ambayo inatengwa kupitia mapato ya halmashauri zetu, lakini tunatenga kupitia pato letu 10% kwa ajili ya kuwakopesha akinamama; vijana; na watu wenye ulemavu. Sijui ni kengele ya pili...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie kwa kusisitiza suala la mikopo. Tunaokusudia kuwasaidia ni watu wenye shida na hasa akinamama na vijana. Sasa kwa tafsiri hiyo niombe sana sana tupunguze masharti yaliyopo, akinamama wengine badala ya kutumaini mikopo hii wanakwenda kukopa kwenye vibanda umiza, kwa hiyo inawaletea madhara makubwa ya kunyang'wanywa vitu vyao na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona nisisitize katika maeneo hayo. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Nilikwishamwita Mheshimiwa Lutengano George Mwalwiba, atafuatiwa na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mheshimiwa

Moses Ludovico Kaegele na Mheshimiwa Said Ali Mbaruku ajiandae.

**MHE. LUTENGANO G. MWALWIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya bajeti. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijaalia afya na uhai leo nimepata nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii muhimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu pia ninachangia kwa mara ya kwanza, ninapenda kutumia nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Busokelo ambao wameamini na kunituma mimi kuwa mwakilishi wao. Ninachowaahidi ni kwamba nitawatumikia kwa kushirikiana nao na uwezo wa Mwenyezi Mungu kwa kasi na ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kwa kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Madelu Nchemba kwa kuaminiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nafasi ya Waziri Mkuu. Pamoja na Mawaziri wengine waliopo katika ofisi yake. Mheshimiwa Dkt. Nchemba, ninadhani ameanza kazi yake kwa kasi kubwa na anarejesha tumaini kwa Watanzania. Ninafikiri kwa mantiki ya kawaida Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba anachokifanya anajaribu kuweka mfano kwa watumishi wa umma namna bora ya kutumikia nafasi zao na kuhudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchangia hotuba hii katika Wizara ya TAMISEMI, nitoe pole kwa wananchi wenzangu wa Wilaya ya Rungwe ambapo kulitokea mafuriko pamoja na maporomoko na hivyo baadhi ya wenzetu wa Wilaya ya Rungwe walipoteza maisha, wengine waliumia na wengine walipoteza mali zao, ninawapa pole sana. Pia ninaishukuru Serikali kwa jinsi ilivyoitikia kwa haraka kuona ni namna gani na wadau wengine jinsi ya kuweza kushirikiana na wenzetu waliopata madhila hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kuchangia TAMISEMI. Wakati unawasilishwa Mpango wa Maendeleo hapa tulisema ili tuweze kupata maendeleo ya kweli, maendeleo na mapinduzi ya kweli ni lazima yaanzie ngazi za chini na tukisema ngazi za chini tunamaanisha TAMISEMI kwa maana ya kwenye mikoa; kwenye halmashauri zetu; kata zetu na vijiji vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaamini kabisa kwamba ili tuweze kufanya hivyo ni lazima sasa Bunge tuone namna gani ya kuweza ku-*empower* na kupeleka nguvu kubwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambayo inasimamiwa na TAMISEMI chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema hivyo? Ni kwa sababu TAMISEMI hadi sasa ipo Sera ya Ugatuaji wa Madaraka na sera hii tunasema kwamba ipo sera, lakini siyo sera tunatumia *policy statement* kutoka mwaka 1997 mpaka leo. Mimi ningetoa wito na rai, ningeshauri Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI waone namna gani wanaweza wakaharakisha kuiandaa sera hiyo pamoja na sheria ili kuweza kupeleka nguvu na mamlaka katika Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakifanya hivyo tutategemea tutapata matokeo makubwa sana. Tumesema kabisa kwamba Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana ya kupeleka maendeleo na kazi hiyo inafanyika kwa usimamizi wa wafanyakazi na watumishi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoweza kukisema hapa ni kwamba pamoja na changamoto zilizoelezewa hapa na baadhi ya Wabunge, lakini ni kweli kabisa kwamba TAMISEMI imefanya kazi kubwa sana. Tunapoongelea ujenzi wa huduma za afya, tunapoongelea ujenzi wa miundombinu ya elimu ni kazi nzuri ambayo imefanywa na TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya pamoja na Wakurugenzi wamefanya kazi nzuri sana.

Wapo Wakurugenzi, wapo Wakuu wa Wilaya na wengine ambao kwa kweli ni vichomi. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC,* tunakwenda kutembelea huko, tukienda kutembea tunaona baadhi ya halmashauri kweli changamoto za msingi zipo, lakini zipo halmashauri wanafanya kazi nzuri za kupigiwa mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu ni lazima tusimamie hili suala la kuhakikisha kwamba tunapeleka mamlaka na nguvu kubwa ili sera hii na sheria ianzishwe na tuweze kupata matokeo makubwa. Nina imani kubwa katika kipindi hiki cha Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na Profesa Shemdoe, ninafikiri Profesa Shemdoe ni mmoja kati ya Watanzania waliopata bahati ya kuijua sana TAMISEMI na inawezekana kutoka uhuru sidhani kama kuna mtu anaijua TAMISEMI kumzidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa amekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri, Profesa amekuwa Katibu Tawala wa Mkoa, Profesa amekuwa Katibu Mkuu wa TAMISEMI na sasa amekuwa Waziri. Ninadhani hiki ni kipindi kizuri cha kuweza kusimamia hayo mabadiliko na sisi tuna imani kubwa sana na hawa viongozi wa TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninalotaka kuchangia ni suala la 10%. Suala la 10% siku za nyuma lilikuwa linafanywa kwa utashi wa halmashauri, lakini mwaka 2018 ilianzishwa sheria na sasa hivi kupeleka michango ya 105 ni takwa la kisheria. Hata hivyo, ninataka niseme katika jambo hilo sasa hivi utoaji wa mikopo unafanyika kwa kutumia mfumo. Kuna maendeleo makubwa na tija imepatikana ila katika maeneo machache katika suala hilo la utoaji mwa 10% zipo dosari na changamoto ambazo ningependa kuzichangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, muda wa utoaji wa mikopo siku 90, siku 90 kutoa mikopo ni muda mrefu sana, ningeomba watendaji wa TAMISEMI waliangalie jambo hili. Hawa akinamama ntilie, hawa vijana wengine miradi yao waliyoipeleka ni ya msimu, mtu anataka kununua mahindi, anataka kununua mpunga siku 90 inawezekana hata andiko lake linakuwa

limepoteza maana. Kwa hiyo, wangeweza kuona ni namna gani wanaweza wakapunguza siku ili kuweza kuleta tija ya hii mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni vizuri kwamba wanatoa mafunzo, lakini changamoto iliyopo hawa wanaotoa mafunzo wanawaita wajasiriamali kwenda halmashauri na inawezekana wajasiriamali wakaitwa zaidi ya mara nne mpaka mara tano na kama tunavyojua wanatumia fedha. Sasa hawa watu kwa kuwaita mara nyingi namna hiyo na fedha wanazokopa mara nyingine unakuta hata ile fedha wanayowakopesha inaanza kupoteza tija kwa kuwa inajifidia katika zile nauli wanazolipia. Kwa hiyo, ningeshauri TAMISEMI waone njia bora ya watumishi wa TAMISEMI ikiwezekana wawafuate wajasiriamali hao kwa makundi aidha kwenye tarafa au kwenye kata ili kuweza kuokoa huu usumbufu wa kwenda na kurudi na kutumia gharama kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninashauri TAMISEMI waone njia bora ya watumishi wa TAMISEMI ikiwezekana wawafuate wajasiriamali hao kwa makundi, *either* kwenye tarafa au kwenye kata ili kuweza kuokoa huu usumbufu wa kwenda na kurudi na kutumia gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika 10% kuna changamoto ipo katika zile halmashauri 10 ambazo ni *pilot*, tulizosema benki zikopeshe. Kwa kweli tu-*declare* kwamba benki zimeshindwa kufanya hii kazi. Sababu ya Serikali kusema tutoe hizi 10% ni kwa sababu watu wengi wanaopata hii mikopo walikuwa hawana sifa ambazo benki wanazitambua ili waweze kuwakopesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii unashangaa kwamba halmashauri zinawa-*asses* watu wanasema wanastahili kupewa mikopo, wakienda benki, benki wanasema hawastahili kupata mikopo. Hili jambo limeleta usumbufu mkubwa sana kwa wenzetu hawa wa kwenye majiji na zile halmashauri 10 ambazo zimekuwa sehemu ya *pilot*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha jambo hilo hizi fedha zinazopelekwa kwenye benki maana yake ni kwamba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ni kengele ya pili, malizia hiyo *point* uliyoanza

**MHE. LUTENGANO G. MWALWIBA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba hizi fedha zinazopelekwa kwenye benki, benki zile ni kama tunazikopesha fedha kwa sababu wanapewa zile fedha halafu wanaendelea kukaa nazo wakati wale watu wanapokwenda wanasema hawana sifa za kukopeshwa na zile fedha wanazo. Sasa hili si lengo la kuanzisha mikopo ya 10%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia mchango huo, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, atafuatiwa na Moses Ludovico Kaegele na Mheshimiwa Said Ali Mbarouk ajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nimeupitia mpango huu wa hotuba ya Waziri Mkuu, ni mpango mzuri unaolenga kuboresha hali ya uchumi ya wananchi wa Tanzania na hatimaye kuwa na maisha bora kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia azma hiyo kuna vipaumbele ambavyo itabidi tuvishughulikie angalau tufikie uchumi ulio bora na wananchi wa Tanzania wawe na maisha bora (lishe bora, makazi bora na matibabu bora). Kwa mfano kichochea uchumi mojawapo ni barabara. Barabara hasa kwa neema hizi za mvua, nikitolea mfano, Mkoa wa Manyara, barabara za Mkoa wa Manyara ni mbovu nyingi, barabara ya kuunganisha mkoa na mikoa mingine, wilaya barabara za vijijini, barabara zina mashimo; makalvati na vivuko vingi vimekatika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Manyara ni Mkoa wenye fursa nyingi sana. Unaweza ukasema hata Wilaya ya Kiteto inatosha kulisha Tanzania nzima kwa mahindi, lakini ni Mkoa ambao huwezi kushawishi wawekezaji wakaja. Manyara imekuwa *marginalize,* wawekezaji wengi utawasikia wako Pwani na sehemu nyingine. Ninaomba Mkoa wa Manyara utazamwe kwa jicho muhimu kabisa kuifungua kwa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara muhimu za Manyara; kwa mfano Barabara ya Karatu - Mbulu kilometa 76, hicho kipande ni muhimu sana. Wananchi wa Mbulu wanategemea soko la mazao yao kwenda Arusha na sehemu nyingine hata nje ya nchi na Kenya, lakini barabara yao muhimu ni Barabara ya Mbulu - Karatu. Barabara iko kwenye Ilani ni kipande kidogo cha kilometa 76, lakini unaweza ukakesha siku nzima usivuke hapo. Barabara nyingine ni ya Mbulu - Garbabi kilometa 25. Tunaomba Serikali imwezeshe yule mkandarasi pale barabara ikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Wilaya za Simanjiro na Kiteto kutokana na jiografia zinaonekana ziko pembeni na hazifikiki. Kuna barabara muhimu ambayo siku zote iko kwenye Ilani, barabara inayotoka Arusha inapita Simanjiro - Kibaya kuingia Kongwa kilometa 453. Ninashukuru sana hata Waziri Mkuu alipita hii barabara, lakini ni barabara muhimu sana kuifungua Simanjiro yenye fursa nyingi pamoja na Kiteto. Tunaomba Serikali iangalie hiyo barabara na kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijua kwamba barabara ni muhimu; kwa mfano mtu wa Simanjiro pale akitaka kwenda makao makuu wilayani, mtu wa Kata ya Ngorika, Msitu wa Tembo inabidi aende Kilimanjaro, aje Arusha ndiyo aje Babati. Kwa ajili hiyo kuna umuhimu sana wa barabara inayotoka Babati kupitia Galapo kwenda Orkesumet au kwenda Kibaya kuwasaidia. Mtu anayetoka Kibaya inabidi azunguke Kondoa. Kwa hiyo, hali ya Mkoa Kilimanjaro ni ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe ushauri tu kwamba tunaomba mkoa ufunguliwe ni mkoa *potential* sana, lakini kwa

barabara za vijiji wenzangu wamesema, tunaomba *TARURA* iongezewe fedha ili *at least* kusaidia hii hali ngumu ya barabara katika Mkoa wa Manyara na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ni kwenye ardhi. Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere alisema ili nchi iendelee inahitaji mambo manne: mojawapo ni ardhi, nyingine ni watu, siasa safi na uongozi. Hakuna uwekezaji unaoweza kufanywa nje ya ardhi, huwezi ukafanya uwekezaji hewani. Ardhi ni jambo muhimu sana, lakini ni Tanzania pekee ambayo kila mtu ana uwezo wa kumiliki ardhi kwa kiasi anachotaka, maadam ana uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kumekuwa na tabia ya kasi kubwa sana ya kuvamia maeneo ya wazi, milima, vyanzo vya maji, maeneo ya uwekezaji na maeneo ya taasisi. Kuna mgogoro mkubwa sana wa ardhi katika Mkoa wa Manyara, ambao mgogoro huu unawanyima amani watu na nafasi ya kufanya kazi. Ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu itakuwa ni shahidi. Watu wengi waliokuwa wanajaa kwenye mikutano yake, wengi walikuwa na migogoro ya ardhi. Wengi karibu zaidi ya nusu ya wanaokuja (mafuriko yale) kwenye mkutano, karibu wote walikuwa na migogoro ya ardhi na migogoro hii imefanya hata nafasi ya ma-*DC* karibu wote katika Mkoa wa Manyara kushughulikia migogoro ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *DC* Mbulu, Kiteto, Simanjiro, Babati, Hanang, kila siku ni ku-*solve* migogoro badala ya kwenda kufanya shughuli zingine. Ninafikiri migogoro hii ifanyiwe kitu muhimu sana. Tena kwa nafasi ya pekee ninawapogeza sana: *DC* mwanamke wa Hanang na *DC* mwanamke wa Babati, wanafanya kazi kubwa sana kwenye kusuluhisha migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hii migogoro mingi inasababishwa na wawekezaji. Kwa mfano, jana wameuliza swali la *Ngano Limited*. Pori liko pale wananchi wananung'unika, ni kwa nini yule bwana? Ni kwa sababu anaweza kulipia hilo eneo na haendelezi hiyo sehemu. Lazima tuangalie ni vitu gani vinapaswa kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wa madini wamesababisha migogoro mingi. Hivi kwa nini mchimbaji anapewa leseni ya kwenda kuchimba bila kuelewana na yule mwenye eneo? Kwa kweli imekua ni *survival for the fittest*. Mtu anapata leseni yake ya kuchimba madini anaenda kwenye eneo bila kuelewana na yule mmiliki wa pale. Mwisho wa siku anasema anakufidia eneo hili kulingana na bei ya soko ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijijini au sehemu ya pembeni utakuta eka moja ni 400,000, haizidi milioni. Wakati yeye akienda kuchimba madini anapata zaidi ya bilioni moja. Hili jambo ni gumu sana kama ni sheria inatakiwa iletwe, mwekezaji yeyote kabla hajapata leseni, ni kwa nini kwanza Wizara hiyo isijiridhishe kwanza kwamba kweli ana eneo ambalo analimiliki kihalali, ndiyo ambapo apewe leseni, kwa sababu imekuwa sehemu ya migogoro mingi, pamoja na viongozi wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wenyeviti wa vijiji wamepewa uwezo wa kuweza kuuza mpaka eka 50, lakini mambo haya yaangaliwe upya na Watendaji wa Serikali. Unakuta ploti moja ina wamiliki zaidi ya wawili, watatu. Kwa hiyo, kuna mambo mengi sana yanachochea migogoro ya ardhi, lakini migogoro ya ardhi imekuwa ni changamoto watu wanapigana, wakulima na wafugaji, mtu na mtu. Hebu Serikali ione inafanyaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri nini kifanyike. Kitu cha kwanza ninaomba Serikali yetu sasa ione kipaumbele cha kufanya mipango ya matumizi bora ya ardhi. Kwa sababu tunavyoenda, kila mtu akijimilikisha eneo lake, iko siku tutakosa maeneo ya malisho ya mifugo (*grazing area)* tena zile ambazo ni *communal*. Hata ile *stock route* ya mifugo kupita itakuwa ni changamoto. Kwa hiyo migogoro itaendelea kuongezeka. Kwa hiyo, hili suala la kupima matumizi bora ya ardhi hata maeneo ya vijijini ambavyo bado *at least* kuna maeneo wazi, ninaomba Serikali izingatie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, mamlaka ya kupima mji ni mamlaka ya mkurugenzi, lakini mkurugenzi anapanga mamlaka

na nani? Utaangalia watumishi wengi wa ardhi hawako kwa mkurugenzi; Maafisa Ardhi, ma-*surveyor,* hawako kwa mkurugenzi, ndiyo maana unaona hii miji midogo midogo inayochipua ilikuwa kijiwe baadaye ni mji mdogo unakuta ni *squatters* ni *slum* kwa sababu kila mtu anavamia anavyotaka. Nchi yetu siku moja itakuja kuwa ni nchi ya ajabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nisisitize kabisa, kwanza mamlaka ya kupima mipango miji ni ya mkurugenzi; watumishi wote ikibidi warudishwe kwa mkurugenzi kwa sababu ardhi iko kwa mkurugenzi iko kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa mwisho ni kwenye sekta za uwekezaji nikisemea kilimo na mifugo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha, malizia.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaiomba Serikali, kwa sababu hizi pembejeo zimetolewa kwa ruzuku, basi Serikali iweke kipaumbele cha kuwalipa wale wazabuni waliotoa ruzuku ya pembejeo ili kwa msimu tunaoenda waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Moses Ludovico Kaegele, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Ali Mbarouk na Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele ajiandae.

**MHE. MOSES L. KAEGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyoitoa. Nianze kwanza kwa kuipongeza Serikali kwa namna ambavyo imewasilisha hotuba hii. Ni hotuba ambayo inalenga kukuza uchumi jumuishi, lakini pia kuboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninajua alifanya ziara ndani ya Jimbo la Nkansi Kusini na kwa upendo wake na kwa jicho la huruma alilokuwa nalo yeye aliamua kutoa ahadi ya kutoa shilingi milioni 500 kwa ajili ya kujenga barabara ya kwenda kwenye kituo cha afya ambacho kimsingi kilikuwa hakifikiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Nkansi Kusini na hususan kwenye Kata ya Nkandasi, wanatamani sana kuona pesa hiyo inaenda haraka sana ili waendelee kutabasamu kwa kadiri ambayo Mheshimiwa Rais anavyotaka wananchi wake waweze kutabasamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwenye Wizara ya TAMISEMI na nitaanza moja kwa moja na *TARURA*. Kwanza niipongeze Serikali kwa namna ambavyo imeongeza bajeti hadi shilingi trilioni 1.2. Ukiangalia wakati nipo kwenye majadiliano kwenye Kamati ya TAMISEMI, unaona *TARURA* wana vyanzo vitatu vya fedha: tozo, *Road Fund* pamoja na shilingi milioni 500 ya jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwamba kwenye tozo pesa itakwenda moja kwa moja kwenye Mfuko wa *TARURA*. Hata hivyi, ninashauri, ni lazima hii shilingi milioni 500 itafutiwe chanzo maalum, hicho chanzo kama ni madini sawa, au chochote kile, ili hiyo fedha nayo iende moja kwa moja kwenye Mfuko wa *TARURA* na kutunisha Mfuko wa *TARURA*. Jambo hili litapelekea barabara zetu hizi zipate tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Nkasi Kusini hadi sasa tarafa moja haiingiliki. Barabara ya kutoka Mpembe hadi Kitosi haipitiki, ukiangalia Barabara kutoka Ninde hadi Namanyere haipitiki. Barabara ya kutoka Kala hadi Sintali haipitiki na ukiangalia chanzo kikubwa ni kwamba bado *TARURA* hawana fedha ya kutosha. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais alivyoahidi kuongeza bajeti ameongeza, ninatamani sana kuona hii fedha yote hata hiyo milioni 500 inaenda moja kwa moja kwenye Mfuko wa *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme TAMISEMI wanafanya kazi kubwa sana na niombe kwenye suala la afya pia, ndani ya Jimbo la Nkasi Kusini tunavyo vituo vya afya sita ambavyo kimsingi Serikali ilitoa milioni 500, milioni 300, bilioni moja, vilivyo vingi bado havijakamilika na hasa Kituo cha Afya cha Kate na cha Chala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki Kituo cha Afya cha Kate ndiyo Makao Makuu ya Tarafa, kinalisha zaidi ya kata tano, lakini shilingi milioni 500 kweli imetumika na milioni 300 imenunua vifaatiba, lakini ukiangalia bado kuna miundombinu ya majengo haijakamilika. Vifaatiba vile havifanyi kazi. Ninaendelea kuwaomba ndugu zangu watu wa TAMISEMI tuhakikishe kwamba kweli fedha inayotolewa katika mwaka unaokuja ili vituo vya afya hivi ndani ya Jimbo la Nkasi Kusini viweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala la kilimo. Mkoa wa Rukwa tunategemea sana kilimo na wananchi hawa kilimo kwao ni biashara na hasa zao la mahindi. Niiombe Serikali hasa Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Viwanda itafakari namna ya kuanzisha kiwanda cha kuzalisha vifungashio vya mazao yetu. Kiwanda hicho kianzishwe ndani ya Mkoa wa Rukwa, kwa sababu tunajua Mkoa wa Rukwa uko kwenye tano bora ya mikoa ambayo inazalisha sana mahindi, ili wananchi hawa waweze kuhifadhi mazao yao wapambane na njaa, inawezekana kuanzisha kiwanda hicho tukapata hata mifuko ya kinga njaa kwa bei ya shilingi 2,000 au 2,500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kuwezesha nchi hii, hawa wakulima ambao wanazalisha sana waweze kuhifadhi chakula chao kwa muda mrefu hasa kipindi ambacho kimsingi wamepata mavuno mengi sana. Tunaipongeza Serikali kwamba mwaka huu imetoa sana ruzuku kwenye mbolea, ruzuku kwenye mbegu na wananchi wamelima sana. Niendelee kuishauri Serikali yetu ina vyombo imara sana kwa usalama. Tudhibiti uuzaji wa mbegu, mbegu ambazo ni feki, lakini tudhibiti uuzaji wa mbolea ambazo ni feki. Mambo haya yanauumiza sana wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa kwamba Serikali yetu chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, inaweza

kabisa kudhibiti na hawa mawakala wachukuliwe hatua, ili kuwawezesha wananchi hawa waendelee kupata tabasamu kupitia shughuli yetu hii ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la mikopo ya 10%, kwanza ninaipongeza Serikali kwa kuisimamia halmashauri, na halmashauri imeendelea kutenga hiyo fedha. Ukiangalia lengo kubwa ni kuwezesha vijana waweze kujiajiri. Katika jambo hili naomba nishauri mambo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kuna kila sababu Wizara ya Elimu, Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Vijana wakae chini watafakari namna ya kuanzisha somo la elimu ya fedha ndani ya nchi yetu. Nimefanya utafiti mdogo hapa, yaani tunaulizana Wabunge hapa, hata sisi wenyewe Wabunge, uwezo wa kutenga bajeti, ukajua mwaka jana ulitumia shilingi ngapi kwenye chakula na mavazi, ni kazi ngumu sana. Je, vijana wetu hawa ambao hawana elimu ya fedha watawezaje kuendesha ujasiriamali kama hawana elimu ya fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ninatamani kuona Serikali inakuja na somo la elimu ya fedha rasmi kwenye mfumo wa elimu, ili vijana wafundishwe kuanzia darasa la awali hadi chuo kikuu. Tuwe na uwezo wa kupanga bajeti, tuwe na uwezo wa kuandika *proposal* za biashara, tuwe na uwezo pia wa kuendesha maisha yetu kwa mpangilio rasmi. Ni kazi ngumu sana kwa hawa vijana, kimsingi ametoka *form four* hajawahi kufanya biashara, tunampa milioni tano akafanye biashara, ndiyo maana waliyo wengi vijana wanakataa mikopo wanaamini kwamba watafungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kila sababu ya kuanzisha somo la elimu ya fedha rasmi kwenye mfumo wetu wa elimu ili vijana wengi wanapomaliza *form four*, au darasa la saba waweze kuendesha maisha yao. Maana ninaamini kwamba ili Taifa liweze kuwa imara lazima tuwe na wafanyabiashara wengi sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa mujibu wa mtaala mpya kuanzia mwaka jana tumeanza kufundishwa elimu ya ujasiriamali kuanzia shule ya msingi na mwaka huu imeanza kuanzia sekondari. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaegele unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. MOSES L. KAEGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea. Ninaendelea kusisitiza kwamba jambo hilo lazima tuwekee mkazo mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la elimu ya uzalendo, tunahangaika sana, nikiwa *DC* nimehangaika sana kusimamia watumishi. Kwanza watu wengi hawajui hata umuhimu wa kufia nchi yao, hawako tayari kupambania nchi yao, kwa sababu sisi vijana ni wapi ambapo tunasoma elimu ya uzalendo. Ninaishauri Serikali, Wizara ya Elimu iendelee kutafakari namna ya kuanzisha elimu ya uzalendo kuanzia shule ya msingi hadi vyuo vikuu, ili tuandae jamii ambayo iko tayari kufia Taifa hili. Nje na hapo tutaendelea kuhangaika na watumishi kuwasimamia na tutaendelea kuwa na watu ambao siyo wazalendo na watu ambao wako tayari kuhujumu miradi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuchangia kwenye suala la Mfumo wa *NeST*. Kwanza ninaiunga mkono Serikali na kuipongeza Serikali kwa namna ambavyo imeanzisha huu Mfumo, ni muhimu sana. Niendelee kuishauri Serikali, *PPRA* waendelea kutoa elimu siyo tu halmashauri lakini kwa Maafisa Tarafa, kwa Watendaji wa Kata, lakini pia na kwa Watendaji wa Vijiji. Kwa dakika moja, niendelee kuiomba Serikali isimamie sana uadilifu wa watu wanaosimamia Mifumo ya *NeST*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashtua sana kama kwenye mkoa X, Mfumo wa *NeST* umeruhusu, mkandarasi mmoja afanye miradi mitano yenye thamani ya bilioni 27, jambo hili inasababisha

wananchi wengine, wawe na chuki, lakini wananchi wengine waone kwamba kuna watu wanaopendelewa. Hata kama mkandarasi yule ana viwango vya hali ya juu sana, kuna umuhimu wa kusimamia vizuri sana maadili ya wasimamizi wa Mfumo wa *NeST* ili wananchi hawa wa Tanzania, tuweze kula keki sawa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Said Ali Mbarouk, atafuatiwa na Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele, Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis ajiandae.

**MHE. SAID ALI MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Ninaomba uridhike kwa kuanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kueleza machache kuhusiana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakishukuru Chama changu cha *ACT* Wazalendo kwa kunisaidia kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, lakini pia, ninawashukuru Mheshimiwa Spika na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuniteua kuwa Mheshimiwa Mbunge katika Bunge hili Tukufu. Ninaomba nianze na suala la utawala bora; katika Kifungu cha Katiba, Ibara ya 14, ninaomba ninukuu kwamba: "Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa Sheria."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 15 inazungumza kwamba, "kila mtu anayo haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru".

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, "Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kuwa huru na kuishi kwa uhuru itakuwa ni marufuku kwa mtu yoyote kukamatwa, kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake vinginevyo isipokuwa tu -

(a) Katika hali na kufuata utaratibu uliowekwa na sheria au

(b) Katika kutekeleza hukumu amri au adhabu iliyotolewa na Mahakama kutokana na shauri au na mtu kutiwa hatiani kwa kosa la jinai". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza na vifungu hivi vya Katiba, Ibara hizi kwamba, kuna zoezi ambalo linaendelea katika Wilaya ninayoishi ya Wete Mkoani Kaskazini Pemba watu kushikwa, kufungiwa na kutokomezwa hadi hivi ninavyozungumza nina majina ya watu wanne, Faki Ally Salim wa Shehiya ya Ukumvi, Wilaya ya Wete; Haji Omar Saidi wa Shehiya ya Bopwe, Wilaya ya Wete; Yaya Mohamed Salum wa Shehiya ya Kambini, Wilaya ya Wete; na Juma Salim Juma wa Shehiya ya Kambini, Wilaya ya Wete. Hawa wameacha watoto 21 wadogo, hawana watu wa kuwashughulikia na jamaa wakienda Polisi Wete kuulizia majaliwa ya hawa, polisi hawana jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili ni tatizo kubwa katika nchi, hatuwezi kuendesha nchi katika hali hii. Sisi, kama Waheshimiwa Wabunge, kama viongozi, ni lazima kuwe na majibu mtu akitoweka tu kwamba, hakuna linalojulikana kuhusu majaliwa yake! Kwa kweli, ni tatizo. Kwa hivyo, ninaomba sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu hili ni lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, polisi ni chombo cha Muungano ambacho kinapaswa kuhakikisha kwamba, masuala haya yanafanyiwa kazi na wananchi wanapata majibu ya maswahibu ya jamaa zao. Haiwezekani hata kidogo tuendelee kufanya mambo mengine na hatujui nani kesho atakamatwa, atafichwa; watu wana uwoga kufanya shughuli zao za kimaisha kwa sababu, hawajui ni nini kitatokea? Nani baada ya yule wa jana? Nani baada ya wa kesho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli hili ni jambo ambalo linahuzunisha na sisi, kama Waheshimiwa Wabunge, hili liwe ni jambo mtambuka, li-*cross* maeneo yetu ya uwakilishi. Tukisikia kuna maeneo mambo haya yanafanyika kwa kweli, lazima tuiambie Serikali kwamba, kuna jambo la kulishughulikia tena kwa

dharura. Hili jambo linasikitisha sana na linatia unyonge kwa sababu, pia, mtu anaenda zake kuvua, hajui kama atarudi salama nyumbani au ndiyo anawaacha watoto nyumbani. Mtu anaenda zake gereji kufanya shughuli za ufundi, hajui kama atarudi salama nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nadhani, imani yangu na imani ya watu wengi, nina hakika Mheshimiwa Mama Samia hili halijui na wala hajaliamrisha. Nina hakika Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Nchimbi, hili halijui na hajaliamrisha. Nina hakika Mheshimiwa Waziri Mkuu hili halijui na hajaliamrisha. Nina hakika Mheshimiwa Dkt. Hussein hili halijui na hajaliamrisha, lakini kuna watu katikati wanajaribu kumharibia mama, sasa hatuwezi, sisi kama Wabunge, kuliacha hili na watu wakaanza kumlaumu mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu katikati hapo, nadhani kuna jambo la kulishughulikia. Kwa hivyo, ninamwomba sana ndugu yangu Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili suala alifuatilie na ni vizuri tukapata Kauli ya Serikali kuhusiana na suala hili. Kama mtu anatuhumiwa na jambo lolote Serikali ina nafasi ya kumshughulikia, kumkamata na kama amekuwa-*retained* tukajua amekuwa *retained* wapi na kwa muda gani, lakini mtu kutoweka tu mwaka, miezi sita na hatujui hatima yake kwa kweli, hili jambo tulifanyie utaratibu wa kulishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninaomba nilizungumze katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, *paragraph* ya 34 na 35, amezungumza kuhusu mapato ni jambo zuri, ninaipongeza Serikali kwa hili. Kuna trilioni kama 26.63 na katika hizo msaada kutoka nje ni shilingi bilioni 754, sawa na 3.41%, hili ni jambo zuri. Kwamba, tunajaribu kutafuta fedha kwa vyanzo vyetu vya ndani bila kutegemea misaada kutoka nje, hili ni jambo zuri, ninaiomba Serikali hilo liendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nina jambo ambalo ni la Kikatiba pia, kwamba, Ibara ya 133/134. Naomba ninukuu hii ya 134 –

(1) "Kutakuwa na Tume ya Pamoja ya Fedha yenye wajumbe wasiozidi saba ambao watateuliwa na Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa ibara hii na masharti na sheria iliyotungwa na Bunge."

(2) Majukumu ya Tume yatakuwa ni:

(a) kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na, au yanayohusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgawo wa kila mojawapo ya Serikali hizo;

(b) kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha wa Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha katika Serikali mbili".

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa kunukuu. Ninaomba kufahamu kutoka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbarouk muda wako umeisha. Malizia.

**MHE. SAID ALI MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo ninamalizia.

**MWENYEKITI:** Malizia, unga mkono hoja.

**MHE. SAID ALI MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba suala hili kutoka Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe. Hili suala ni la muda mrefu, sijasikia limefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka 2006 mpaka 2026 mfuko huu haujaundwa rasmi na kwamba, baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wakilishi, nikiwemo mimi kuwa na imani kwamba, Mfuko huu utaundwa vizuri, utasimamiwa vizuri, mapato yanayotokana na Muungano na matumizi yake kwa shughuli za

Muungano, basi itabaki bakaa ambayo itagawanywa kwa matumizi ya Serikali mbili. Sasa muda wa miaka 20...

**MWENYEKITI:** Ninaomba umalizie.

**MHE. SAID ALI MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana nipate majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Bahati nzuri alikuwa Waziri wa Fedha, suala hili lilianza vipi na limemalizika vipi? Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninamwita sasa Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele. Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo ajiandae.

**MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa ninachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, ambaye amenijalia kuwa na pumzi hadi muda huu na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu. Pia, ninakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili niwe mmoja kati ya wachangiaji wa jioni hii ya leo katika kuchangia hotuba iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa Uongozi wake imara ambao unaonesha dira na dhamira ya dhati katika kututumikia sisi wananchi wa Tanzania na kutuletea maendeleo. Sote ni mashahidi, tumeshuhudia kazi kubwa ambayo imetekelezwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo basi tuna kila sababu ya kumsifu na kumpongeza kwa hatua kubwa ya maendeleo ambayo ametufikisha kupitia sekta mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitauelekeza moja kwa moja katika mambo mawili. Jambo la mwanzo, ninaelekea katika 10% ambayo inatengwa katika halmashauri zetu kupitia mapato ya ndani ya halmashauri. Serikali imeanzisha mikopo hii ya 10% kwa lengo la kuwakwamua vijana, wanawake na watu wenye ulemavu; mikopo hii imewekewa Sheria, lakini pia,

imetengenezewa miongozo mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha haki inawafikia makundi yote kwa utaratibu ambao umewekwa kuwawezesha wanufaika waweze kupata fursa hii, ili kujiendeleza kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya miongozo mbalimbali kufanyiwa marekebisho, kufuatia changamoto iliyojitokeza hapo nyuma kutokana na mikopo hii, kuna baadhi ya halmashauri wameshindwa kupeleka fedha hizi moja kwa moja katika makundi haya, hususan kundi la watu wenye ulemavu. Wachangiaji wengi wamezungumzia hapa suala hili, kwa kipindi cha 2025/2026 halmashauri nyingi nchini zimeshindwa kutenga hizi fedha, hasa kwa upande kwa watu wenye ulemavu, kwa visingizio vya kwamba hakuna vikundi vya watu wenye ulemavu vilivyojitokeza katika halmashauri. Kisingizio ni kwamba, waliojitokeza kuomba hawakuwa na vigezo vya kupewa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliamua kuweka makundi haya tofauti tofauti kwa kuwa, inaelewa kwamba, kuna watu wenye ulemavu wanawake na kuna watu wenye ulemavu vijana, lakini hawakuishia hapo, wakasema kundi maalum litengwe kwa watu wenye ulemavu kutokana na umahsusi wa mahitaji yao. Leo kundi hili liliwekwa hivi kutokana na kwamba, huko nyuma walikuwa wanasahaulika kupitia fursa mbalimbali zinatolewa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kupitia asilimia mbili hii waliyotenga ilikuwa ni mkombozi pekee wa kuwafanya watu wenye ulemavu, kwanza waweze kupata haki yao hii, lakini pia, waweze kujiendeleza kiuchumi na wao wapate maisha bora kama walivyo watu wengine. Kama watu wenye ulemavu wameonekana hawana uwezo wa kurejesha mikopo au kama hawakujitokeza, hapa pana shida na kwanza ni aidha, hawajaelimishwa, lakini cha pili, hawajapewa kipaumbele cha kuhakikisha kwamba, hawa watu nao hii fursa wanaipata na wanaitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, ninahisi na ninashauri tusiishie hapo na kuna maelekezo yametoka kwamba, kundi ambalo limeshindwa kuchukua mkopo ambao wametengewa,

basi fedha ile ipelekwe kwenye kundi lingine. Hii ninaona siyo sahihi, wataturudisha kulekule tulikotoka ambapo, kundi la watu wenye ulemavu lilikuwa linasahauliwa kutokana na mtazamo wa jamii; kama hawajajitokeza basi hawajapata elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, Serikali ihakikishe inatenga fedha maalum ya kuhakikisha inatoa elimu kwa jamii, hasa kundi la watu wenye ulemavu, waweze kuelewa fursa ambazo zipo, kwa ajili yao na waweze kuchukua mkopo, lakini baada ya kupata elimu, wataweza kuchukua mikopo vizuri, wataweza kuitumia vizuri na watarejesha marejesho vizuri. Watu wenye ulemavu na wasio na ulemavu watakapokwenda kuomba, wasipewe mkopo mpaka wapewe mafunzo kwanza; wakishapewa mafunzo wataelimika, watachukua mkopo na watarejesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ninagusia sekta ya elimu. Kwanza kabisa ninaipongeza Serikali, imefanya jitihada kubwa ya kuwekeza katika elimu, tumeshuhudia takribani shule 26 za sekondari zimejengwa Tanzania hii, za wasichana. Hii ni hatua kubwa ya maendeleo. Hatua hii itakwenda kusaidia kumkomboa mtoto wa kike, lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umekwisha, malizia.

**MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ushauri wangu ni, ninaomba uridhie, kuna walimu wenye ulemavu ambao wana mahitaji makubwa zaidi, hawa watengewe bajeti ya kupatiwa mafunzo ili na wao waweze kufundisha, waende na kasi ya ufundishaji wa sasa. Kutokana na mahitaji makubwa ya wanafunzi wenye ulemavu na watoto wengi walio katika mikoa yetu wana ulemavu, ninaishauri Serikali ifanye jitihada watenge fedha, kwa ajili ya kujenga shule; angalau kila mkoa wajenge shule moja ambayo itachukua wanafunzi wenye ulemavu kwa mujibu wa mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele, atafuatiwa na Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo na Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala ajiandae.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetujalia afya njema ya kuwepo hapa siku ya leo. Pia, ninampongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa hatua kubwa anazozichukua katika kudhibiti hali ya ukosefu wa mafuta katika dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri sana anayoifanya hapa nchini. Sisi sote ni mashahidi kwa kazi anazozifanya, hasa anaposafiri katika mikoa mbalimbali. Ninaomba nichangie maeneo kama matatu hivi kwa kifupi; kwanza kabisa, kabla sijalitaja hili ninalotaka kusema, kwa mara ya kwanza ninaipongeza sana Serikali kwa kuimarisha huduma ya maji katika nchi yetu, ingawa yapo baadhi ya maeneo bado huduma hii haijawa ya kuridhisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma hii nzuri ya maji imesababisha changamoto katika baadhi ya miji nchini, changamoto ya udhibiti wa majitaka. Katika Jiji la Dodoma, wote tunafahamu Jiji la Dodoma linazidi kukua, linazidi kujengeka, watu wanazidi kuingia katika Jiji la Dodoma, lakini mifumo ya majitaka katika kata za katikati ya mji imeshindwa kuendana na idadi ya watu waliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo kata nitazitaja za katikati ya mji, Kata za Majengo, Uhuru, Madukani, Hazina, Kilimani, Chamwino, Kizota, Nzuguni, Makole, Viwandani; hizi ni baadhi ya kata za katikati ya Jiji la Dodoma ambazo zimekumbwa na tatizo la uondoaji wa majitaka kwa sababu, mfumo uliopo ni mdogo, umeshindwa kuendana na hali ya sasa ya wingi wa watu katika Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kwamba, katika bajeti hii basi Serikali iangalie namna ya kuondoa tatizo hili. Kwa hapa Dodoma uko mradi ambao tumeupata, kama nchi, kutoka kwa

Serikali ya Korea, mradi wenye thamani ya dola milioni 700 ambao mpaka sasa hivi bado haujaanza kuwekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni mkubwa, tumeambiwa kwamba mkandarasi alipatikana lakini alikuwa na kasoro anatafutwa mkandarasi mwingine. Tunashauri mkandarasi huyu atafutwe haraka huu mfumo wa majitaka uweze kutengenezwa na kuleta nafuu katika mitaa hii. Ukipita katika mitaa hii na kwa wanaotembea Dodoma utakuta kwa kweli kuna mitaa harufu ni kali sana ya majitaka, ni muhimu suala hili likatafutiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni suala la Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Serikali za Vijiji katika nchi yetu. Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Vijiji ndiyo mhimili wa Serikali, ndiyo viongozi wanaoishi na watu ndiyo viongozi wanaobeba mizigo yote ya changamoto katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi hawa wa Serikali za Mitaa na Vijiji ndiyo wenye *register* ya wakazi, ndiyo wanaodhibiti wahamiaji haramu, ndiyo wanaoshughulika na wahalifu kule vijijini, kwa sababu vijiji vyetu vilivyo vingi havina vituo vya polisi, kwa hiyo kwa namna moja ama nyingine nyumba za hao Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji zinageuka kuwa mahabusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi mimi mzee wangu alishawahi kuwa Mwenyekiti ninafahamu hii hali. Watoto na familia zinashindwa kupata utulivu kwa sababu wakati mwingine inatakiwa Mwenyekiti wa Kijiji ama Mtaa aweze kuwapokea watu waliopata matatizo, migogoro ya familia, wamepigana mume na mke wameumizana, wenyeviti hawa ndiyo wanaopokea mizigo yote hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wenyeviti katika baadhi ya maeneo hawana posho ya aina yoyote wanayopata. Niseme tu kwa Jiji la Dodoma Wenyeviti hawa wanapewa shilingi 40,000 kwa mwezi. Ni pendekezo langu katika bajeti hii tushauri Halmashauri zetu, watendaji kwa maana ya Wakurugenzi wahakikishe kwamba wanakusanya mapato ya kutosha wawawekee posho

walau hata laki moja tu, kwa sababu hawa ndiyo mhimili wa Serikali katika maeneo yetu, ndiyo wanausalama wa kwanza kabisa katika nchi yetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninaomba kuongelea kuhusiana na suala la barabara. Tumeeleza umuhimu wa barabara zetu na barabara ndiyo msingi wa uchumi wa nchi yetu. Hapa Dodoma iko barabara ambayo ikitengenezwa inaweza kupunguza umbali kutoka Dodoma kwenda Mikoa ya Katavi, Songwe, Mbeya pamoja na Rukwa. Barabara hii inaanzia Bihawana, wanaoijua Iringa *Road* inaanzia Bihawana inakwenda, Bihawana ipo katika Jiji la Dodoma unakwenda katika Wilaya ya Bahi, unakwenda mpaka Sanza, unakwenda moja kwa moja unavuka mapori ya Muhesi, Kizigo pamoja na Rungwa unaenda kukutanisha njia inayotoka Itigi kwenda Makongorosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia hii kwa utafiti uliofanywa hivi karibuni ni kwamba ikijengwa itaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa safari kutoka Dar es Salaam au kutoka Dodoma kwenda Mbeya na ikawa ni kilometa 350 tu badala ya kilometa 670 ambazo tunatumia kupitia Iringa kwenda Mbeya. Barabara hii tunapendekeza ifanyiwe upembuzi yakinifu iweze kujengwa hata kama siyo kwa sasa, kwa siku zijazo. Barabara hii itakuja kusaidia kwa kiasi kikubwa sana kupunguza mizigo, kupunguza *pressure* ambayo Barabara ya Dar es Salaam – Iringa - Mbeya inaipata kwa magari mengi ambayo yanapita kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Bandari ya Dar es Salaam ilipokea mizigo yenye uzito wa tani milioni 27.8. Katika tani hizi, tani milioni tisa ilipita katika njia ya Iringa. Bandari ya Dar es Salaam pia inaendelea kupanuliwa, hivyo mzigo mkubwa sana utakuwa unapita kwenye njia hiyo. Njia hii ninayoisema iwapo Serikali itaijenga itapunguza kwa kiasi kikubwa *pressure* ambayo inaipata hii Barabara inayopita Morogoro - Iringa, kwenda Mikoa ya Mbeya na hata Nchi jirani za Zambia na *Congo*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea hapa kuhusiana na kuinua uchumi, kuimarisha uchumi, barabara hii itaimarisha

uchumi wetu. Pia katika hayo mapori kuna fursa kubwa sana za utalii kwa sababu ni maeneo ambayo wapo wanyama wengi. Hatua ya kufungua hiyo njia itapelekea kuimarisha utalii katika nchi yetu kwa wageni kutoka Dodoma na kwenda kuona wanyama katika mapori haya ya Muhesi, Kizigo pamoja na Rungwa. Kwa msingi huo mapato ya nchi yataongezeka kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo ni ushauri tu Serikali ifanye upembuzi yakinifu pamoja na njia hii inayokwenda Manyoni ambayo inaitwa Chali - Igongo - Bihawana *Junction*. Pia Serikali ianze kufikiria kuipasua hii njia kupitia haya mapori matatu kutoka Bihawana kupita Sanza kwenda Rungwa na kuelekea Mbeya kwa kilomita 350 tu badala ya kilomita 670 ambazo tunazitumia kupitia Iringa, hii itasaidia

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii itawafanya Wabunge hata waliopo humu ndani, Wabunge wa Mikoa ya Rukwa, Katavi, Mbeya pamoja na Songwe kupita hii njia badala ya kupita njia ndefu ya Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wakazi wa Mpanda, kwa Wabunge wa Mpanda waliopo hapa ni kwamba ile njia ikapasuliwa maana yake ukishafika Rungwa unakwenda Ipole, Ipole unaondoka kwenda Inyonga, Inyonga unaenda Mpanda. Njia hii itakuwa ni msaada mkubwa na itafungua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala na Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila ajiandae.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya, amani, kwani amani ndiyo tunu kubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kumshukuru na kumpongeza sana Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazozifanya. Ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anazozifanya hususan kwa kuzunguka Tanzania nzima, Mikoa yote, Wilaya na Majimbo yote. Ninamshukuru sana *RC* Nurdin Babu, Mkuu wetu wa Mkoa wa Kilimanjaro, pia ninawashukuru sana kwa kuwa nami ni mara ya kwanza kusimama katika Bunge hili Tukufu kuchangia, ninaomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Moshi Mjini kwa kuniamini na kunichagua kwa kura nyingi za kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru mke wangu mpendwa Jasmine pamoja na watoto wake kwa kunivumilia katika safari hii ya kuja hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwamba uchumi wetu umekua kwa asilimia 6.0 katika robo ya tatu ya 2025, mfumuko wa bei umesalia chini ya asilimia 3.3 na mapato ya Serikali yameongezeka kwa 103.7%. Hii inaonyesha ni jinsi gani kuelekea dira ya 2050 umeweza kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la elimu. Ninafurahi kuona ufaulu umeongezeka katika ngazi zote. Darasa la saba ufaulu umeongezeka kwa 81.30%, kidato cha nne ufaulu umeongezeka hadi 94.98% na Serikali imeajiri walimu 7,000 kuongeza ubora wa ufundishaji katika Taifa letu. Hata hivyo, katika Jimbo letu la Moshi Mjini changamoto ya nyumba za walimu, madarasa, vituo vya walimu pamoja na matundu ya vyoo ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru pia Waziri Mkuu katika ziara yake aliyekuja Mkoani Kilimanjaro alitoa tamko kwa nchi nzima na ametoa miezi sita kuhakikisha matatizo ya vyoo vyote katika mashule iwe ni historia. Amewapa Wakurugenzi maelekezo wahakikishe wanashughulikia masuala ya vyoo kutoka kwenye mapato ya halmashauri zetu. Nimpongeze sana Waziri Mkuu kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Waziri Mkuu kupitia TAMISEMI itusaidie watu wa Moshi fedha za ujenzi wa madarasa 4,193 zilizotengwa kwa halmashauri zitoke kwa wakati ili tujiandae kwa wimbi la kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza 2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masuala ya maji, ninashukuru katika Jimbo langu la Moshi Mjini suala la maji kwetu sisi limekamilika kwa 100%, vilevile ninashukuru masuala ya maji katika nchi yetu hususan vijijini yamefaulu kwa 85.2%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Waziri Mkuu kwamba na atoe maelekezo kwa Waziri wa Maji kwamba katika Jimbo letu la Moshi Mjini kuna changamoto kubwa sana ya majitaka. Kuna changamoto kubwa ya majitaka ambapo zipo kata ambazo mpaka sasa hivi hazijafikiwa kuhusu majitaka, mfumo wa majitaka na mifumo ni ya zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa ni mabao 11 kupokelea, kuchuja na kusafisha, takribani tunahitaji karibu bilioni 1.15, kwa hiyo ninamwomba Waziri Mkuu endapo tutapata hizi fedha, ninaamini kabisa nasi masuala ya mfumo wa majitaka itakuwa historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niseme kwamba Serikali ikiweza kutupatia bilioni 2.8, kuna kisima kimoja kinaitwa Mshilingi ni kisima ambacho kiko pale Moshi Mjini, kina maji mengi sana, kisima hiki kikichimbwa kwa bilioni 2.8 kitaweza kusaidia majirani zetu ili kuweza kupata maji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiongelea suala la afya katika ninampongeza Rais kwa programu yake ya *Samia Health Super Specialization Program* ambayo tayari imewawezesha wataalam 1,483 Madaktari Bingwa na ubingwa ubobezi. Kwa hiyo niombe kabisa safari hii ya hawa Madaktari tuna Hospitali yetu ya *KCMC* pale tuombe nayo ifaidike na Madaktari hawa ili kuepusha wananchi wa Kilimanjaro hususani Jimbo la Moshi kusafiri kwenda kupata matibabu Mkoani Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masuala ya miundombinu niseme kwamba nishukuru Serikali barabara za lami sasa hivi zimetengenezwa karibu kilomita takribani 4,413 na ukarabati wa barabara za vijijini umetekelezeka, lakini kwenye Jimbo la Moshi Mjini kwa kweli bado hali siyo nzuri barabara zetu nyingi tu hazina lami, barabara zina vumbi hususani Kata za Njoro, Pasua, Karanga kwa hiyo niombe kwamba watu wa *TARURA* waweze kuongezewa fedha na zile fedha za *TARURA* ziweze kwenda kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Moshi ni Makao Makuu ya Mkoa wa Kilimanjaro, Moshi mpaka sasa hivi kuna shida kubwa sana changamoto za taa za barabarani, kuna changamoto ya *traffic lights*. Sasa ukiangalia ule mji ni mji wa kimkakati, kuna mlima mkubwa pale na wageni ni wengi. Tuna takribani watu 400 kwa siku wanaingia wageni wazungu pale kutoka mataifa mbalimbali, magari pale hayapitiki, changamoto ni kubwa sana ya kwenye masuala ya miundombinu ya barabara pamoja na *traffic light*. Kwa hiyo, ninaomba *TARURA* waweze kutusaidia kuhakikisha kwamba bajeti ambayo imetengwa ya mwaka huu itoke kwa wakati na itufikie watu wa Moshi ili tuweze kutatua changamoto hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niendelee kuunga mkono wito wa Waziri Mkuu kuhusu uwajibikaji na uzalendo, watumishi wa ardhi wahakikishe wanatatua migogoro ya ardhi kwa wakati na migogoro ya ardhi kwa wakati ili kuwafanya wananchi waweze kuendeleza shughuli zao za kibiashara na uchumi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache ninaomba kuunga mkono Makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Bunge kwa mwaka wa fedha 2026/2027. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala, Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila atafuatia, Mheshimiwa Lucy Simiria Kombani ajiandae.

**MHE. FARAJI B. NANDALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Kwa sababu leo hii ni mara ya kwanza ninasimama kwenye Bunge hili kuchangia ningependa nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ndanda kwa imani kubwa waliyonipa na niwaahidi kwamba sitawaangusha nitafanya ile kazi ambayo wameniagiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutuamini vijana na mimi ni kijana, kwenye Bunge hili tuna vijana wengi na hata kwenye Baraza la Mawaziri kuna vijana wengi Rais anaupiga mwingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wote tuko humu Bungeni leo hii ili tuhakikishe kwamba tunaweza kupitisha bajeti ya Serikali ambayo ina ukomo wa zaidi ya shilingi trilioni 61.93. Hapa juzi Waziri Mkuu aliwasilisha bajeti ya Wizara yake ambayo ina ukomo wa zaidi ya trilioni 12.5 ambayo ni sawa na 20% ya Bajeti Kuu ya Serikali 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni nyingi sana. Ukubwa wa fedha hii unatokana na umuhimu wa Wizara hii na Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwenye hii Ofisi ya Waziri Mkuu ndiko ambako kwenye TAMISEMI. Nami mchango wangu leo hii ningependa sana niuelekeze kwenye TAMISEMI kwa sababu TAMISEMI ndiyo uti wa mgongo wa Taifa hili. TAMISEMI ndio kitanzi cha Wabunge wengi. TAMISEMI ndiyo tumaini la wananchi wengi.

Mheshimiwa mwenyekiti, ili tuweze kuisaidia TAMISEMI yapo mambo ya msingi ambayo kama Taifa tunabidi tutafakari. Jambo la kwanza ni namna gani tunaweza kuisaidia TAMISEMI ili iweze kufanya mambo yake ambayo wananchi saa hizi wanataka kuyasikia. Kwanza leo hii tunaona kwamba namna gani TAMISEMI imekuwa muhimu sana katika kuleta mabadiliko na maendeleo kwenye Taifa hili, lakini kutokana na ufinyu wa bajeti, TAMISEMI imeshindwa kutekeleza mambo mengi ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kama Mbunge ningeomba nishauri ili TAMISEMI iweze kufanya kazi vizuri lazima tujihakikishe kwamba tunaongeza jitihada za kukusanya mapato ili tuweze kuisaidia TAMISEMI iweze kuleta faraja kwa wananchi, njia pekee ya kuisaidia TAMISEMI kupata mapato ni kwa kwenda kuwekeza kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ndiyo uti wa mgongo na 90% ya Watanzania ni wakulima. Hatuwezi kuepuka kuwekeza kwenye kilimo, lazima tuhakikishe kwamba tunaongeza mnyororo wa thamani wa mazao yetu kuhakikisha kwamba Serikali inawekeza kwenye kilimo kwa kutafuta masoko ya mazao yetu ili tuweze kupata mapato ambayo yatakwenda TAMISEMI na kwenda kujenga barabara na kwenda kujenga hospitali na kwenda kujenga shule, lakini pia kwenda kutoa mikopo ya 10% kwa vijana wengi ambao wamekuwa wameitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua shabaha ya Serikali kufikia 2030 ni kwenda kuongeza tija kwenye kilimo kwa 10%, lakini haya yasiwe ni maneno tu lazima Serikali ione kwamba uti wa mgongo wa Taifa hili lazima uwe ni kilimo, tuwekeze kwenye kilimo ili tuweze kutoa tija ile ambayo sisi tumeikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuongeza mapato hali ya kuwa mazingira ya wakulima siyo mazuri, hivyo ni lazima kabisa tuandae mazingira mazuri kwa wakulima ili waweze kufanya vizuri. Kwa mfano, kwenye Jimbo langu la Ndanda leo hii kuna mgogoro kati ya wakulima na wafugaji, leo hii shughuli nyingi za kilimo zimesimama kule kutokana na migogoro inayoendelea kila siku ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Ndanda tumebarikiwa kupata ardhi yenye rutuba na leo hii tunategemea sana kilimo kuweze kufanya shughuli zetu, lakini shughuli za kilimo zinasimama kule Ndanda kwa sababu ya hawa Ndugu zetu wafugaji wanakuja na ng'ombe zao, wanalisha kwenye mazao yetu na kuleta vita. Badala ya kufanya shughuli za maendeleo imekuwa ni eneo la vita kila siku tunapigana, tunauana na tunashindwa ku-*concentrate* katika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali ni lazima tuje na njia muhimu ya kuondoa tatizo hili la migogoro kati ya wakulima na wafugaji ili tuweze kuleta tija ambayo inakusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ili tuweze kuisaidia TAMISEMI ni lazima tujitahidi sana kuziba mianya ya upotevu wa fedha za umma. Leo hii ukipita kwenye Halmashauri zetu fedha nyingi za umma zimekuwa zikipotea, ili tuweze kupata mapato ambayo tunaweza kwenda kutekeleza bajeti hii ni lazima tufunge mkanda tuangalie namna gani tunaweza kuziba mianya yote ya upotevu wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika sana kila siku ninapoona kuwa ripoti za *CAG* zinapokuja hapa Bungeni kutoa maagizo tunashindwa kabisa kufuatilia yale matekelezo ya *CAG*. Ni lazima tukubaliane sisi kama Taifa tuangalie tumetoka wapi, tuko wapi na tunaelekea wapi. Leo hii tunaizungumzia bajeti ya trilioni 63.39, hizi ni fedha nyingi sana. Je, tunawezaje kwenda kutekeleza bajeti hii ilihali tunaendelea kuruhusu mianya ya upotevu wa fedha nyingi za umma huko kwenye halmashauri zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali na niombe sana Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia TAMISEMI tuangalie namna bora ambayo itatusaidia sisi kama Taifa kuziba mianya yote ya upotevu wa fedha za umma, hasa kwenye mifumo ambayo inatumika kwenye kukusanya kodi na pia kudhibiti matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kwenye Taifa hili tuna mifumo mingi sana ya kukusanya kodi. Ukitaka kufanya tathmini hapa leo inafika zaidi ya mifumo 100; lakini je tumeangalia ufanisi wa hii mifumo? Mimi binafsi nimejaribu kufanya tathmini nimeona kwamba hii mifumo inaendelea kuliingizia hasara kubwa Taifa. kwa nini sisi kama Taifa tusiwe na mifumo michache ambayo itaongeza ufanisi na kuleta tija katika nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ningependa pia nichangie kuhusiana na suala la mikopo ya 10% ambayo imekuwa ni janga kubwa sana kwa Taifa hili. Kule kwangu kwenye Jimbo la Ndanda sisi Halmashauri yetu iko

mbuyuni. Mwananchi wa kawaida ili aweze kunufaika kwenye mikopo ya 10%; kwa mfano mwananchi wa Nanganga anatakiwa asafiri umbali usiopungua kilomita 96; yaani kutoka Nanganga kwenda mpaka Mbuyuni. Kwenda na kurudi ni kilomita 182.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunaambiwa ili uweze kupata mikopo hii ni zaidi ya siku 90. Ndani ya siku 90 huyu mnufaika anatakiwa akae siku 42, na ndani ya hizo ndani ya siku 42 siku sita awe anakwenda na kurudi kwenda kupata mafunzo. Gharama ya kutoka Nanganga kwenda mbuyuni kwenda tu ni shilingi 30,000 kwenda na kurudi shilingi 60,000. Hatimaye anaomba ule mkopo anapewa milioni mbili milioni tatu. Ukiangalia gharama alizotumia katika kufuatilia ule mkopo zinazidi ule mkopo aliopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema wanataka tulisaidie hili Taifa; tunawezaje kulisaidia Taifa ilihali kuna mazingira ambayo siyo rafiki? Kwa hiyo niombe na niishauri Serikali kutafuta namna ya kupunguza haya masuala, hizi siku 90, ili tuweze kuwa kuwafikia Watanzania wengi na tuweze kuwahudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilikwishamwita Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Damas Simirya Kombani na Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, ajiandae. Mheshimiwa Magangila inaonekana hayupo. Tuendelee na Mheshimiwa Lucy Simirya Kombani.

**MHE. LUCY S. KOMBANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 20262027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na leo hii nimeweza kusimama hapa. Kipekee ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa juhudi alizofanya. Si juhudi tu bali ni juhudi kubwa sana

katika kutekeleza zile ahadi zake alizoahidi ndani ya siku 100. Kubwa likiwa ni kuzindua Sera ya Bima ya Afya kwa wote pamoja na kuwapatia wananchi milioni moja laki nne na bima za afya bure kabisa, hili ni jambo kubwa sana kwa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na kuongezea kwenye suala hili la bima ya afya. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeonyesha kwamba kuna awamu inayoendelea ambayo ni ya kutibia watu wenye magonjwa sugu. Ninaomba hili zoezi liwe kwa uwazi zaidi na *speed* iongezeke. Watu wenye magonjwa sugu wapo wengi, hasa watoto. Inasikitisha zaidi kwamba wale watu wanaishia kuombewa hela mitandaoni na wakati mwingine wale watoto hata hela zile bado hazijatimia watoto wanakufa, tunawaona huko kwenye mitandao. Kwa hiyo zoezi hili litazamwe vizuri, hasa hawa watoto ambao wanabeba magonjwa makubwa mno na jinsi ya kupata hii huduma basi uwazi uongezeke ili kila mtu ajue kwamba akimwona mtu ana ugonjwa sugu kama ampeleke kwa Mkuu wa Mkoa haya, kama anampeleka kwa *DMO* aende ili aweze kutibiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ninapenda niipongeze Serikali kwa kuonelea kwamba sasa hivi wafadhili wengi wamejitoa miradi mingi imekufa, imeamua kufanya *amendment* kwenye kanuni za mafao. Kwa sasa wanachama wanaweza waka-*opt* kuchukua mafao yao yote ama kuchukua kidogo; kitu ambacho zamani ilikuwa wanachukua 33.3% tu au 50%. Kwa hiyo nipongeze Wizara ya Ajira na Vijana na tumshukuru Rais kwa kuona umuhimu wa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo ninataka kumalizia ni kuhusiana na bilioni 200 za vijana. Zile bilioni 200 za vijana siku zinakabidhiwa ile cheki iliandikwa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliichukua ile cheki akamkabidhi Waziri Mkuu na baadaye akakabidhiwa Waziri wa Vijana. Mawazo ya vijana wote zile bilioni 200 ziko Wizara ya Vijana, lakini fedha hizi zimekuja kutawanywa Wizara tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chipando alishawahi kuongea, alisema kuwa vijana hawapendi kona kona; lakini kile

kilichofanyika zile ndizo kona kona. Vijana wanalalamika, mkopo unatangazwa Wizara ya Mifugo na Kilimo unakwenda kuombewa TAMISEMI kwa Mkurugenzi baadaye nani anakuja kuwajibika na fedha hizi? Kwa hiyo inapotokea vitu kama hivyo, Wizara imeshaundwa, tuiachie Wizara ya Vijana waendelee na mambo yao waweke mipango yao, mambo haya hizi hela nyingi baadaye kuwajibisha mtu inakuja kuwa vigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo ninaomba niishie hapo na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Yohana Stephen Msita atafuatiwa na Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu. Mheshimiwa Lulu Guyo Mwacha, ajiandae.

**MHE. YOHANA S. MSITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Dkt. Mwigu Lamek Nchemba kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya mapato na matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa namna ambavyo ametupa uzima na uhai mpaka dakika hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza ninaomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya ndani ya nchi yetu. Nimpongeze sana Rais huyu, hakika amefanya mambo makubwa, amefanya mambo mengi na sisi Wabunge wote tunajivunia kuwa na Rais wa aina yake Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pili, ninaomba nimpongeze Makamu wa Rais Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuendelea kuchapa kazi akimsaidia Mheshimiwa Rais kwenye nchi yetu. Anafanya kazi kubwa na anastahili kupongezwa. Mtu wa tatu ninaomba nimpongeze mwenye hotuba yake, Waziri wetu Mkuu Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, zao la Wanasingida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu ameanza kazi vizuri. Tangu alipoitoa hotuba yake hapa alipoteuliwa alisema anakwenda na fyekeo na rato na kwa kweli ameanza ziara akizungukia mikoa mbalimbali. Tumeona namna ambavyo ziara zake zimeleta tija sana kwenye nchi yetu kwa namna ambavyo ametatua migogoro. Amekutana na changamoto nyingi sana na kuzitafutia majawabu. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni hotuba nzuri sana, imetupa matumaini imetupa mwanga mzuri kuonyesha namna gani tunakwenda sasa kufanikiwa katika mambo mengi sana kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze na suala la barabara. Nchi yoyote duniani ili iweze kufanikiwa lazima ihakikishe miundombinu ya barabara iko vizuri kweli kweli. Kama tunataka kwenda kwenye uchumi ule wa kati wa juu ni lazima tuhakikishe miundobinu ya barabara iko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunashuhudia kumekuwepo na mafuriko ya mvua, mvua ni kubwa sana nchini kwetu na kwa kweli ukipita barabara nyingi hizi za lami za *TANROAD* utaona namna gani ambavyo zimechimbika sana kwa kiwango kikubwa. Matokeo yake kwa kweli imesababisha magari, maroli yamekuwa yakianguka yakipata ajali na wakati mwingine mabasi yakipata ajali. Sasa tuna kazi kubwa sana ya kufanya ukarabati wa hizi barabara ili nchi yetu iweze kupitika kirahisi, iwe mchana au usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu la Itigi tunayo Barabara ndefu inayoanzia Mkiwa – Itigi – Mitundu – Rungwa kuelekea Makongolosi - Chunya. Hii barabara ni kiungo muhimu sana kwenye nchi yetu. Imekuwepo kwenye ahadi kwa muda mrefu. Sasa tunazungumzia vipi kwenda kutekeleza hii Dira ya 2050 bila kuhakikisha kuwa miundobinu ya barabara inaweza kupitika wakati wote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ni kiungo muhimu katika uchumi wetu, barabara ni ajira, barabara ni kama ni kama mshipipo wa damu kwenye mwili wa binadamu. Hii barabara imekuwa ni barabara muhimu kwa sababu inaunganisha mikoa takriban minne ya Songwe, Mbeya, Tabora, Singida na mpaka

hapa Dodoma. Leo barabara hii inaweza ikasaidia sana usafiri na wasafirishaji kutoka Zambia, Malawi na kadhalika. Kusini yote ikapita hii Barabara ya kutoka Chunya – Makongorosi – Rungwa kuja Itigi na kuja mpaka hapa Dodoma. Hii barabara isipokamilika maana yake tutakuwa tunajichelewesha katika zile mbio za kwenda kutafuta ule uchumi mzuri wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumza barabara huwezi kuacha kuitaja kutaja barabara za *TARURA* ambazo kwa kweli ndizo nyingi; maana barabara za lami ni kama kilomita 14,000 mpaka 15,000 ambazo zimejengwa kwa kiwango cha lami, lakini barabara za vumbi ziko takriban kilomita 140,000. Unaweza kuona kwenye hizi barabara za *TARURA* asilimia mbili hadi tatu labda ndizo zenye lami. Kwa hiyo tuna kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Waheshimiwa Wabunge ni lazima tuhakikishe kuwa fedha zinaongezeka kweli kweli ili tuweze kutatua changamoto za barabara ambazo kwa kweli kwa kiwango kikubwa zimeathiriwa sana na mvua nyingi ambazo zimeendelea kunyesha. Kwa hiyo tuendelee kuongeza fedha kwenye kwa *TARURA* ili barabara zetu ziweze kukarabatiwa na zipitike wakati wote, ziweze kuchochea uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoka kwenye Wilaya ya Manyoni. Sasa Wilaya ile ya Manyoni ina mapori matatu; mapori ya Rungwa, Muhesi na Kizigo. Mapori haya yana hifadhi Wanyama, lakini mle ndani pia kuna madini na vilevile kuna mazao ya misitu, kwa maana ambayo na kadhalika. Sasa leo tunavyozungumza Jimbo langu la Itigi lina wakazi takribani laki mbili elfu kumi na sita; linatosha kabisa kuwa wilaya. Hata hivyo, kwa sababu ya pori hili limekuwa ni kubwa sana matokeo yake watu wengi sana wanashindwa kujitanua kuendesha shughuli zao za ufugaji na zao za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wito wangu kwa Serikali mapori haya ambayo yana rasilimali kubwa, yana rasilimali nyingi ya nchi tunaweza kutafuta namna bora ya kuhakikisha kwamba tunasogeza ule mpaka wa *game reserve* ili uweze kutanua wigo. Hii ni kwa sababu tangu wakati mapori haya yanatengwa idadi ya watu ilikuwa ndogo sana. Leo tunavyozungumza watu wako

karibu laki mbili na kitu. Iko haja sasa ya angalau tuongeze ule mpaka angalau kilomita tano ili tuweze kuwasaidia wafugaji wakulima wakazi waweze kujiendesha na shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. YOHANA S. MSITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, tuna changamoto kubwa sana pia ya *NIDA* na vyeti vya kuzaliwa, wananchi wetu kule kijijini wanapata changamoto kubwa sana. Muda mwingi wakienda mahali ambapo wanahitaji kupatiwa *NIDA* wanaambiwa mtandao hakuna; nenda rudi mtandao hakuna. Huu mtandao huwa unasumbua kwenye kipindi ambacho watu wanahitaji *NIDA* na vyeti vya kuzaliwa. Isije ikawa kuna wakati watu wamejaribu kutengeneza kamradi, kwamba waweze kuwahudumia wananchi wapewe chochote. Suala la *NIDA* na vyeti vya kuzaliwa limekuwa changamoto sana.

Mheshimiwa mwenyekiti ninaomba kuunga mkono hoja. Ninawashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu atafuatiwa na Mheshimiwa Lulu Guyo Mwacha.

**MHE. DOTTO J. BAHEMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nipate nafasi kuchangia kwenye hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nianze kusema kwamba leo ni mara ya pili, ninapata nafasi ya kuchangia Bungeni, lakini ni mara ya kwanza tangu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametimiza siku 100 tangu ameapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumpongeza kwa sababu alikuja Ngara kutuomba wananchi wa Jimbo la Ngara tumchague kuwa Rais wetu na akatuahidi kuna mambo ambayo angetufanyia katika kipindi cha siku 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale mambo ambayo aliahidi katika Jimbo la Ngara na yale ambayo yanawagusa moja kwa moja wananchi wa Ngara yote tayari Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekwishayatimiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza alituahidi mikopo sisi vijana pamoja na wajasiriamali; tayari zile fedha zimekwisha fika na tayari Maofisa Maendeleo ya Jamii wako kwenye kata wanatoa elimu na baadhi ya maombi tayari yameshaanza kutumwa na vijana kwa ajili ya kuomba mikopo ya fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi alituahidi kwamba atatuletea walimu wapya 7,000 nchi nzima na sisi Jimbo la Ngara tayari tumekwishapokea walimu 34 wa shule za sekondari; na Mungu akipenda mwezi Aprili tutapokea walimu wengine wa shule za msingi kuhusu watumishi alituahidi watumishi 5,000 nchi nzima. Sisi Jimbo la Ngara tayari tumepokea watumishi 64. Kuhusu bima za afya aliahidi vilevile na mpaka leo tayari tumepokea orodha ya wanufaika wale wenye mahitaji maalum zaidi ya 7,000, ambao tumepewa kwa awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakwenda kuipitia kwa ajili ya uhakiki na Mungu akipenda tutakuja kuongezewa nyingine. Hayo ni miongoni mwa mambo ambayo aliahidi Mheshimiwa Rais kutufanyia sisi wananchi wa Jimbo la Ngara ndani ya zile siku 100. Kwa hiyo tunamshukuru sana na tunampongeza. Tunazidi kumwombea kwa Mwenyezi Mungu ampe nguvu, Tanzania bado inamtegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo amekuwa akifanya kazi zake. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wengine wengi wameongea na wamepongeza jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya ziara zake na kwa jinsi

ambavyo ameenda hadi kwa wananchi wenye mahitaji ya chini kwa ajili ya kwenda kuwasikiliza na amekuwa akitoa suluhisho ya matatizo yao pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafurahisha na ndiyo maana tunampongeza; lakini ninaomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wengine wote ambao walisema kwamba ni vizuri, lakini haikutakiwa kuwa hivyo. Kule kote ambako Mheshimiwa Waziri Mkuu anakwenda kuna viongozi mpaka ngazi za chini kabisa na sisi wote tumekuwa ni mashahidi. Kumekuwa tukiona zile kero ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu anazisikiliza na kuzitatua. Ni kero nyingine ambazo nyingine bado ziko katika *level* ambazo zingeweza kufanyiwa kazi kule kule chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunapopongeza ina maana ni kwamba tunawapongeza wale walioko kule chini, kwamba wao hawafanyi kazi yao vizuri. Ndiyo maana Waziri Mkuu akienda akifika sehemu watu wanashangilia. Kwa hiyo tulikuwa tunaomba kwamba Serikali iangalie namna gani ya kulifanya hili kuwa suluhisho la kudumu. Tusitegemee kiongozi wa juu kutoka juu kuja chini katika Wilaya ya Ngara kuja kusikiliza kero za wananchi ilihali kuna viongozi kuanzia ngazi ya kijiji hadi ngazi ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tutaifanya pale ambapo tutarudia yale ambayo yalishaahidiwa nyuma; kwamba Serikali ina mpango wa kutengeneza mfumo mzuri wa kwenda kuratibu utendaji kazi wa wale watu ambao wameajiriwa, kuanzia ngazi ya Waziri hadi kwa yule wa chini; hatuoni kama yanatekelezwa kwa jinsi ambavyo tunaona. Kama yanatekelezwa basi yanatekelezwa katika hali ambayo si ya wazi. Kwa hiyo tunaomba wafanyike kwa wazi ili wananchi waone kwamba wameiweka Serikali kwa ajili ya kuwasikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika hotuba wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, wamezungumza namna gani nyingine ambayo watakuwa wanaitumia kwa ajili ya kusikiliza kero za wananchi. Wamezungumza kuhusu mfumo wa *e-Mrejesho*, pia wamezungumza mfumo wa barua pepe. Hata hivyo, bado kuna maeneo mengine mengi ambayo wananchi hawawezi waka-

*access* hii mifumo. Kwa mfano, mfumo wa barua pepe ukienda Ngara kule yaani kusema wananchi watume malalamiko kwa *email,* ni wachache sana ambao wanaweza wakafikia hatua hii. Kwa hiyo, ninaomba tuangalie basi angalau kama inawezekana wale viongozi ambao wako kule chini wawe wanafanya kwa namna ambayo wananchi wanapata suluhisho la hapo kwa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Ngara waliyofanyiwa ni mengi na ndiyo maana wamekuwa watiifu sana kwa Serikali, wamekuwa na imani kubwa sana kwa Serikali yao, na wamekuwa na imani kubwa sana kwa Chama Cha Mapinduzi kwa sababu yaliyofanyika ni mengi sana na sisi tunaishukuru sana Serikali, lakini kadri siku zinavyozidi kwenda tunaanza kuvunjika moyo sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavunjika moyo kwa sababu kuna mambo mengine mengi ambayo tumeyaomba kwa muda mrefu, lakini mpaka sasa hivi yamekuwa hayatekelezeki. Ni tofauti na vile ambavyo sisi tunatoa kuipa Serikali na Chama Cha Mapinduzi, wao siyo yale ambayo wanayarejesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi katika Jimbo la Ngara leo, hata ukija kufanya mkutano wa kampeni, ukasema Jumapili saa tatu kamili asubuhi unataka watu wajae uwanjani, watajaa uwanjani, watakuja kukusikiliza na watapiga kura nyingi kwa wingi. Utamaliza utaenda katika wilaya ngumu ambazo lazima ukusanye watu jioni; sisi Ngara hatuko hivyo. Ukija saa moja asubuhi tunakusanyika uwanjani, tunakupigia kura unaondoka zako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitegemea basi angalau kwa haya ambayo tunajitolea kwetu sisi wananchi wa Jimbo la Ngara, basi na Serikali irudishe. Haiwezekani sisi tumeomba barabara tu, kuna barabara moja ambayo imekuwa ikiombwa, mimi ni Mbunge wa saba ambaye ninaizungumza hii barabara. Hii barabara imeanza kuombwa tangu Wabunge wengine sita waliopita nyuma yangu. Kila Mbunge amekuwa akizungumza barabara hii hapa Bungeni zaidi ya mara tatu. Mimi leo ni mwezi

wangu wa nne nikiwa Mbunge, lakini leo ninazungumza kwa mara ya tatu kuhusu ile barabara. Barabara ya kutoka Nyakahura kupita Rulenge mpaka Murugarama, ijengwe kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile barabara itakapojengwa kwa kiwango cha lami, kata tisa zitanufaika moja kwa moja kwa sababu zinapitiwa na ile barabara moja kwa moja. Pia, ile barabara itaturahisishia sisi watu wengine ambao tunatoka huku katikati kwenda Nchi ya Burundi, inapitika kirahisi kuliko kupita katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba, kwa sababu hii ni hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, sisi watu wa Ngara kwa sasa hivi, kitu cha kwanza ambacho tungependa kusikiliza watufanyie Serikali watujengee hii Barabara ya kutoka Nyakahura kupita Rulenge mpaka Murugarama. Sababu kubwa imekuwa ikisababisha hii barabara, hata viongozi wa Serikali wakija kufanya ziara katika Mkoa wa Kagera hawafiki Ngara, wanatuambia watu wa Ngara njooni Biharamulo, wanatuambia watu wa Ngara twendeni tukakutane Karagwe, Ngara hawafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata juzi amekuja Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi hakufika Ngara, tumeambiwa Ngara njooni Biharamulo kwa sababu ile barabara haipitiki, hawezi kufika. Wakati wa kampeni alikuja mgombea mwenza Dkt. Emmanuel Nchimbi, Makamu wa Rais, alitumia helkopta hakutumia barabara, alikuja akakaa nusu saa akaondoka kwa sababu kule hakufikiki. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba hii barabara itoshe kusema kwamba wananchi wa Ngara tumeshazungumza vya kutosha, sasa inatosha tunaomba yaende kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tuna mradi wetu wa Kabanga *Nickel* ambao ni wa uchimbaji wa *nickel*. Tunashukuru Mungu tumeona mambo mengi yanaendelea na hata juzi nimezungumza na Mheshimiwa Waziri wa Madini ameniahidi kwamba tayari ule mradi unakwenda *take-off*. Kwa hiyo, tunaomba ile ahadi ambayo Mheshimiwa Waziri ameniahidi na ambayo hata Mheshimiwa Rais alizungumza katika hotuba yake,

tunaomba kwamba chochote kisibadilike, tunaomba ule mradi uende u-*take-off* kama ambavyo Waziri ametuaahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Ngara kuna mambo mengi na kuna matatizo mengi sana. Vijana wengi wa Ngara hawana ajira na kuna changamoto nyingi sana ambazo zinatukabili wananchi wa Jimbo la Ngara. Miradi mingine haipo lakini tukipata angalau ule mradi, tunaamini kwamba kuna baadhi ya vitu vingine vingi vitakwenda kufanikiwa. Tutapata zahanati ninajua na vijana wetu wengi watapata ajira. Kwa hiyo, ninaomba tusipate *story* nyingine yoyote katikati hapo kwamba huu mradi kuna namna nyingine. Tunaomba ufanyike kama ambavyo Serikali imeahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji, katika Mkoa wa Kagera wilaya nyingine zinaungwa na maji kutoka katika Ziwa Victoria, lakini sisi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DOTTO J. BAHEMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumalizia, dakika moja. Sisi jimbo letu la Ngara hatuna chanzo cha maji cha uhakika, ila tuna mradi ambao tayari umekwishasanifiwa wa kutoka Mto Ruvubu ambao utakwenda kupeleka maji katika kata tano. Ukipeleka maji katika kata tano, changamoto ya uhaba wa maji katika Jimbo la Ngara itakwenda kuwa ni historia katika kata za upande huu mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba haya mambo ambayo tumeomba mambo matatu: Barabara yetu ya Nyakahura, Mradi wa Kabanga *Nickel* na huu Mradi wa Maji wa Mto Ruvubu uende ukafanyiwe kazi na Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. DOTTO J. BAHEMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Lulu Guyo Mwacha.

**MHE. LULU G. MWACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa ilii niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Awali ya yote ninapenda sana kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima na kibali, nguvu na afya ya kuniwezesha leo kusimama katika Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan na Amiri Jeshi Mkuu pamoja na chama changu kwa kuniamini na kuniteua na kupendekeza jina langu niwe kati ya wagombea wa Ubunge katika kundi la vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa pia ninapenda kuwashukuru vijana wa Taifa hili, vijana wa Chama Cha Mapinduzi walioniamini na kunipigia kura za kishindo ili nikawe sauti yao katika Bunge hili Tukufu. Niwaahidi kwa moyo wa dhati kabisa nitaenda kuwatumikia kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia tena kwa kuipongeza Serikali yangu, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa iliyofanyika kwa kipindi cha siku 100 za Dkt. Samia Suluhu Hassan, yamefanyika mambo makubwa na mambo ambayo yameweza kutoa Taifa letu kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine. Mambo makubwa katika kila sekta tumeona sekta ya nishati, sekta ya maji, sekta ya afya na sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na maboresho na maendeleo ya miradi mikubwa ya kimkakati ambayo imeenda kuchangia katika Taifa letu kuendelea kupiga hatua ya kimaendeleo. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba kwa hotuba yake yenye mashiko ambayo

nayo imeenda kuonyesha dira ambayo tunajua Taifa letu linapotaka kuelekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita katika maeneo matatu na maeneo haya husSo kwenye kundi letu la vijana. Katika sekta ya elimu, niipongeze sana Serikali kwa juhudi zake kubwa za kuhakikisha vijana wetu kuanzia shule za awali na shule za sekondari, Serikali imejitahidi sana katika ujenzi wa shule, lakini pia kumekuwa na ajira nyingi ambazo walimu wameajiriwa ambao wataenda kuwasaidia vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sana sana Serikali pamoja na jitihada nyingi sana katika sekta ya elimu, ninaomba sana waendelee kuwaangalia vijana hawa, waendelee kwenye ukarabati wa shule, waendelee kuongeza vifaa ambavyo vitawasaidia vijana wetu. Japokuwa kumekuwa na ajira hizo za walimu, bado hazijatosheleza, bado kuna uhaba kiasi wa walimu. Kwa hiyo, ningeomba sana Serikali yetu Tukufu ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iangalie suala zima la elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza hapo, ilikuwa ninaomba sana kwenye mitaala yetu liongezeke suala zima la elimu ya fedha. Kuna Mbunge mmoja aliongelea suala la elimu ya fedha, lakini kuna Mbunge mwingine alimpiga taarifa kwamba tumeanzisha elimu ya ujasiriamali. Elimu ya ujasiriamali na elimu ya fedha ni vitu viwili tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya fedha inaenda kumsaidia kijana kuanzia akiwa mdogo kuwa anajua namna ya kuweka matumizi yake, namna ya uwekezaji na namna ya kuweka akiba, lakini elimu ya ujasiriamali inaenda kumsaidia kijana aweze kuwa mbunifu na kuanzisha biashara itakayozidi kumjenga. Kwa hiyo, ni elimu mbili tofauti. Ninaomba sana kusisitiza kwamba elimu ya fedha ni muhimu sana kuanzia vijana wetu wakiwa wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende pia kwenye suala la utolewaji wa mikopo. Nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan, hii shilingi bilioni 200 aliyoitoa ninaomba sana sana kwa sababu hii ni fursa kubwa kwetu sisi vijana wa Taifa letu, iende ikawasaidie vijana ikawe na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa mikopo ikitolewa kunakuwa na mlolongo wa vitu vingi sana ambavyo vinaenda kukwamisha vijana wasiweze kupata fedha hizo. Tunaomba wapunguze masharti vijana wapate kwa unafuu. Pia, niwaombe vijana wa Taifa letu mkipewa mikopo hii mrejeshe. Mkiaminiwa na ninyi muaminike ili vijana wengine nao waweze kuaminika kwa wakati mwingine muweze kurejesha fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la uvuvi vijana wamekuwa wanapata sana changamoto pale wanapokwenda kuanzisha vizimba vya ufugaji wa samaki. Kumekuwa na mlolongo wa vibali vingi sana ambavyo vinahitajika, ikiwa mojawapo ni kibali cha *NEMC*, lakini pia kuna kibali cha uvuvi ambacho kinatoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kuna kibali pia kingine kinachotoka kijiji, kuna taratibu ndefu na mchakato mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye hivi vibali kuna fedha ambazo zinatakiwa kutolewa. Ikiwa lengo letu ni kumsaidia kijana, kuna hizi fedha nyingi bado zinatolewa, anakuwa kabla hajafikisha malengo fedha nyingi zimeshatumika hapo tunazidi kumkwamisha kijana asiweze kufikia malengo yake ya kujiajiri. Kwa hiyo, niwaombe sana Serikali wazidi kupunguza hii michakato mingi ambayo inamfanya kijana wa Kitanzania aende kukata tamaa hata kabla hajaanzisha biashara ambayo alikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala zima la afya, niipongeze sana Serikali yangu kwa kuendelea kujali afya ya Mtanzania. Bila afya hakuwezi kuwa na maendeleo. Kwenye suala la Bima ya Afya kwa Wote ninaiomba sana Serikali yangu, kwanza niipongeze sana kwa sababu hili suala litaenda kusaidia watu wengi sana kutoka kwenye kadhia ya malipo ambayo inasababisha saa nyingine wanakosa huduma iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana suala la bima liende kwa kasi ili liweze kuwafikia na watu wengi hususan wale watu wa

vijijini, wengi bado haijawafikia. Pia, kumekuwa na ujenzi na ukarabati wa vituo vyetu vya afya, ninaomba sana viendelee mpaka kwenye vijiji ili mwananchi aweze kupata huduma bora ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, niweze kusema vijana ni nguvu kazi ya Taifa na ni msingi wa maendeleo ya baadaye; tukiwapa kipaumbele leo tutalihakikishia Taifa letu kesho iliyo imara na bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe sana Serikali yangu iwajali sana vijana. Ninasisitiza sana mambo yanayokwamisha vijana kupata mikopo, michakato mirefu na vibali ambavyo vingine havina msingi. Niwaombe sana Serikali ipunguze. Itaenda kumsaidia kijana kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninashukuru sana kwa nafasi na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa michango kwa siku ya leo. Hatukuwamaliza wote, lakini wale ambao wamekosa nafasi leo, basi wataanza kesho asubuhi na tutoe angalizo, ukishakuwa kwenye orodha ya wachangiaji hakikisha unakuwa hapa na kama umepata udhuru toa taarifa mapema.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaahirisha Bunge mpaka kesho siku ya Ijumaa tarehe 10 Aprili, 2026, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.52 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 10 Aprili, 2026, Saa Tatu Asubuhi)*